ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.

20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame Makaazi, Maji na Nishati/	Naibu Waziri wa Ardhi, Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake

42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
56.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
57.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
58.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
61.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
62.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe

69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Nane - Tarehe 27 Mei, 2014

(Saa 3:00 asubuhi kikao kilianza)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora kwa mwaka 2014/2015.

Mhe. Shadya Moh'd Suleiman (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa naomba kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora kwa mwaka 2014/2015.

Mhe. Fatma Mbarouk Said (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika) (*PAC*): Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*), naomba kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*) kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mwaka 2014/2015.

MASWALI NA MAJIBU

Nam.1

Mpango wa Kusaidia Wanafunzi Wanaofeli *F.II* na *F.IV*

Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Aliuliza:-

Idadi ya wanafunzi wanaofeli kidato cha pili *(Form Two)* na kidato cha nne *(Form Four)* imekuwa ikiongezeka kila mwaka wanafunzi hao wanapofanya mitihani yao na kupelekea wanafunzi wengi kubaki mitaani bila ya muelekeo wowote wa elimu katika maisha yao, hivyo kusababisha ongezeko la vijana wasio na ajira Zanzibar.

(a) Serikali ina mpango gani wa kuanzisha '*program'* maalum hasa za ufundi kwa wanafunzi waliofeli mitihani yao ya kidato cha pili na ile ya kidato cha nne.

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza na kuboresha vyuo vya amali na kuweka mazingira rahisi kwa wanafunzi kama hao kujiunga na vyuo hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mwakilishi swali lake namba 1 lenye sehemu (a) na (b). Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa idadi ya wanafunzi wanaomaliza masomo ya Kidato cha Pili na Kidato Nne wanaongezeka kila mwaka, ingawa asilimia ya wanafunzi wanaofaulu na kuchaguliwa kuendelea na masomo ya Kidato cha Tatu na Kidato cha Tano inaongezeka. Hata hivyo wengi wa wanafunzi wanaomaliza masomo hawana ujuzi wa kutosha kuwawezesha kuajiriwa au kujiajiri, na hivyo idadi kubwa ya vijana wasiokuwa na ajira inaongezeka. Pia ninakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa vijana hawa wanahitaji kupatiwa mafunzo ya ufundi wa amali ili waweze kujiajiri wenyewe na kuchangia katika kuinua uchumi wa nchi yetu. Baada ya maelezo hayo, napenda kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

a) Wizara imeweka mkazo katika elimu ya ufundi na amali ili vijana kupatiwa maarifa na ujuzi utakaowawezesha kujiajiri wenyewe au kuajiriwa. Wizara imeanzisha mradi maalum wa Uimarishaji wa Elimu ya Ufundi kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo Skuli ya Sekondari ya Kengeja na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia na kuzipatia vifaa vya ufundi ili wanafunzi wengi zaidi waweze kupata mafunzo ya Ufundi na Amali kulingana na mahitaji ya soko la ajira. Pia Wizara imeanzisha programu ya Elimu Mbadala na amali ili kuwapatia mafunzo ya amali vijana walioacha masomo njiani na waliomaliza masomo katika Kidato cha Pili na Kidato cha Nne. Awamu ya kwanza ya mradi huu, imeonesha mafanikio mazuri kwani vijana wengi wameweza kupata ajira na wengine wamejiajiri wenyewe.

b) Kutokana na mafanikio ya awamu ya kwanza ya mradi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika, imeanzisha awamu ya pili ya Mradi wa Elimu Mbadala na Amali, ambapo Vituo viwili vipya vya Mafunzo ya Amali, na Vituo viwili vya Elimu Mbadala vitajengwa katika sehemu mbali mbali za nchi yetu. Ujenzi wa Vituo hivyo unatarajiwa kuanza katika mwaka wa 2014/2015. Kujengwa kwa vituo hivyo kutasaidia sana kueneza mafunzo ya kazi za amali katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba wana mpango wa kuongeza vyuo hivi vya amali ili kuona kwamba vijana wengi wanapata elimu hii ya amali.

a) Kwa hivi sasa Zanzibar tuna vyuo vingapi vya amali na vipo katika wilaya zipi za Zanzibar.
b) Kuna suala la mikopo baada ya kumaliza *course* ya miaka mitatu. Je, suala hili limefikia wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru sana, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

a) Kwa hivi sasa Mhe. Naibu Spika, tuna kituo cha elimu mbadala kimoja Rahaleo lakini tuna vituo vya amali vitatu; Vitongoji, Mkokotoni na Mwanakwerekwe.

b) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuwa kawaida huu mkopo vijana wenyewe wanapomaliza mafunzo yao wanatakiwa waombe na mpaka hivi ni kikundi kimoja tu ambacho kimeomba, maana yake wanatakiwa kuji-*organize* pamoja na kufanya vikundi. Hivyo kuna kikundi kimoja tu ambacho kimeomba mpaka hivi sasa. Na jambo ambalo tumeligundua kwao ni kuwa wana ujuzi wa mafunzo ya amali lakini hawana ujuzi wa biashara. Kwa hivyo tuna mtaalamu ambaye amebobea katika mambo haya ya amali anaitwa Dkt. Aggra Awal anatoa mafunzo pale pale chuoni kwanza mpaka atakapoona tayari wanaweza sasa watapewa hizo pesa, pesa zipo na watapewa Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

a) Serikali ina mpango gani wa kuanzisha viwanda vidogo vidogo na kampuni za ujenzi ili vijana wanaomaliza katika vyuo vya amali waweze kunufaika na ajira baada ya kuhitimu na kubaki katika majumba.

b) Kwa nini serikali hawaweki kipaumbele kwa kampuni za ujenzi wa nyumbani ili ziweze kuwanufaisha vijana wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake (a) na (b). Mhe. Naibu Spika, swali la (b) naomba nikiri kwamba sikulisikia uzuri.

a) Suala la serikali kuanzisha viwanda vidogo vidogo hilo sidhani kama lipo katika Wizara ya Elimu.
La pili naomba Mhe. Naibu Spika, naomba aliulize sikumsikia vizuri.

Mhe. Naibu Spika: Rejea swali la (b).

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana ninafikiri hata la mwanzo hakulisikia. Naona nianze la mwanzo vile vile.

a) Serikali ina mpango gani wa kuanzisha viwanda vidogo vidogo na kampuni za ujenzi ili kunufaisha vijana wetu baada ya kumaliza masomo hayo ili wapate ajira badala ya kubaki nyumbani.

b) Kwa nini serikali haiweki kipaumbele kwa kampuni za ujenzi za nyumbani ili ziweze kunufaisha vijana wengi wanaomaliza masomo katika vyuo vya amali.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake (a) na (b) ambayo yote yana mtiririko mmoja.

Suala la serikali kuanzisha viwanda au makampuni si suala ambalo linahusu Wizara ya Elimu. Suala hilo ninadhani linaweza likawa lipo katika Wizara ya Biashara, Viwanda, Masoko na Utalii.

Kwa hivyo sina jibu la kuanzisha vikampuni au...

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nyongeza lenye (a) na (b) la Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama hivi ifuatavyo.

Kwanza nimshukuru Mhe. Naibu Waziri wa Elimu kwa maelezo yake sahihi. Baada ya hayo nieleze kwamba,

a) Mhe. Naibu Spika, serikali imejitoa kabisa katika masuala mazima ya kufanya biashara. Na jambo ambalo imelifanya serikali ni kujenga mazingira mazuri kwa ajili ya wafanyabiashara waweze kuanzisha viwanda vidogo vidogo. Na hapa niweze kutoa wito hususan kwa Mhe. Jaku na wafanyabiashara wenzake wafanye shughuli hiyo, wasishughulike sana na zile biashara za uagizaji tu kwa kiasi fulani zimepitwa na wakati, na hivi sasa ni wakati hasa wa kufikiria namna ya kuanzisha viwanda vidogo vidogo ambavyo vitatokana na raslimali za ndani.

b) Lakini vile vile la kuanzisha makampuni ya ujenzi. Serikali pia imeweka utaratibu mzuri na kuhamasisha kabisa watu mbali mbali kuanzisha kampuni za ujenzi pamoja na kukaribisha kampuni za ujenzi kutoka nje ya nchi ili kushirikiana na nchi yetu katika kuhakikisha kwamba majenzi ya aina zote yanafanikiwa katika nchi yetu.

Kuhusu kutoa kipaumbele kwa wananchi katika kazi za hapa ndani, ndio inavyofanya serikali lakini pale ambapo wananchi wetu au kampuni za ndani zinashindwa kufanya shughuli fulani ndio maana tunapendelea sana kutoa nafasi hizo kwa kampuni za nje ili shughuli zifanyike. Lakini kipaumbele namba moja kinatolewa kwa kampuni zetu za ndani, pale inaposhindwa ndio mara nyingi hupewa kampuni za nje.

Na wakati mwengine pia kampuni zetu za ndani zinakuwa zina upungufu wa kutekeleza wajibu kama inavyotakiwa, ndio maana zinavunja moyo jitihada hizo za serikali katika kupewa kipaumbele. Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa swali la mwisho la nyongeza, Mhe. Mohammed Mbwana Hamad.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, ninashukuru. Napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa Serikali ya Zanzibar ilianzisha vyuo mbali mbali kwa ajili ya kuwaimarisha vijana wanapomaliza masomo waweze kujiajiri kama vile Mikunguni, Karume na kadhalika. Lakini pia hivi sasa serikali kupitia Wizara ya Elimu imeanzisha vyuo vya amali kama alivyovitaja Mkokotoni na kwengineko.

Je, Mhe. Naibu Spika, vyuo hivi mumeviwezeshaje kivifaa vya kisasa ili vijana watakapotoka katika masomo yao waweze kujitegemea kiajira bila ya kuitegemea serikali. Mhe. Naibu Spika, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru sana naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Kama nilivyozungumza katika jibu langu mama kama mbali ya vituo hivi ambavyo tumevianzisha na tunavyotarajia kuviendeleza au kujenga upya, lakini pia tunaimarisha vile vyuo ambavyo tumevianzisha na vina wanafunzi tayari. Kitu kimoja ambacho nilisema hivi sasa vipo katika zoezi hilo na tayari tumewapatia pesa ni Chuo cha Kengeja na Chuo cha Sayansi cha Karume.

Kwa hivyo na hivyo vyuo vyengine vitafuata kadri ya hali ya uwezo wa wizara na serikali tutakavyopata.

Nam.15

Kupandishwa Kodi Kwa Nyumba za Michenzani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:-**

Hivi karibuni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepandisha viwango vya kodi ya nyumba za maendeleo za Michenzani, ambazo malengo ya kimapinduzi ya kujengwa kwake ni kuwasaidia wananchi wanyonge waweze kumudu kuishi katika makaazi bora.

(a) Je, tathmini ipi ya kitaalamu imefanywa kujua uwezo wa wananchi wanyonge wanaoishi katika nyumba hizo wa kulipa viwango hivyo vya juu vya kodi.

(b) Je, kwa nini Serikali imepandisha viwango vya kodi bila ya kuzifanyia ukarabati na kuziweka katika hali bora.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 15 (a), (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa napenda ieleweke kuwa Serikalli imepandisha kodi za nyumba zake ikiwemo nyumba za Maendeleo Michenzani kwa nia safi kabisa.

Pia ieleweke kuwa Serikali kwa muda mrefu haijafanya mapitio ya kodi za nyumba zake tokea mwaka 2003, ni zaidi ya miaka kumi...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa Naibu Waziri sauti haisikilizani, sogea kwenye *microphone*.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Pia ieleweke kuwa Serikali kwa muda mrefu haijafanya mapitio ya kodi za nyumba zake tokea mwaka 2003, ni zaidi ya miaka kumi. Kiwango cha kodi kilichokuwa kinalipwa kilikuwa ni kidogo sana ambacho kwa sasa kimeshapitwa na wakati.

Kodi iliyokuwa ikilipwa kwa fleti za vyumba viwili ilikuwa ni Shillingi Elfu tisa (Tsh. 9, 0000/=) na vyumba vitatu ilikuwa ni TSh. 11,000/=. Na kwa sasa fleti ya vyumba viwili ni shilingi 22,500/= na fleti ya vyumba vitatu ni shilingi 30,000/=.

Mhe. Naibu Spika, nia ya serikali ni kuona nyumba zake zote zinafanyiwa matengenezo yanayofaa na kwa wakati muafaka ili kuondoa tatizo hilo na hali mbaya inayojitokeza katika majengo hayo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, nyumba hizo zinakabiliwa na matatizo mengi ikiwemo uchakavu, ukosefu wa huduma muhimu kama vile maji, mifumo ya maji machafu na kukwama kwa sehemu za karo.

Kwa nini serikali inakusanya kodi bila ya kuondoa matatizo yanayokabili nyumba hizo. Hilo moja.

La pili, serikali ina mpango gani wa nyumba zilizotaifishwa ambazo zimekabiliwa na ukosefu na nyengine kuhatarisha kuanguka. Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha nyumba hizo wenyewe.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, ahsante naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kwanza nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli kwamba kuna baadhi ya nyumba za Michenzani au za maendeleo za serikali zipo katika hali ngumu ya uchakavu, lakini lengo la serikali ni kuzifanyia matengenezo nyumba hizo kama nilivyoeleza hapo awali lakini bado hali ya fedha haijaruhusu kutokana na hali ya kibajeti.

Lakini pindi hali ya fedha itakaporuhusu basi nia na madhumuni ya serikali ni kuzifanyia matengenezo nyumba hizo kama inavyostahiki.

Swali la pili naomba Mhe. Mwakilishi alirejee, sikulifahamu vizuri.

Mhe. Naibu Spika: Anasema kwamba ziko nyumba zilitaifishwa muda mrefu na serikali, lakini hazifanyiwi kazi na zinakaribia kuanguka. Je, mna mpango gani juu ya hizo? Mtawarejeshea wenyewe?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Naibu Spika, ni kweli kuna baadhi ya nyumba zimetaifishwa na serikali, lakini lengo la serikali ni kuzifanyia matengenezo nyumba hizo, sio kuziacha zikaendelea katika hali ya maharibiko; ni kuzifanyia matengenezo na baadaye kuwapa wananchi wa Zanzibar ili wanufaike na makaazi ya nyumba zile.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, ningeomba kutoa maelezo ya nyongeza ya swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo. Nia na dhamira ya serikali ya kutaifisha nyumba zile ambazo zilitaifishwa wakati huo zitaendelea kuwa mali ya serikali na hazitorudishwa kwa wenyewe.

Dhamira ya serikali ni kutengeneza nyumba hizo ili ziwe katika hali nzuri zikalike na ndio maana serikali hivi sasa imo katika mchakato wa kuanzisha Shirika la Nyumba, kwa nia na madhumuni ya kuzitengeneza nyumba zote ambazo ziko katika hali mbaya, zitengenezwe ili ziwe nzuri na wananchi wetu waweze kukaa katika nyumba hizo kwa kupangishwa ili ziweze kutoa fedha, tutazidi kuziangalia kila siku ili kuepukana na haya matatizo yanayojitokeza ya uharibikaji na usumbufu mwengine ambao wananchi wetu wanapata. *(Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa dhamira ya serikali hii ya Mapinduzi kujengwa nyumba zile ni kuwasaidia wanyonge ili waweze kuishi katika makaazi bora. Napenda nimuulize Mhe. Waziri.

Je, ni watu wangapi ambao wenye uwezo waliopewa nyumba zile na wizara yake?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Naibu Spika, lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwagaia au kuwapa wananchi wanyonge au wananchi wote wa Zanzibar makaazi stahiki. Kwa hivyo, nyumba za Maendeleo za Serikali kila mwananchi wa Zanzibar anastahiki kupewa nyumba hiyo, pindi pale atakapoomba na kufuata masharti yanayostahiki. Kwa hivyo, wananchi wanyonge wanaangaliwa, wananchi wa kawaida wanaangaliwa. Kwa sababu wapo wale ambao wana uwezo lakini hawana makaazi.

Kwa hivyo, lengo la serikali ni kuhakikisha kuwapa nyumba za makaazi wale wananchi wote wanaostahiki wa Zanzibar kwa mujibu wa taratibu zinazofaa.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, lakini kuna nyumba ambazo sasa hivi ni mbovu sana.

Kwa mfano, kama nyumba ya Kengeja ilioko katika Jimbo la Mhe. Hija Hassan Hija, ambapo tulipiga kelele sana katika vipindi vya bajeti vilivyopita na nyumba hiyo iliwahi kutengewa shilingi milioni 100 kwa ajili ya kuanza

kufanyiwa ukarabati, lakini bahati mbaya nyumba ile mpaka sasa haijakarabatiwa na muna raia wetu, ambao ni wananchi wetu wa serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar na nyumba ilikuwa imeanza kukatika vipande.

Je, ni lini hasa wizara yake Mhe. Naibu Waziri ataona kwamba nyumba ile kuna haja ya kuikarabati ili tusije tukapata hasara wananchi kuja kupigwa na nyumba wakafa?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli jengo la nyumba za Maendeleo Kengeja liko katika hali ngumu, lakini Wizara yangu kupitia Idara ya Nyumba tumejitahidi, kwa kipindi cha kwanza kutaka kuifanyia matengenezo nyumba hiyo; na katika hatua tuliochukua hapo awali ni kutaka kuliezeka jengo hilo. Lakini baada tu ya kuanza shughuli hizo, kuna raia wasiokuwa waaminifu wamefika kwenye nyumba hiyo na kuziondoa bati ambazo tayari tulikuwa tumeshaziweka.

Kwa hivyo, lengo la serikali ni kuhakikisha nyumba zake zote inazifanyia matengenezo kama nilivyoeleza hapo awali. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi avute subira na tushirikiane katika kulilinda jengo hilo.

Nam. 7

Matengenezo ya Barabara ya Chambani

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ilijenga barabara sita Mkoa wa Kusini Pemba kwa mfumo wa *'labour base.'* Baadhi ya barabara hizo zimejengwa chini ya kiwango, na kwa kuwa barabara ya Chambani imeanza kuchimbuka maeneo kadhaa ikiwa ni mwaka mmoja tu tokea kufunguliwa.

Je, ni lini Wizara yako itazifanyia ukarabati sehemu zilizochimbuka kabla ya kuathirika zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 7 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ilijenga barabara sita katika Mkoa wa Kusini Pemba, zenye jumla ya urefu wa 42.83km kwa kutumia nguvu kazi watu na mitambo yaani (*mixed labour base and equipment).* Barabara hizo zilijengwa kwa kutumia lami baridi na kokoto zenye sifa maalum. Lengo la ujenzi kwa kutumia nguvu kazi watu, zaidi lilikuwa ni kutoa ajira kwa jamii pamoja na kuboresha usafiri kwenye maeneo husika, ili kupita kwa urahisi na wakati wote.

Kwa kuwa teknolojia hii ndio kwanza ilianza nchini kwetu, ni dhahiri kuwa kulikuwa na kasoro zilizofanyika na hivyo baadhi ya sehemu ya barabara hizo, hasa zilizoanza mwanzo kujengwa zilianza kufumka na kusababisha mashimo. Tunaamini changamoto hizo zenye kujitokeza zitawekwa sawa na barabara hizo kubaki nzima na salama.

Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu imekuwa ikitenga fedha kila mwaka wa fedha, kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara, kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo barabara zote zilizojengwa kwa lami, ili kukakikisha kuwa zinaendelea kuwa na hali nzuri na zinapitika kwa urahisi wakati wote.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, wizara yangu itahakikisha kuwa sehemu zote zilizochimbuka kwenye barabara hizo zitafanyiwa matengenezo stahiki ili kuondosha usumbufu kwa wananchi watumiao barabara hizo.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru na namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa kukiri kwamba barabara hizi zinakuwa na kasoro mbali mbali. Kwa kuwa miongoni mwa kasoro zilizojitokeza katika barabara hizi ikiwemo ya Chambani, ni wembamba na ufinyu kiasi ambacho haina uwezo wa kupishana gari mbili kwa pamoja. Na kwa kuwa sehemu zote zenye misingi zilizomalizia barabara hizi, zimekuwa zikichimbika siku hadi siku.

a) Je, Mhe. Naibu Waziri ni lini barabara hizi zitafanyiwa utanuzi ili ziweze kupishana angalau gari mbili kwa wakati mmoja.

b) Kwa kuwa wananchi wengi walikatiwa miti yao ikiwemo ile ya matunda pamoja na mikarafuu, lakini hadi leo hii hawajalipwa fidia zitokanazo na matengenezo ya barabara ile. Mhe. Naibu Waziri ni lini, kwa uhakika wa utekelezaji, wananchi hawa wanyonge watalipwa fidia ya miti yao iliyokatwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, swali la msingi lilikuwa linaulizia namna ya athari zilizojitokeza katika barabara na nini mipango ya serikali katika kukarabati barabara hizo.

Katika majibu yetu tumeeleza kwamba barabara hizo katika bajeti ya mwaka huu, tutaendelea na utaratibu wa kuzifanyia ukarabati. Sasa swali la nyongeza Mhe. Mwakilishi anaulizia kuwa ni lini serikali tutatanua barabara hiyo. Mimi namuomba Mhe. Mwakilishi akumbuke mazingira halisi ya barabara zenyewe zilivyo, mradi wenyewe ulivyo na hiki ambacho anakiomba hivi sasa.

Tunapozungumzia suala la barabara zile tuzitanuwe. Wewe mwenyewe ni shahidi, umesema sasa hivi hapa kwamba kuna watu hawajalipwa fidia na njia zenyewe unaziona. Unaposema njia zile uzitanuwe maana yake unaongeza tatizo jengine sasa la fidia na huo itabidi utengeneze mradi mpya.

Njia zile ni kweli nyembamba, lakini tunaamini kwa matumizi yaliyokusudiwa au yaliyolengwa njia zile zinakidhi na sitegemei kwamba barabara hizo magari mawili yashindwe kupishana. Kwa sababu barabara zote zimejengwa zinazidi mita 3.5 upana wake, kwa kuamini kwamba vipimo hivyo vinakidhi gari mbili kuweza kupishana. Lakini tuwaahidi lini barabara zile tutazitanua hatuwezi kuahidi, kwa sababu huo ni mradi mpya.

Swali la pili anauliza ni lini serikali italipa fidia kuhusiana na miti. Maelekezo ya serikali yako wazi kwamba kila barabara ambayo tutakuwa tunajenga, kipaumbele chetu kulipa fidia itakuwa ni nyumba, miti itaendelea kusubiri na tutahakikisha kama kuna deni basi wananchi wetu tutawalipa, tunaweza kuchelewa lakini deni ni lazima tulilipe.

Tulifanya hivyo kwa barabara za Unguja, tulifanya hivyo kwa barabara za Pemba. Tutafanya hivyo kwa barabara za Unguja na tutafanya hivyo kwa barabara za Pemba.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, mbali na barabara ya Chambani ambayo ilijengwa kwa *labour base*, lakini kuna barabara ya Mtambile Kengeja ambayo ilijengwa kwa njia hiyo hiyo, lakini barabara hiyo ni mbovu na haifai.

a) Je, ni lini serikali itazifanyia ukarabati pia barabara hiyo?

b) Barabara ya Kinazini - Biziredi - Kariakoo hivi karibuni iliharibika kwa mvua kubwa iliyonyesha. Je, wizara ina mpango gani kuifanyia ukarabati barabara hiyo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri majibu, japokuwa barabara zilizozungumzwa za Pemba, wewe umeongeza na za kwa Biziredi. Kwa hivyo Mhe. Naibu Waziri akiweza atajibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, barabara hizi tunazozizungumza tumejenga kwa mfumo wa *labour base* kwa maana kwamba sehemu kubwa ya matayarisho ya barabara hizi ilikuwa ikitumika mikono na nguvu kazi za watu, mashine matumizi yake yalikuwa madogo. Ni kweli kwamba barabara ya Mtambile Kengeja ndio barabara ya kwanza kujengwa katika mfumo huu na ndio barabara ambayo imeonesha athari nyingi.

Mhe. Naibu Spika, kwa barabara ya Mtambile kuna sehemu ya Mjimbini pale mbele baada ya uwanja wa mpira, kuna barabara baadhi ya sehemu imetoka na imeathirika vibaya. Lakini pia barabara ya Mizingani - Wambaa kuna sehemu tatu zimeathirika sana, Ziwadini *base* imetoka nje lami imeondoka, eneo la Tumbi barabara imeharibika,

lakini pia tumegundua kwamba *base* ilikuwa dhaifu, *canvas* ya mwisho maji yanapita juu ya barabara, kwa hivyo yamekokoa zile *shoulder* za barabara zimeathirika.

Kwa hivyo, malengo yetu ni kuwa mwaka huu wa bajeti tutaendelea na utaratibu wa kufanya matengenezo kwa barabara hizo sita za Pemba, barabara nyengine zote za Unguja na Pemba nazo pia zitafanyiwa ukarabati hatua baada ya hatua. Kama tunavyotambua kwamba mfuko wa barabara umeingia mkataba na idara yetu ya *UUB* kwa mfumo wa *PA*. Madhumuni makubwa ni kuona kwamba kunafanywa ukarabati kila sehemu ambazo zimeathirika. Kwa kipindi hiki tulishindwa kufanya ukarabati kwa sababu ya mvua, tukiamini kwamba tunaweza tukakarabati asubuhi jioni mvua ikaathiri tena. Kwa hivyo, tunapisha mvua zipite tutafanya ukarabati maeneo yote ya mjini, yakiwemo maeneo ya Rahaleo, Kwa Biziredi na maeneo yote ya Unguja pamoja na Pemba.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii, naomba pia nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana yenye ufafanuzi mzuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi nina swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Kwanza huu mfumo wa *labour base* ni mzuri sana. Lakini ningeomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, anahakikisha vipi kuwabana wakandarasi ili watumie mfumo wa *labour base* ilioko hapa hapa Zanzibar na sio ya kutoka nje ya Zanzibar. Kwa sababu mara nyingi hawa wakandarasi wakija, huwa wanakuja na timu zao au kambi zao, wanapiga kambi kwa kule Pemba na kwa hapa Unguja pia.

Kwa hivyo, wizara yake inahakikisha vipi kuchukua *labour base* ambayo iko Zanzibar, kwa sababu tuna vijana wetu wengi ambao wako majimboni, wako kwenye maskani wanakaa. Vijana wa Chumbuni, Kiembesamaki, Watumbatu, Kiwani na kadhalika. Sasa vipi wizara yake wakati inampa mkataba yule mkandarasi itahakikisha kwamba *labour base* ile itoke hapa, ili hawa vijana wetu waweze kufaidika na ile *casual labour*. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, wanapotoa mikataba Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano, katika ile mikataba sheria zao wakati kuna pesa za kutoka nje na pesa za serikali au Mfuko Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Vipi wanaweza kuhakikisha kwamba yule mkandarasi anabanwa zaidi kuipendelea Zanzibar kuliko upendeleo wa yule mkandarasi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, swali la kwanza alikuwa anazungumzia suala la *labour base.* Naomba tu nichukue nafasi hii kumfahamisha vizuri, swahiba yangu na kaka yangu Mhe. Mahmoud Thabit Kombo nini maana ya *labour base*.

Barabara hizi ambazo tulikuwa tunazungumza kuwa zimetengenezwa kwa mfumo wa *labour base*, ni barabara ambazo tukipata ufadhili wa Norway. Fedha ambazo zilitumika kujenga barabara hizi za kilomita 48, zilikuwa ni karibu dola milioni 11.4 na Serikali ya Mapinduzi tukalazimika kuchangia dola milioni moja. Kwa hivyo, mradi huu utauona ni mradi rahisi kigharama katika utekelezaji wake, lakini barabara hizi zilizojengwa ni barabara za ndani, ni barabara ambazo hazihitaji mzigo mkubwa matumizi yake.

Labour base maana yake ni kwamba teknolojia iliyotumika sehemu ilikuwa inahusisha wananchi kwa kutumia mikono kulikoni vifaa. Kwa hivyo, barabara hizi nyengine wanalazimika kutafuta ma-*contractor* wengine wa kutumia vifaa zaidi kutokana na mahitaji ya barabara zenyewe. Kwa sababu barabara nyengine tunajenga zenye upana zaidi wa mita 5 mpaka mita 6 kwa ajili ya kutumika kubeba mzigo wa tani 10 mpaka tani 15, na mpaka tani 20, barabara hizi tunazozizungumza hakuna ambayo ina uwezo wa kubeba zaidi ya tani 5 kwenda juu.

Kwa hivyo, *labour base* inayotumika inahitaji maeneo maalum, kwa maana kwamba yale matumizi ya barabara husika. Ingekuwa kama tuna uwezo wa kuwaajiri hao watu kuweza kujenga mabarabara makubwa, ingekuwa ni vizuri kwa sababu gharama zingepungua, lakini umadhubuti wenyewe na uwezo wa barabara bila shaka utakuwa mdogo ukilinganisha na barabara ambazo zitajengwa kwa kusimamia vifaa vya kisasa na vya kimitambo.

Suala la pili ni kwamba wakandarasi wanatakiwa kuwekeza Zanzibar. Huu ni utaratibu uko wazi kabisa kwamba kama mnaingia mkataba wa kufanya kazi basi muhakikishe kuwa mkataba ule una maslahi makubwa na mazuri zaidi kwa wananchi wa Zanzibar na serikali yake. Hatutoingia mkataba ambao tutakuwa na uhakika kwamba

mkataba huu utakuwa una-*favour* upande wa pili, kwa maana kwamba mkandarasi atanufaika zaidi kulikoni wananchi ambao wanahitaji ile huduma ambayo serikali itakuwa imeingia mkataba.

Kwa hivyo, tutaendela tu kusisitiza kwamba mikataba hiyo itakayoingiwa na serikali itakuwa na msingi huo, kuona kwamba serikali na wananchi wake ndio wanaonufaika zaidi na mkataba kulikoni yule mkandarasi au mtu mwengine ambaye amepaswa kuingia katika mkataba kwa ajili ya kutoa huduma au kutoa ufundi maalum au mahitaji yanayohitajika.

Mhe. Waziri wa Muindombinu na Mawasiliano: Nashukuru Mhe. Naibu Spika. Kwanza namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake. Isipokuwa mimi ninataka kuongezea tu hii sehemu ya pili ya jibu.

Kwa kuwa mikataba ya nje inayowahusu makandarasi ina sehemu mbili; wizara imechukua jukumu la ziada la kuona kwamba mkandarasi anabanwa zaidi kuipendelea Zanzibar kwa kuongezea nguvu ya yule mshauri mwelekezi au *Consulted;* pamoja na kwamba mkataba unakuwa na *consultant* lakini Wizara kupitia Idara ya *UUB* inatoa mtaalam kwa kila mradi anakuwa ni *site engineer,* kwa hivyo yeye anaisaidia Wizara moja kwa moja kupitia *consultant* ili kuona kwamba shughuli za *consultant* zinakwenda salama ahsante sana.

Nam. 81

Fidia kwa Watuhumiwa Wanaokosa Hatia Mahakamani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Kwa kuwa haki inayocheleweshwa ni sawa na haki inayonyimwa. Na kwa kuwa kumekuwa na mtindo wa Mahkama zetu kucheleweshe kesi kupata maamuzi.

(a) Je, ni kwa nini kesi hizi zinachelewa kupata maamuzi.

(b) Je, Serikali itakubaliana na mimi kuwa watuhumiwa wanaocheleweshewa hukumu wanapoonekana hawana hatia walipwe fidia kwa siku zote walizokuwa mahabusu.

Mhe. Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Kny: Waziri wa Katiba na Sheria) – Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 81 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba haki inayocheleweshwa ni sawa na haki inayonyimwa, lakini sio nia ya Mahkama zetu kucheleweshe kesi kupata maamuzi, kwani Mahkama katika shughuli zake za utoaji wa haki kunahitaji msaada wa taasisi mbali mbali katika kufanikisha kazi yake hiyo.

Kuna sababu nyingi za kucheleweshe kwa kesi kupata maamuzi kama vile kutokamilika kwa upelelezi ambao unafanywa na Jeshi la Polisi, Jamii kutofika Mahkamani kutoa ushahidi, utoro wa washtakiwa, miundo isiyokidhi shughuli za Mahkama, dharura mbali mbali za Mahakimu, Waendesha Mashtaka, Wataalamu mbali mbali na uchache wa fedha za kuwalipa Mashahidi.

(b) Bado Serikali haijaweka utaratibu wa Kisheria ili kuwalipa fidia wale Watuhumiwa ambao walikuwa Mahabusu na wale waliokuwa nje wakati kesi zao zinaendelea ambao walicheleweshwa kutolewa hukumu kesi zao na kuonekana hawana hatia.

Mhe. Spika, naomba ieleweke zaidi tu utaratibu huu ndivyo ulivyo karibu ulimwengu mzima, lakini kinachofanywa ili kuwaondolea shida watuhumiwa hao ni kuharakisha kesi zao.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Ni sababu gani za msingi zinazotayarisha kesi mfano ya mauaji mtu akae miaka mitatu bila ya kuhukumiwa wakati eneo la mazingira yapo, vyombo vya uchunguzi vipo, na Mahakama ipo, hilo moja.

La pili, uzoefu unaonesha kesi zinazofunguliwa na wakubwa hasa za madai zinakwenda haraka Mahakamani, sababu gani za msingi zilizopelekea kesi za ardhi kukaa miaka sita Mahakamani.

Mhe. Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Kny: Waziri wa Katiba na Sheria): Kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya swali la msingi kwamba ucheleweshaji wa kesi una sababu nyingi, haiwezekani katika utaratibu wa nchi unaofuata Sheria na Utawala bora kwamba; kwa sababu mtu tu kwa kuwa amehukumiwa mauaji basi siku ya pili na yeye anyongwe, ni lazima utaratibu wa kisheria wa Mahakama ufuatwe; vielelezo vipatikane, mashahidi wapatikane, ili kuhakikisha kwamba kesi imekwenda vizuri na kila mtu mwenye haki yake anaipata.

Kwa hiyo sio nia ya Mahakama kucheleweshe kesi, lakini utaratibu mzima wa kuhitaji ushahidi na vielelezo vyengine ambavyo vinawezesha hukumu itolewe kwa njia ya haki. Kwa hivyo hayo ndiyo mazingira ambayo yanatokea, wakati wowote ambapo ushahidi ukipatikana basi Mahakama inatoa hukumu ya kesi hizo bila ya kucheleweshe.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Waziri zipo haki za watuhumiwa au kwa mahabusu wanaokuweko ndani wanahitaji wazipate, haki hizo ikiwa ni mwanamke au mwanamme, Je. Mhe. Waziri iwapo kuwa watuhumiwa wale hawakubainika na kosa na haki zile za ndani ambazo wanatakiwa wazifanye hawakuzifanya Je, Serikali ina mpango wa kuwalipia fidia?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Kny: Waziri wa Katiba na Sheria): Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna haki ambazo mwananchi aliyeko ndani ya Mahabusu angepaswa kuzipata kesi mbali mbali, lakini kwa kuweko kwake Mahabusu haki hizo hazipati na ndio maana ya kuweko kwake Mahabusu, kwa hivyo Serikali kwa hivi sasa haifikirii utaratibu ambao utawezesha kuwalipa fidia wale watu waliokuwepo mahabusu tu, kwa sababu walikosa burudani hii au ile, hayo ni mambo ya kawaida; la msingi watu wetu wahakikishe kwamba wajitahidi kadiri iwezekanavyo katika maisha yao waepuke utaratibu ambao wataingia mahabusu na maeneo mengine ambayo watakosa kupata burudani na haki nyengine za kijamii ambazo wanapaswa wazipate.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika majibu yake amesema kwamba taasisi zinazofanya kazi na Mahakama ndizo ambazo zinapelekea ucheleweshaji wa kesi, swali ni Mahakama inachukua hatua gani kuona kwamba Taasisi ambazo inafanya kazi, nazo zinatoa ushirikiano wa haraka ili kuona kwamba kuna urahisi wa kusikilizwa hizi kesi, kwa sababu kucheleweshwa kwa kusikilizwa hizi kesi kunasababisha uzoroteshaji wa baadhi za taasisi za Serikali kama Chuo cha Mafunzo kwa kuwahudumia hawa mahabusu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Kny: Waziri wa Katiba na Sheria): Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mahakama mara nyingi imekuwa ikifanya vikao mbali mbali na wadau wa kesi katika nchi yetu ili kuendelea kuelimisha umuhimu wa kufanya kazi zao vizuri ili kuharakisha kesi zao, kwa hivyo kazi hiyo Idara ya Mahakama imekuwa ikifanya mara nyingi na tutaendelea kuifanya Idara kuona kwamba suala hili linaendelea, lakini zaidi na wananchi nao wanatakiwa kuja kutoa ushahidi Mahakamani nao ni muhimu wahakikishe kwamba wanapopata wito wa Mahakama wafanye hivyo, kwa sababu kutokuja kwao kunasababisha kesi ziendelee kuzorota na hivyo watu wengine wacheleweshwe kupata haki zao.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujamuita Mhe. Waziri naomba niwatambulishe tumepata ugeni, ugeni huu mwenyewe ni Mhe. Hassan Hamad Omar Mwakilishi wa Jimbo la Kojani kaleta timu yake ya

Shaba Sports Club; ambayo imepanda daraja na safari hii itacheza ligi daraja la kwanza, ina jumla ya wachezaji 26 wakiongozwa na Ndugu Juma Ali Shaame kiongozi Mkuu asimame (*Makofi*)

Baadae kuna ndugu Hassan Makame Mkuu msaidizi wa msafara asimame na yeye. Baadae kuna ndugu Masoud Shaame mjumbe wa kamati tendaji ya timu, kuna ndugu Shaame Hamad; Kocha wa timu, kuna ndugu Bakari Suleiman Zambiya; yeye nahodha wa timu, kuna Ndugu Juma Shaaban Msaidizi nahoza wa timu (*Makofi*).

Kwa hivyo naomba na wale wachezaji wote wasimame. Ahsante kaeni kwa niaba ya Baraza tunakushukuruni sana na tunawaambia karibuni na tunawapongeza.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwenda kunywa chai waende watu kwa utaratibu, tunatoka Baraza zima kwenda kunywa chai, tunabaki mimi na Waziri si jambo zuri. Kwa hivyo mmoja anakwenda akirudi aende mwenziwe, akitoka mmoja akirudi aende mwenziwe, huo ndio utaratibu.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kwa mwaka wa Fedha 2014/15 Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu, likae kama Kamati kwa madhumuni ya kupokea, kujadili, kuzingatia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Kazi za Maendeleo ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma kwa kutujaalia uzima na afya njema na kuweza kutukutanisha katika kikao hiki muhimu cha bajeti kwa faida ya nchi yetu na wananchi wote kwa ujumla. Nchi yetu imeendelea kuwa yenye amani, utulivu na usalama ikizingatia misingi ya Utawala Bora, Demokrasia na Haki za Binadamu. Namuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie neema hii iliyostawi iliyotokana na Mapinduzi Matukufu ya Januari 1964. Tunamuomba Mola Karimu atuzidishie upendo, umoja na mshikamano katika nchi yetu na atujaalie kuyaenzi Mapinduzi ya Januari 1964 milele kwa faida yetu sote na kwa vizazi vyetu vijavyo.

Mhe. Naibu Spika**,** tarehe 12 Januari, 2014, nchi yetu iliadhimisha kutimia miaka 50 (Nusu Karne) tokea kuasisiwa kwa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964. Hivyo basi, kwa namna ya pekee natoa pongezi za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuadhimisha kwa mafanikio makubwa sherehe hizo adhimu ambazo kauli mbiu yake ni *"Tudumishe Amani, Umoja na Maendeleo ambayo ni Matunda ya Mapinduzi Yetu - Mapinduzi Daima".*

Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine tena naomba niungane na Watanzania wenzangu wote kuwapongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa Maadhimisho ya Miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Sherehe za kutimiza miaka 50 ya Muungano ziliadhimishwa kwa kauli mbiu **"***Utanzania Wetu ni Muungano Wetu, Tuulinde, Tuuimarishe na Kuudumisha"*. Namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekima na awape umri mrefu na afya njema ili waweze kuendelea kuiongoza vyema nchi yetu na kuzidi kuijengea taswira nzuri Kitaifa na Kimataifa. Nawapongeza Watanzania wote kwa kutimiza miaka 50 ya Muungano wetu tukiwa katika hali ya amani, upendo na utulivu. Mungu ibariki Zanzibar, Mungu ibariki Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza hili Tukufu kwa uongozi wenu mahiri. Naomba pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Hamza Hassan Juma; Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura. Vile vile, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Hesabu za Serikali *PAC* inayoongozwa na Mheshimiwa Omar Ali Shehe; Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake. Namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekima na busara katika kazi zao za kusimamia Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kutupatia miongozo na ushauri ambayo

inatusaidia sana katika utekelezaji wa majukumu na malengo yetu. Naomba pia kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa mashirikiano yao makubwa wanayoendelea kuipatia Ofisi yetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nihitimishe sura hii ya Utangulizi kwa kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Mahmoud Thabit Kombo kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Kiembesamaki kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM). Ushindi huo mkubwa unadhihirisha imani kubwa waliyonayo wananchi wa Kiembesamaki kwake na Chama Cha Mapinduzi kwa ujumla, sambamba na kuonesha matumaini waliyonayo wananchi wa Jimbo hilo katika kuwaletea maendeleo.

MUUNDO NA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Naibu Spika, katika mwezi wa Agosti, 2013, muundo wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ulibadilika ambapo Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho na Idara Maalum za SMZ ziliondolewa na kuhamishiwa katika Ofisi mpya inayoitwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Aidha, katika mabadiliko hayo Idara ya Utawala Bora, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Tume ya Mipango pamoja na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali zilihamishiwa katika Ofisi hii.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na muundo huo mpya, majukumu ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi yanatekelezwa na Idara pamoja na Taasisi zifuatazo:-

i. Ofisi ya Faragha;
ii. Ofisi ya Baraza la Mapinduzi;
iii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
iv. Idara ya Mawasiliano – Ikulu;
v. Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
vi. Ofisi ya Usalama wa Serikali (GSO);
vii. Idara ya Utawala Bora;
viii. Ofisi ya Ofisa Mdhamini – Pemba;
ix. Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje;
x. Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi;
xi. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;
xii. Tume ya Mipango;
xiii. Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

SHABAHA YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Naibu Spika**,** Shabaha kuu ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni:-

i. Kuimarika kwa huduma bora kwa wananchi;
ii. Kuwa na mipango endelevu ya maendeleo inayolenga kukuza uchumi na kupunguza umasikini (kuimarika kwa maendeleo ya Zanzibar);
iii. Kuimarika kwa Utawala Bora na Haki za Binadamu;
iv. Kujenga jamii inayopinga na kukataa vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi;
v. Kuimarika kwa uhusiano wa Kikanda na Kimataifa wenye tija kwa Zanzibar;
vi. Kuongeza mchango wa Wazanzibari wanaoishi nchi za nje (*Diaspora*) katika shughuli za kimaendeleo na kijamii – Zanzibar.

MWELEKEO WA BAJETI YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeandaa bajeti yake kwa mujibu wa miongozo ya Serikali ikiwa ni pamoja na kutayarisha maelezo ya bajeti inayotumia mfumo wa *"Line Item Budget"* unaoenda sambamba na mfumo wa*"Program Based Budget".* Katika kutekeleza bajeti hii, jumla ya Programu Kuu 17 zimeandaliwa pamoja na Programu Ndogo 8 ambazo zitakuwa chini ya Programu Kuu.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, mwelekeo wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni kutekeleza mambo makuu yafuatayo:-

i. Kuimarisha huduma za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
ii. Kuandaa vikao vya Kamati ya Makatibu Wakuu, Baraza la Mapinduzi na mikutano ya tathmini ya mipango ya utekelezaji kazi kwa kila robo mwaka kwa Wizara na Ofisi za SMZ;
iii. Kufanya ukaguzi wa hesabu za Serikali kwa kuzingatia thamani halisi (*Value for Money*);
iv. Kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi;
v. Kuanzisha Ofisi ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Pemba;
vi. Kukamilisha Sera ya Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje (*Diaspora*);
vii. Kuanzisha Sera, Sheria na Miongozo ya ushirikiano wa Sekta binafsi na Umma (PPP);
viii. Kuandaa Sera ya Maendeleo ya Rasilimali Watu ya Zanzibar;
ix. Kuandaa Kanuni zitakazosaidia utekelezaji mzuri wa Sheria ya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi;
x. Kufanya utafiti juu ya masuala ya Majukumu ya Kijamii (*Corporate Social Responsibility*);
xi. Kufanya utafiti juu ya Mchango wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje (*Diaspora*) katika Maendeleo ya kiuchumi na kijamii Zanzibar;
xii. Kufanya Utafiti wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar;
xiii. Kufanya Utafiti wa Kipato na Matumizi ya Kaya;
xiv. Kuandaa Mpango Mkakati wa Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi pamoja na kuandaa mpango kazi wa mwaka;
xv. Kuandaa miongozo ya kufanya tafiti mbalimbali.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI YAOFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014 NA MALENGO YALIYOPANGWA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2013/2014umezingatia mambo yafuatayo:-

i. Dira ya Zanzibar (*VISION 2020*);
ii. Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar *(MKUZA II);*
iii. Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (2011 – 2017);
iv. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2010-2015;
v. Ushauri wa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakati wa kujadili hotuba ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2013/2014;
vi. Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, na Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia Hesabu za Serikali *(PAC).*

OFISI YA FARAGHA

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Faragha imeendelea kuratibu shughuli za huduma za Ikulu.Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Faragha ilitengewa jumla ya TZS 2,197.2milioni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi 2014, Ofisi ya Faragha imeingiziwa TZS.1, 589 sawa na asilimia 72.3 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Naibu Spika, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein alifanya ziara mbili za kikazi nje ya nchi. Ziara hizo ni ya Uholanzi iliyofanyika mwezi Agosti, 2013 na ziara ya India iliyofanyika mwezi Februari, 2014. Katika ziara iliyofanyika mwezi Agosti, 2013 nchini Uholanzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein alikutana na kufanya mazungumzo na Mfalme wa Uholanzi Mhe. Willem Alexander, Waziri Mkuu wa Uholanzi Mhe. Mark Rutte pamoja na Waziri wa Biashara za Nje na Uhusiano wa Kimataifa Mhe. Lilianne Ploumen. Mazungumzo na Viongozi hao yalihusu kuimarisha uhusiano baina ya nchi zetu pamoja na kuendeleza mashirikiano katika sekta ya Afya, Kilimo na Nishati. Aidha, pamoja na mambo mengine masuala yanayohusu kuiendeleza sekta ya Mafuta na Gesi, mazingira, kuhamasisha uwekezaji na kuimarisha utalii yalizingatiwa.

Mhe. Naibu Spika, katika ziara ya Uholanzi Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na ujumbe wake walipata fursa ya kuitembelea Kampuni ya Shell ambapo Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban na Mwakilishi wa Kampuni ya Shell Bwana Axel Knospe walisaini Waraka wa Makubaliano (MoU) ambao utawezesha kuanza mashirikiano ya kufanya utafiti wa kuwepo kwa mafuta na gesi hapa nchini. Aidha, Kampuni ya Shell iliahidi kushirikiana na Zanzibar katika kuendeleza Utalii kwa wote, na kuwajengea uwezo vijana katika stadi za maisha na ujasiriamali.

Mhe. Naibu Spika**,** ziara ya nchini Uholanzi ilimpa fursa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kukutana na Viongozi wa Kampuni mbalimbali zinazohusika na huduma za afya, na alichukua jukumu mwenyewe la kuwaelezea kwa kina juu ya maendeleo ya sekta ya Afya Zanzibar ikiwemo mipango ya kuanzisha Skuli ya Sayansi ya Afya na Tiba katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA).

Miongoni mwa Kampuni alizokutana nazo ni "*Tax Force Health Care", "African Medical and Research Foundation" (AMREF)* na *"Medical Export Group".* Kufuatia ziara hiyo, ujumbe wa aina yake wa kwanza wa Wawekezaji na Wafanyabiashara 50 kutoka Uholanzi ukiongozwa na Waziri wa Biashara za Nje na Uhusiano wa Kimataifa, Mhe. Lilianne Ploumen ulitembelea Zanzibar tarehe 20 Februari, 2014 kwa madhumuni ya kuimarisha uwekezaji na biashara.

Mhe. Naibu Spika, mnamo mwezi wa Februari, 2014, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein alifanya ziara ya kiserikali nchini India na kukutana na mwenyeji wake, Makamu wa Rais wa India, Mhe. Mohammad Hamid Ansari. Katika mazungumzo yao, Viongozi hao waligusia haja ya kuimarisha uhusiano wa kisiasa na kidiplomasia kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na India pamoja na kukuza ushirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya India.

India imekubali kushirikiana na Zanzibar katika upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika Mji wa Zanzibar. Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ametumia fursa hiyo vile vile kuwaalika Wafanyabiashara na Wawekezaji wa India kuja kuwekeza Zanzibar. Aidha, India iliihakikishia Zanzibar kuwepo kwa fursa za kibiashara ikiwa ni pamoja na soko la kutosha kwa bidhaa zake.

Mhe. Naibu Spika, katika hatua nyengine ya ziara hiyo, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alifanya mazungumzo na Waziri wa Afya na Familia wa India, Mhe. Ghulam Nabi Azad. Katika mazungumzo hayo, pande hizo mbili zilikubaliana kushirikiana katika sekta ya Afya kupitia nyanja ya Afya ya Mama na Mtoto. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetiliana saini Waraka wa Makubaliano na Hospitali ya *Manipal* (Bangalore) wa kuimarisha ushirikiano na kupendekeza kujenga Hospitali ya kisasa hapa Zanzibar kwa ajili ya wananchi na watalii.

Maeneo mengine ambayo Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein na ujumbe wake waliyatembelea ni Chuo cha Mafunzo ya Amali cha *"Barefoot College",* Jaipur, Chuo cha Utafiti wa Kilimo (IARI), Delhi, Umoja wa Wasafirishaji wa Dawa na Kiwanda cha kutengenezea dawa (NATCO), Hyderabad. Kadhalika, walitembelea Kiwanda cha usindikaji wa viungo cha Everest na Kiwanda cha Matrekta cha Mahindra & Mahindra Mumbai. Wakati ujumbe huo ukiwa Mumbai ulifanya mkutano na Kampuni za Kitalii na kuzitaka kuleta Watalii Zanzibar. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein alipata fursa ya kuweka shada la maua katika kaburi la Baba wa Taifa la India, Mhe. Mahatma Gandhi na aliyekuwa Waziri Mkuu wa India Marehemu Indira Gandhi.

Mhe. Naibu Spika, kufuatia ziara hiyo ya India na mwaliko wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tayari ujumbe wa Kampuni ya *Mahindra & Mahindra Limited* kutoka India umeshakuja Zanzibar na kukutana na watendaji wa Wizara ya Kilimo na Maliasili na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kufunga Mkataba wa Maelewano utakaorahisisha utaratibu wa kuipatia Zanzibar zana za kilimo. Aidha, ujumbe kutoka Chuo cha Mafunzo ya Amali cha *"Barefoot"*umeshawasili kuangalia eneo litakalojengwa Chuo cha Amali cha Wanawake huko Kibokwa, Mkoa wa Kaskazini Unguja, kitakachotengeneza bidhaa zinazotumia nishati ya jua.

Mhe. Naibu Spika, katika kuimarisha uhusiano baina ya Zanzibar na nchi marafiki, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein alikutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Marekani

Mhe. Barack Obama tarehe 1 Julai, 2013 na Waziri Mkuu wa Finland Mhe. Jyrki Katainen tarehe 30 Januari, 2014; ambapo waligusia zaidi ushirikiano katika nyanja ya uchumi, ustawi wa jamii na siasa.

Watu wengine mashuhuri waliokutana na Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein ilikuwa siku ya tarehe 11 Januari, 2014 ni pamoja na Rais wa Commoro Mhe. Dkt Ikililou Dhoinine, Waziri wa Serikali za Mitaa wa China Mheshimiwa Jiang Weixin.

Aidha, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alikutana na Waziri wa Uingereza anayeshughulikia Mambo ya Afrika, Mhe. Mark J. M. Simmonds tarehe 13 Julai, 2013 na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Chama cha Kikomonisti cha Jamhuri ya Watu wa China Mhe. Ai Ping tarehe 10 Oktoba, 2013. Vile vile, Mhe. Rais alionana na Rais wa Uganda Mhe. Yoweri Kaguta Museveni aliyehudhuria katika Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 50 kuadhimisha Mapinduzi ya Zanzibar tarehe 12 Januari, 2014.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Faragha ina jukumu la utunzaji na utengenezaji wa majengo ya Ikulu Kuu ya Mnazi Mmoja, Ikulu ndogo ziliopo Kikwajuni, Kibweni, Mkokotoni na Bwefum. Nyengine ni Ikulu ndogo ya Chake Chake, Mkoani, Micheweni, Dar es Salaam na Dodoma. Aidha, nyumba nyengine zinazosimamiwa na Ofisi hii ni Mazizini I na II ziliopo Unguja.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Faragha kwa mwaka wa fedha 2013/2014, imeendelea kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi wake katika ngazi ya Cheti, Stashahada na Shahada ya Uzamili. Wafanyakazi watano wamehitimu masomo yao katika Chuo cha Maendeleo ya Utalii Maruhubi, wanne kati yao wamehitimu masomo ya Stashahada ya Uongozi na Ukarimu wa Utalii na mmoja Stashahada ya Upishi. Kadhalika, mfanyakazi mmoja anaendelea na masomo ya Shahada ya Uzamili katika fani ya Habari nchini China.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Faragha imepanga kutekeleza malengo manne yafuatayo:-

i. Kuimarisha huduma za Ikulu;
ii. Kuimarisha mazingira ya kazi;
iii. Kuendelea na matengenezo ya majengo ya Ikulu Unguja, Pemba, Dodoma na Dar-es-salaam;
iv. Kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi sita katika ngazi ya Stashahada, watatu ngazi ya Cheti na kutoa huduma stahiki kwa wafanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, ili Ofisi ya Faragha iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS. 2,446.8 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi imeendelea kutekeleza kazi zake za kuratibu shughuli za Baraza la Mapinduzi. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi ilitengewa jumla ya TZS. 1,379 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2014, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi iliingiziwa TZS. 909.7 milioni sawa na asilimia 66 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi imeandaa jumla ya vikao 18 vya kawaida vya Baraza la Mapinduzi na vikao 32 vya kawaida vya Kamati ya Makatibu Wakuu ambapo katika vikao hivyo, nyaraka zaidi ya 110 zilijadiliwa zikiwemo Miswaada ya Sheria, Sera, Miongozo na Taarifa mbalimbali. Aidha, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi imeratibu na kusimamia mkutano mmoja wenye vikao 17 vya pamoja kati ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Viongozi na Watendaji wa Wizara mbalimbali za Serikali ili kujadili na kutathmini mipango ya utekelezaji kazi kwa Wizara za SMZ pamoja na shughuli nyengine za Serikali.

Mhe. Naibu Spika, katika kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi imekamilisha matengenezo ya sehemu ya jengo la Jumba la Wananchi Forodhani linalotumiwa na Ofisi hii. Aidha, Ofisi imeendelea na kazi ya utengenezaji wa kumbukumbu pamoja na nyaraka na kuziweka katika mifumo ya Vitabu na kumbukumbu za Elektroniki yaani *"Hard copy and Soft copy"*. Ofisi ya Baraza la Mapinduzi imeendelea

kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi wake katika ngazi na kada mbalimbali ambapo imedhamini mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi wanne katika ngazi ya Shahada ya Kwanza, Shahada ya Pili na Stashahada katika fani za Uhazili, Utawala, Uhusiano wa Kimataifa na Sheria.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi imepanga kutekeleza malengo manne ya kazi kama yafuatayo:-

i. Kutayarisha na kusimamia Vikao vya Baraza la Mapinduzi na Kamati ya Makatibu Wakuu;
ii. Kuandaa na kusimamia Mikutano ya kutathmini mipango ya utekelezaji kazi kwa kila robo mwaka kwa Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
iii. Kuimarisha mazingira ya kazi na kuwaongezea ujuzi wafanyakazi;
iv. Kuendelea na kazi ya uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka mbalimbali za Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, ili Ofisi ya Baraza la Mapinduzi iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS. 1,458.2 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeendelea na jukumu lake la kuratibu na kusimamia uandaaji wa Sera, Sheria na Mipango ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ilitengewa jumla ya TZS. 522.4 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida na TZS 750 milioni kwa ajili ya matumizi ya miradi miwili ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi mwaka huu, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeingiziwa jumla ya TZS. 262.9 milioni sawa na asilimia 50.3 ya makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida na TZS 450 milioni sawa na asilimia 60 ya makadirio ya matumizi ya kazi za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imekamilisha mapitio ya Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wa mwaka 2014/2015 – 2016/2017. Aidha, Ripoti za robo tatu kwa mwaka 2013/2014 pamoja na taarifa jumuishi ya mwaka 2012/2013 za utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zimetayarishwa na kuwasilishwa kunakohusika.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*) imeandaa vipaumbele vya maeneo ya utafiti kwa ajili ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imechapisha nakala 800 za Kitabu Maalum kinachoitwa "Taarifa ya Miaka 50 ya Maadhimisho ya Sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar". Kitabu hicho chenye sura nane, pamoja na mambo mengine kinaelezea historia fupi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Muundo wake na namna ulivyobadilika katika nyakati tofauti, majukumu na malengo ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, mafanikio, changamoto na matarajio ya baadae. Nakala za vitabu hivyo zimegaiwa kwa wananchi na wadau mbalimbali wakati wa Maonesho ya Maadhimisho ya Sherehe za Kutimia Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Taarifa za kitabu hicho pia zinapatikana kupitia Tovuti (*Website*) ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa anuani ya www.ikuluzanzibar.go.tz.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, wafanyakazi 10 walihudhuria mafunzo mbalimbali ambapo watano kati yao wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi katika ngazi ya Shahada ya Pili, Shahada ya Kwanza na Stashahada katika fani za Sheria, Uchambuzi wa Sera, Maendeleo ya Jamii, Teknohama na Ukatibu Muhtasi. Aidha, wafanyakazi wengine watano wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi katika fani za Uandaaji na Usimamizi wa Bajeti na Usimamizi wa Tovuti (Website). Sambamba na hilo, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeendesha mafunzo ya siku tatu kwa watendaji 23 wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi yaliyolenga kuwajengea uwezo juu ya matumizi ya Kompyuta.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuratibu uandaaji wa Mipango, Sera, Sheria na Tafiti mbalimbali;

ii. Kuanzisha Mfumo Shirikishi wa Ufuatiliaji na Tathmini;
iii. Kuendesha mafunzo mbalimbali kwa watendaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusu usimamizi wa utekelezaji wa malengo ya bajeti na namna ya kuandaa mipango inayozingatia matokeo *(Result-Based Planning);*
iv. Kuimarisha ukusanyaji, uhifadhi, usimamizi na matumizi ya takwimu na taarifa za utekelezaji wa malengo ya bajeti katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
v. Kuimarisha huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA).

Mhe. Naibu Spika, ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS. 428.3 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na TZS 530 milioni kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

IDARA YA MAWASILIANO – IKULU

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mawasiliano Ikulu imeendelea kuimarisha mawasiliano baina ya Ikulu na Umma kwa kutoa elimu na taarifa mbalimbali kwa wananchi kupitia Tovuti, majarida na vyombo vya habari. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Mawasiliano – Ikulu ilitengewa jumla ya TZS. 242.7 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2014, Idara ya Mawasiliano – Ikulu imeingiziwa TZS. 131.7 milioni sawa na asilimia 54.3 ya makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mawasiliano – Ikulu imechapisha nakala 12,000 za matoleo manne ya "Jarida la Ikulu" na kuzisambaza kwa wananchi pamoja na Taasisi mbalimbali za Serikali na Sekta binafsi. Aidha, vipindi 31 vya Televisheni na 13 vya Redio vimerushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC). Vipindi hivyo vinaonesha matokeo mbalimbali ya utekelezaji wa kazi pamoja na ahadi alizozitoa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mawasiliano - Ikulu imeandaa na kurusha hewani makala za filamu *(documentary films)* zenye kuonesha mafanikio yaliyopatikana katika sekta za Utalii na Miundombinu ikiwemo Barabara na Viwanja vya Ndege. Makala hizo pia zimeonesha hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuimarisha zao la karafuu. Aidha, makala 24 za magazeti ziliandikwa na kuchapishwa. Uandaaji wa makala hizo ulikwenda sambamba na shamra shamra za Maadhimisho ya Sherehe za Kutimiza Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Mawasiliano - Ikulu imepanga kutekeleza malengo manne ya kazi yafuatayo:-

i. Kuendeleza taswira nzuri ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuimarisha na kuendeleza mawasiliano na wananchi;
ii. Kuendelea kuimarisha mazingira mazuri ya kazi;
iii. Kuanzisha kitengo maalum cha uwekaji wa kumbukumbu za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
iv. Kuwajengea uwezo wa kiutendaji wafanyakazi wake.

Mhe. Naibu Spika, ili Idara ya Mawasiliano – Ikulu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS. 225.8 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi iliendelea kusimamia Sheria na Kanuni za Utumishi kwa wafanyakazi. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ilitengewa jumla ya TZS. 1,274.6 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2014, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imeingiziwa TZS. 764.7 milioni sawa na asilimia 60 ya makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imehakikisha kuwa wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wamewekwa katika muundo wa utumishi na mishahara yao inalingana na kada

zao.

Aidha, malalamiko ya wafanyakazi wenye uzoefu nayo yameshughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi. Idara ya Uendeshaji na Utumishi imefanya matengenezo makubwa katika jengo la Utawala liliopo mkabala na Ikulu ya Mnazi Mmoja. Jengo hilo la Utawala hivi sasa linatumiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje, Idara ya Utawala Bora na Idara ya Mawasiliano - Ikulu. Matengenezo mengine yamefanyika katika jengo la Utawala Ikulu ambayo yalijumuisha uwekaji wa madirisha ya "*aluminium*", matengenezo ya stoo ya kuwekea majalada na uwekaji wa mbao kwenye ngazi ya jengo hilo.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imechukua hatua za kuhakikisha kuwa Viongozi na Watendaji wanashirikishwa katika maamuzi kwa azma ya kufikia lengo la Utawala Bora.

Katika kufikia hilo, kikao kimoja cha Kamati ya Uongozi na vikao vitano vya Kamati Tendaji vimefanyika. Aidha, vikao tisa vya Bodi ya Zabuni na vikao vinne vya Kamati ya Ukaguzi wa Ndani pia vimefanyika, sambamba na kuandaa mpango wa manunuzi wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti Baraza la Mapinduzi wa mwaka 2013/2014. Vikao hivi vimesaidia sana katika kuimarisha utekelezaji wa Sheria Namba 5 ya mwaka 2005 ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Umma.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imewajengea uwezo wafanyakazi saba katika ngazi ya Shahada ya Uzamili, Shahada ya Kwanza, Stashahada na Cheti. Wafanyakazi wawili wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani za Maendeleo na Ujasiriamali kwa Wanawake na Udereva. Katika hatua ya kuimarisha michezo kazini, Klabu ya Michezo ya Ikulu *(Ikulu Sports Club)* imewezeshwa kushiriki katika mashindano mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuandaa mpango wa matumizi ya Rasilimali Watu *(Norminal Roll);*
ii. Kuongeza ufanisi wa kazi kwa kuimarisha mazingira ya utendaji kazi na maslahi ya wafanyakazi;
iii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya Nchi;
iv. Kuwajengea uelewa wafanyakazi juu ya Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma; na
v. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi kwa kusimamia vikao vya Bodi ya Zabuni na vikao vya Kamati ya Ukaguzi wa Ndani.

Mhe. Naibu Spika, ili Idara ya Uendeshaji na Utumishi iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 1,131.8 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

OFISI YA USALAMA WA SERIKALI *(GSO)*

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Usalama wa Serikali *(GSO)* Zanzibar imeendelea kufanya kazi zake za udhibiti wa shughuli za Usalama wa Serikali na Utumishi wa Umma. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Usalama wa Serikali Zanzibar ilitengewa jumla ya shilingi. 61.6 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2014, Ofisi ya Usalama wa Serikali iliingiziwa shilingi. 25.8 milioni sawa na asilimia 41.9 ya makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Usalama wa Serikali *(GSO)* imepokea jumla ya maombi 932 ya uchunguzi wa

wafanyakazi kutoka Taasisi na Wizara mbali mbali za Serikali. Maombi yote yaliyopokelewa kutoka Wizara, Mamlaka za Serikali, Mashirika na Taasisi nyengine za Umma yamefanyiwa upekuzi *(Security Vetting)* na ushauri unaostahiki umetolewa kwa Wizara na Taasisi husika.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Usalama wa Serikali pia imefanya ukaguzi katika Tume ya Uchaguzi Zanzibar (*ZEC*), Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (*ZAECA*), Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*), Tume ya Kurekebisha Sheria, Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa Mchangamdogo Pemba, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano Zanzibar pamoja na Visima vya maji Bumbwini Kidanzini na Makoba.

Aidha, watumishi wa Serikali wamejengewa uwezo wa kiutendaji kwa kuwapatia mafunzo ya utunzaji na udhibiti wa siri za serikali. Taasisi ambazo watendaji wake walipatiwa mafunzo hayo ni Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Chuo cha Utumishi wa Umma (*IPA*) na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (*ZEC*).

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Usalama wa Serikali imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kufanya upekuzi kwa watumishi 1,907 wanaotarajiwa kuajiriwa na Serikali;
ii. Kuendelea kufanya ukaguzi wa kiusalama katika majengo ya Ofisi za Serikali na Taasisi 12;
iii. Kuongeza uelewa wa watumishi wa umma juu ya umuhimu wa uhifadhi, utunzaji na udhibiti wa nyaraka na kumbukumbu za Serikali; na
iv. Kufuatilia na kufanya tathmini ya maagizo yaliyotolewa wakati wa ukaguzi katika Taasisi husika ili kuona kama kasoro zilizojitokeza zimerekebishwa.

Mhe. Naibu Spika, ili Ofisi ya Usalama wa Serikali iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 47.1 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA UTAWALA BORA

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Utawala Bora imeendelea na jukumu lake la kuratibu na kutathmini utekelezaji wa Misingi ya Utawala Bora Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Utawala Bora ilitengewa jumla ya shilingi 216.5 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2014, Idara imeingiziwa shilingi 143.5 milioni sawa na asilimia 66.3 ya makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Utawala Bora imekamilisha utayarishaji wa Rasimu ya Sheria ya Maadili ya Viongozi ambayo tayari imeshajadiliwa katika Kikao cha Makatibu Wakuu pamoja na Baraza la Mapinduzi. Rasimu hiyo imeshapelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu *(Attorney General Chamber)* kwa ajili ya kutayarishwa Mswaada wa Sheria ambao unatarajiwa kusomwa kwa mara ya kwanza katika Kikao hichi cha Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Utawala Bora imeandaa muongozo wa mafunzo ya Utawala Bora na Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa Taasisi mbali mbali za Serikali na Sekta Binafsi na kutoa mafunzo hayo kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Maofisa Wadhamini, Maofisa Tawala wa Mikoa na Wilaya pamoja na Wawakilishi wa Jumuiya za Kiraia za Kisiwani Pemba. Aidha, vipindi 24 vilivyozungumzia Misingi ya Utawala Bora na Haki za Binaadamu vimerushwa hewani kupitia Redio ya Shirika la Utangazaji la Zanzibar (*ZBC*) na vipindi viwili vimerushwa hewani kupitia Redio za *Chuchu FM, Zenji FM* na *Coconut FM.*

Mhe. Naibu Spika**,** Idara ya Utawala Bora imefanya mikutano mitatu ya mafunzo ya Kikundi Kazi cha Utawala Bora kinachojumuisha Wakurugenzi Mipango, Sera na Utafiti, watendaji wa Asasi za Kiraia na Sekta binafsi. Mafunzo hayo yamelenga namna ya kuandaa viashiria vya utawala bora vya Kitaifa na kuratibu uandaaji wa viashiria vya utawala bora kisekta. Aidha, matayarisho ya utafiti mdogo unaohusu masuala ya utawala bora yamefanyika kwa kuandaa madodoso yatakayotumika katika kukusanyia taarifa za utafiti huo ambao utafanyika katika mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Utawala Bora imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kufanya utafiti mdogo wa Utawala Bora;
ii. Kuendelea kutoa mafunzo juu ya Misingi ya Utawala Bora kwa Viongozi wa Kisiasa, Kiutendaji na wananchi;
iii. Kutayarisha Ripoti ya Mwaka ya Utawala Bora; na
iv. Kutoa Elimu ya Uraia kupitia Redio na Televisheni.

Mhe. Naibu Spika, ili Idara ya Utawala Bora iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya TZS. 227.7 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

OFISI YA OFISA MDHAMINI - PEMBA

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Ofisa Mdhamini Pemba imeendelea kuratibu shughuli za utawala na huduma za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zinazofanyika Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Ofisa Mdhamini Pemba ilitengewa Jumla ya shilingi 645.8 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2014, Ofisi ya Ofisa Mdhamini iliingiziwa shilingi 377.8 milioni sawa na asilimia 58.5 ya makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Ofisa Mdhamini imeratibu ziara za Viongozi Wakuu wa Kitaifa waliotembelea Pemba katika nyakati tofauti. Ziara hizo ni za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais Mstaafu wa Zanzibar wa Awamu ya Sita na Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa ziara za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Ofisi ya Ofisa Mdhamini imeratibu ziara mbali mbali zikiwemo za kutembelea vituo vya karafuu, kukagua ujenzi wa barabara zilizokuwa zikijengwa kupitia Mradi wa Changamoto za Milenia Tanzania *(MCA-T),* kuzungumza na wananchi waliomo katika *"Sober Houses",* ufunguzi wa kituo cha Polisi cha Mchangamdogo, ufunguzi wa Skuli ya Kengeja pamoja na kuzungumza na viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, Ofisi ya Ofisa Mdhamini imeratibu ziara ya ufunguzi wa Skuli ya Sekondari ya wanawake ya Utaani, uzinduzi wa barabara tano zilizojengwa kwa ushirikiano na Shirika la Changamoto la Milenia pamoja na uzinduzi wa mradi wa umeme katika Kijiji cha Ukunjwi.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Ofisa Mdhamini imetoa mafunzo kuhusu athari za uvunjifu wa Haki za Binaadamu kwa Kamati nne za Shehia za Ng'ambwa, Mkoroshoni, Piki, Mzambarauni pamoja

na kurusha hewani vipindi vitatu kuhusu elimu ya uraia kupitia Redio Jamii Micheweni.

Mhe. Naibu Spika, aidha, Ofisi imewapatia mafunzo wafanyakazi wake katika ngazi ya Shahada ya Uzamili, Shahada ya Kwanza na Stashahada katika fani za Manunuzi, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Chakula na Vinywaji na Rasilimali Watu. Mafunzo ya mapambano dhidi ya maambukizi ya *VVU* na UKIMWI kwa wafanyakazi 53 nayo yametolewa.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Ofisa Mdhamini Pemba imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi;
ii. Kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu;
iii. Kuratibu shughuli za ufuatiliaji na tathmini;
iv. Kuratibu utekelezaji wa malengo ya bajeti na namna ya kuandaa mipango inayozingatia matokeo *(Result-Based Planning);*
v. Kuendelea kuratibu mpango wa utoaji wa taaluma ya Utawala Bora na Haki za Binaadamu;
vi. Kuendelea kutoa taaluma kwa Viongozi na wafanyakazi wa Ofisi ya Ofisa Mdhamini juu ya Mapambano dhidi ya UKIMWI na magonjwa yasiyo ya kuambukiza *(Non Communicable Diseases);* na
vii. Kuendelea kutoa mafunzo juu ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa watendaji wa Serikali na wananchi.

Mhe. Naibu Spika, ili Ofisi ya Ofisa Mdhamini Pemba iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 599.9 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA NA URATIBU WA WAZANZIBARI WANAOISHI NCHI ZA NJE

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje (*Diaspora*) imeendelea na utekelezaji wa majukumu ya kuimarisha ushiriki wa Zanzibar katika Mtangamano wa Kikanda na Ushirikiano wa Kimataifa. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje ilitengewa jumla ya shilingi 873 milioni kwa matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi 2014, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje iliingiziwa shilingi 348.8 milioni sawa na asilimia 40 ya makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje imewawezesha wataalamu kushiriki katika vikao vya Mashauriano vya Kikanda vilivyofanyika Dar-es-Salaam. Mashauriano hayo yalihusu ushiriki wa Zanzibar katika mikutano ya majadiliano ya Kikanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) na Jumuiya za Nchi zilizopo katika Ukanda wa Bahari ya Hindi (*IORA*). Aidha, wataalamu wa Zanzibar wameshiriki katika majadiliano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki nchini Burundi na Uganda. Wataalamu wa Zanzibar pia wameshiriki vikao vya Kikanda vya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) nchini Malawi. Kikao cha Baraza la Mawaziri wa Nchi za Jumuiya zilizopo katika Ukanda wa Bahari ya Hindi kilifanyika nchini Australia ambapo pamoja na mambo mengine kilizungumzia kuhusu kukuza ushirikiano wa biashara, uwekezaji, uvuvi na mafunzo kwa nchi wanachama.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya mwaka jana, Zanzibar imeteuliwa kuwa Makao

Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Taratibu zote za kuanzisha Kamisheni hiyo zimekamilika. Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki imetenga jumla ya *US $* 2.009 milioni katika bajeti ya mwaka 2014/2015 kwa ajili ya kuanza kazi Kamisheni hiyo.

Mhe. Naibu Spika, katika kutoa mchango wake SMZ nayo imeshaidhinisha kukabidhiwa Kamisheni hiyo jengo la *EACROTANAL* liliopo mtaa wa Mpirani hapa Mjini Unguja. Aidha, mambo yanayoendelea kupewa umuhimu katika majadiliano ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ni kufanya tathmini ya utekelezaji wa Soko la Pamoja, utekelezaji wa Umoja wa Sarafu na Shirikisho la Kisiasa. Katika Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) Wakuu wa Nchi wamemteua Mheshimiwa Joyce Banda, Rais wa Jamhuri ya Watu wa Malawi kuwa Mwenyekiti wa *SADC* kwa mwaka 2013/2014 na kumteua Ndugu Stergomena Tax kutoka Tanzania kuwa Katibu Mtendaji mpya.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje imeshirikiana na Mashirika ya Kimataifa ya *"Intra Africa Caribean Pacific for Migration Facility" (ACP), "International Organization for Migration" (IOM) na "United Nations High Commission for Refugees" (UNHCR)* katika utayarishaji wa Sera ya Diaspora ya Zanzibar na Sera ya Uhamiaji na Maendeleo kwa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, Sera ya Diaspora Zanzibar imefikia katika hatua kubwa ya maandalizi ambapo kwa sasa Rasimu ya kwanza imekamilika na imewasilishwa kwa Wadau. Sera hii itakuwa imekamilika na kuanza kutumika katika mwaka 2014/2015. Aidha, Tovuti (*Website*) ya Diaspora Zanzibar imekamilika na inapatikana kupitia *www.zanzibardiaspora.go.tz.*

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje imeendelea kuelimisha umma juu ya dhana ya Diaspora kupitia vipindi vya Redio na Televisheni. Naomba kuchukua fursa hii kukipongeza kituo cha utangazaji cha Redio ya *Zenji FM* kwa kuanzisha kipindi maalum cha masaa mawili kila Jumapili kuzungumza na Diaspora wa Kizanzibari na Watanzania wakiwa huko huko nje katika sehemu zao za kazi za kujitafutia maisha.

Mhe. Naibu Spika, aidha, tunaipongeza Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*) kwa kuandaa mazingira mazuri ya Diaspora wa Zanzibar kuleta fedha zao Zanzibar. Pia, kwa jitihada kubwa wanayofanya kuitangaza *PBZ* kwa Diaspora wa Zanzibar waliopo nje ya nchi. Sambamba na hayo, vipeperushi (*brochures*) mbali mbali vinavyohusiana na dhana ya Diaspora na ushirikiano wa Kikanda vimechapishwa na kusambazwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuratibu ushirikiano wa Zanzibar na Jumuiya za Kikanda, Mashirika ya Kimataifa na Nchi nyengine;
ii. Kuwashajihisha Wazanzibari wanaoishi nchi za nje kuekeza na kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya nchi yao; na
iii. Kuimarisha hali za watendaji, mazingira ya kazi na kuwajengea uwezo watendaji wa Idara.

Mhe. Naibu Spika, ili Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 808.2 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (*ZAECA*) imeendelea na kazi ya kuijenga Taasisi na kuanza mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu wa uchumi. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi ilitengewa jumla ya shilingi 810 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida na jumla ya shilingi 480 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2014, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi imeingiziwa shilingi 353.9 milioni sawa na asilimia 43.7 ya makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 229.9 milioni sawa na asilimia 47.9 ya makadirio ya matumizi ya kazi za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (*ZAECA*) imefanya uchunguzi juu ya tuhuma 21 zinazohusiana na makosa ya kutoa na kupokea rushwa, matumizi mabaya ya Ofisi, ulanguzi wa tiketi za kusafiria, ukwepaji wa kodi, kughushi nyaraka na ukiukwaji wa taratibu za manunuzi. Aidha, Mamlaka imeshaanza kuwasilisha majalada ya uchunguzi katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa ajili ya kuendelea na hatua za kimashtaka.

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi imetoa elimu juu ya kupambana na rushwa na uhujumu wa uchumi kwa wananchi wa Shehia za Jambiani Kibigija, Fumba, Kinyasini na Chwaka kwa upande wa Unguja. Taaluma kama hiyo ilitolewa kwa wananchi wa Shehia za Kangagani, Mjini Ole, Kichungwani, Tibirinzi, Msingini na Chachani kwa upande wa Pemba. Aidha, elimu dhidi ya rushwa na uhujumu wa uchumi imetolewa kwa wanafunzi wa Skuli za Ben bella, Lumumba, Mkwajuni, Mwanakwerekwe C, Dunga, Fujoni, Tumekuja na Makunduchi. Kadhalika, elimu hii imetolewa kwa Maofisa Wadhamini, Maofisa Tawala wa Mikoa na Wilaya pamoja na Wawakilishi wa Jumuiya za Kiraia Pemba.

Mhe. Naibu Spika, wafanyakazi 28 wamejengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo ya awali ya uchunguzi kwa lengo la kuimarisha utendaji wao wa kazi. Vilevile, wafanyakazi 10 wamepatiwa mafunzo mafupi juu ya udhibiti wa fedha haramu. Aidha, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi imeshiriki Mkutano Mkuu wa Saba wa Jumuiya ya Nchi Wanachama wa Mamlaka za Kuzuia Rushwa Duniani – *"International Association of Anti-Corruption Authorities" (IAACA)* na Kikao cha Tano cha Nchi Wanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Rushwa –*"United Nations Convention Against Corruption" (UNCAC).* Mikutano yote hiyo ilifanyika nchini Panama katika mwezi wa Novemba mwaka 2013.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kufungua Ofisi ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Pemba;
ii. Kuendelea na uchunguzi wa tuhuma za rushwa na uhujumu wa uchumi;
iii. Kuendelea kukuza uelewa wa wananchi katika masuala ya rushwa na uhujumu wa uchumi kupitia Redio na Televisheni, mikutano ya hadhara, vijarida na vipeperushi;
iv. Kuimarisha mazingira bora ya kazi;
v. Kushiriki katika mikutano mbali mbali ya Kitaifa na Kimataifa; na
vi. Kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo.

Mhe. Naibu Spika, ili Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 815.4 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 621.7 milioni kwa matumizi ya kazi za

maendeleo.

OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeendelea na jukumu lake la ukaguzi wa hesabu za Serikali na Taasisi zake. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar ilitengewa jumla ya shilingi 1,911 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2014, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeingiziwa shilingi 1,549.3 milioni sawa na asilimia 41.1 ya makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2013/2014 imekagua hesabu za Wizara 16, Mashirika ya Umma manane na miradi 12 inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo. Aidha, Ripoti ya Ukaguzi ya Mwaka 2012/2013 imekamilika kwa mujibu wa Katiba. Kwa upande wa ukaguzi wa hesabu za viinua mgongo pamoja na madai ya fidia, jumla ya majalada 1,914 yamepokelewa ambapo majalada 1,025 ya Wastaafu na majalada 19 ya madai ya fidia yamekaguliwa ili yafanyiwe malipo na Wizara ya Fedha. Aidha, majalada 870 ya viinua mgongo yamekaguliwa kwa upande wa malipo yanayofanywa na Mfuko Mkuu wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (*ZSSF*).

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imekamilisha matengenezo makubwa ya jengo la ofisi hiyo liliopo Pemba kwa asilimia 99, matengenezo hayo yanaendana na vigezo vinavyotakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Usalama na Afya Kazini. Ofisi hiyo inatarajiwa kuhamiwa rasmi tarehe 1 Juni, 2014.

Mhe. Naibu Spika, watendaji wanane wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wameshiriki katika mafunzo yanayoendeshwa na Taasisi Kuu za Ukaguzi Duniani zikiwemo *"International Organization of Supreme Audit Institutions"* (*INTOSAI*), *"African Organization of Supreme Audit Institutions" (AFROSAI)* na *"Southern Africa Development Community of Public Accounts Committees"* (*SADCOPAC*). Mafunzo hayo yamelenga kuwajengea uwezo Wakaguzi hususan katika matumizi ya viwango vya Kimataifa vya ukaguzi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, wafanyakazi 10 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi 15 wanaendelea na masomo katika vyuo mbalimbali. Wafanyakazi wengine 25 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ya ukaguzi yakinifu pamoja na tathmini ya kugundua maeneo hatarishi ya ukaguzi (*Risk Based Audit)*. Sambamba na mafunzo hayo, wafanyakazi 30 wamepatiwa mafunzo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo (*Donor Funded Programmes*).

Mhe. Naibu Spika, aidha, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imefanya mapitio na kurekebisha Muongozo Maalum wa Ukaguzi (*Regularity Audit Manual*). Marekebisho yaliyofanyika yamewezesha muongozo huo kwenda, sambamba na mazingira ya sasa na viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeandaa Muundo wa Utumishi (*Scheme of Service*) wa Ofisi hii ili kuimarisha maslahi na majukumu ya Wafanyakazi. Serikali tayari imeshaikubali *"Scheme of Service"* hiyo na hivi sasa inazingatiwa na Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kwa ajili ya utekelezaji. *"Scheme of Service"* hiyo ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatarajiwa kuanza kutumika katika mwaka ujao wa fedha 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

imepanga kutekeleza malengo makuu matano kama inavyooneshwa kwenye kifungu 80.

i. Kuendelea kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba ya ukaguzi wa hesabu za Serikali na Taasisi zake na kutoa taarifa za ukaguzi huo kwa wakati;
ii. Kuendelea kuimarisha uwezo wa wafanyakazi kitaaluma katika fani mbali mbali za ukaguzi kama vile ukaguzi wa kimazingira, ukaguzi wa kompyuta (*Computerized Audit*), uchambuzi wa taarifa za ukaguzi, ukaguzi yakinifu (*Value for Money)* na mafunzo ya muongozo wa ukaguzi (*Regulatory Audit Manual*);
iii. Kuratibu mafunzo ya ukaguzi wa hesabu unaozingatia viwango vilivyowekwa Kimataifa katika ufungaji wa hesabu na uwekaji wa kumbukumbu kwa wadau;
iv. Kutoa mafunzo ya mabadiliko ya bajeti kwa wakaguzi kutoka katika Mfumo wa Vifungu (line item) kwenda katika Mfumo Unaozingati Matokeo (*Programme Based Budget)*; na
v. Kuongeza nguvu katika ukusanyaji wa mapato ili kufikia lengo la kukusanya jumla ya Shilingi 18 milioni katika mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, ili Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 2,023 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

TUME YA MIPANGO

Mhe. Naibu Spika, Tume ya Mipango ndio chombo cha juu cha kutayarisha, kuratibu na kutekeleza mipango ya kiuchumi na kijamii nchini. Kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Mipango Namba 3 ya mwaka 2012, Tume ya Mipango inaongozwa na Mwenyekiti ambae ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Sekretarieti ya Tume inaongozwa na Katibu Mtendaji na inaundwa na Idara tatu ambazo ni Idara ya Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umasikini, Idara ya Ukuzaji Uchumi na Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi.

IDARA YA MIPANGO YA KITAIFA MAENDELEO YA KISEKTA NA KUPUNGUZA UMASIKINI

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Mipango ya Kitaifa Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umasikini ilitengewa jumla ya Shilingi 688.2 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida na jumla ya Shilingi 2,037.8 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2014, Idara ya Mipango ya Kitaifa Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umasikini imeingiziwa Shilingi 504 milioni sawa na asilimia 73.2 ya makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida na Shilingiu 1,029.8 milioni sawa na asilimia 50.5 ya makadirio ya matumizi ya kazi za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umasikini imechapisha jumla ya nakala 300 za vitabu vya Mapitio ya Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2012/2013 na nakala 500 za vitabu vya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2013/2014. Ziara mbili za ufuatiliaji wa Programu na Miradi ya maendeleo zimefanyika ambapo jumla ya programu 18 na miradi 60 ilitembelewa kwa Unguja na Pemba. Lengo la ufuatiliaji huo lilikuwa ni kufanya tathmini juu ya hatua za utekelezaji wa miradi hiyo kuwa inaendana kama ilivyoainishwa katika mpango kazi.

Mhe. Naibu Spika, aidha, idara iliratibu Maabara za Utalii, Mazingira Bora ya Biashara na Upatikanaji wa Rasilimali Fedha kwa lengo la kuendeleza sekta hizi ikiwemo uibuaji wa Programu na Miradi inayotekelezeka kwa haraka na kuleta matokeo mazuri kwa ustawi wa wananchi. Lengo jengine lilikuwa kutafuta Rasilimali Fedha za

utekelezaji wa mipango iliyopangwa.

Mhe. Naibu Spika, idara imezijengea uwezo sekta mbali mbali hususan katika nyanja za ufuatiliaji na tathmini. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara imetoa mafunzo ya siku mbili ya ufuatiliaji na tathmini kwa Maofisa Mipango 30 wa Taasisi za Serikali za Pemba. Aidha, mafunzo juu ya utayarishaji wa malengo, Shabaha, viashiria vya ufuatiliaji na uandishi wa ripoti yalifanyika kwa Wakurugenzi Mipango, Mhe. Naibu Spika, Sera na Utafiti pamoja na Maofisa Mipango Wakuu wa Taasisi za Serikali. Sambamba na mafunzo hayo, idara imewajengea uwezo Maofisa 40 wa Mipango na Uchumi kwa kuwapatia mafunzo ya siku nne juu ya uandaaji na uchambuzi wa Sera. Mafunzo hayo yote yana lengo la kuzijengea uwezo sekta katika kuandaa Miradi na Programu inayozingatia matokeo (*Result-Based Projects*), ufuatiliaji na tathmini, uandaaji wa taarifa za utekelezaji wa miradi pamoja na uandaaji na uchambuzi wa Sera mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, Mikutano ya uhamasishaji na majadiliano na wananchi katika maeneo ya Bumbwisudi na Kiembesamaki Wilaya ya Magharibi imefanyika na kujadili mipango ya maendeleo ya Kitaifa ikiwemo Dira ya Maendeleo 2020 na MKUZA II. Aidha, Idara ya Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umasikini imeandaa warsha tatu za kujadili matokeo ya ukusanyaji wa taarifa za mifumo iliyopo ya ufuatiliaji na tathmini ndani ya sekta za serikali.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umasikini imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kufanya mapitio ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2014/2015 na kuandaa Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2015/2016;
ii. Kutoa mafunzo ya utayarishaji wa miradi, ufuatiliaji na tathmini yenye kuleta matokeo kwa watendaji wa mipango na vitengo vya ufuatiliaji na Tathmini vya Wizara za Serikali;
iii. Kufanya uchambuzi na kuandaa Sera (*Policy brief*) kwa sekta za elimu na Biashara;
iv. Kuratibu utayarishaji wa miradi kwa ajili ya kupelekwa kwa Washirika wa Maendeleo kupata msaada wa udhamini (*Funding*);
v. Kufanya uchambuzi wa hali ya umasikini kwa vijiji vitano na kuandaa taswira ya umasikini (*Poverty profile*) kwa kuzingatia Ripoti ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya;
vi. Kuandaa maonesho ya maadhimisho ya wiki ya umasikini; na
vii. Kufanya ushajihishaji wa Mipango ya Kitaifa (DIRA 2020, MKUZA II, MKUZA IP) kwa wananchi kwenye maeneo tofauti.

Mhe. Naibu Spika, ili Idara ya Mipango ya Kitaifa Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umasikini iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka fedha 2014/2015. Naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi. 441.4 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi 1,888.1 milioni kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

IDARA YA UKUZAJI UCHUMI

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Ukuzaji Uchumi iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 426.7 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi 150 milioni kwa kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2014, Idara ya Ukuzaji Uchumi imeingiziwa jumla ya Shilingi 337.5 milioni sawa na asilimia 79.1 ya makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi milioni 10 sawa na asilimia 6.7 ya makadirio ya matumizi ya kazi za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Ukuzaji Uchumi imefuatilia Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi kwa kutoa taarifa ya Pato la Taifa kwa kila robo mwaka ili kujua ukuaji na mchango wa kila sekta katika Pato la Taifa. Aidha, tathmini ya hali ya mfumko wa bei imefanyika kupitia Kamati ya Kutathmini Hali ya Mfumko wa Bei kila mwezi na kutoa mapendekezo yaliyowasilishwa katika kikao cha Ukomo cha Wizara ya Fedha.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Ukuzaji Uchumi imeandaa mafunzo ya Programu za kifedha (*Financial Programing*) yaliowashirikisha Maofisa saba kutoka Tume ya Mipango, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu, Benki Kuu Tawi la Zanzibar, Bodi ya Mapato ya Zanzibar na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Aidha, idara imewajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ambapo wafanyakazi watatu walipatiwa mafunzo ya muda mrefu katika fani ya uchumi na wafanyakazi sita wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani za uchumi na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hayo, Kitengo cha kutunza Taarifa za Takwimu za Kifedha za Serikali (*GFS*) kimeimarishwa kwa kuongeza wigo wa kukusanya takwimu za Serikali za Mitaa. Idara ya Ukuzaji Uchumi imefanya mapitio ya mfumo wa Utabiri wa Uchumi na Utabiri wa Mapato (*MACMOD* na *Tax Model)* ili kurahisisha kufanya makadirio ya viashiria vya uchumi. Kadhalika, idara imefanya tafiti zinazohusiana na misamaha ya kodi, mwenendo wa bei za mafuta katika Soko la Dunia na uhusiano wa bei za samaki na misimu ya utalii.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Ukuzaji Uchumi imeshiriki katika mikutano pamoja na majadiliano ya mashirikiano ya kikanda kwa lengo la kuishauri serikali kuhusu misimamo mbali mbali ya kuimarisha uchumi. Wafanyakazi watatu wameshiriki katika vikao vya Kikanda vikiwemo vya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*), Mashirikiano ya Jumuiya ya Utatu (*EAC, COMESA* na *SADC*), Umoja wa Afrika (*AU*), Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*) na Umoja wa Nchi za Ulaya (*EU*).

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2014/2015, Idara ya Ukuzaji Uchumi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kutoa taarifa ya Pato la Taifa kwa kila robo mwaka kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na Benki Kuu ili kujua hali ya ukuaji wa kila sekta katika Pato la Taifa;
ii. Kutathmini hali ya mfumko wa bei kila mwezi ili kutoa mapendekezo ya hatua za kudhibiti mfumko wa bei nchini;
iii. Kufanya mapitio ya takwimu na kuimarisha kitengo cha kutunza Taarifa za Takwimu za kifedha za Serikali (*GFS*);
iv. Kufanya tafiti mbili za kiuchumi katika maeneo ya mchango wa wajasiriamali wadogo wadogo na wa kati katika Uchumi na utafiti juu ya Maendeleo ya Viwanda Zanzibar;
v. Kufanya uchambuzi wa tafiti kutoka katika sekta kwa kuzingatia maeneo ya vipaumbele kama yalivyoainishwa katika Agenda za Tafiti za Taifa Zanzibar;
vi. Kuendelea kufanya mapitio ya Modeli ya Uchumi na ya Kodi kila zinapopatikana takwimu mpya ili kufanya makadirio;
vii. Kuratibu mapendekezo ya marekebisho ya kodi kupitia kitengo cha Sera ya Kodi na kutoa ushauri juu ya mwenendo wa kodi;
viii. Kuwapatia wafanyakazi mafunzo juu ya programu ya kifedha ili kuweza kuchambua uchumi na kufanya makadirio ya viashiria vya uchumi kwa kipindi cha robo mwaka;
ix. Kufanya uchambuzi wa nafasi ya kiuchumi Zanzibar;
x. Kushiriki katika vikao vya kitaalamu vya Kikanda ikiwa ni pamoja na vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mashirikiano nchi za Jumuiya ya Umoja wa Ulaya na Mashirikiano ya Jumuiya ya Utatu, (*EAC- COMESA na SADC*) na Umoja wa Afrika;

xi. Kuijengea uwezo Idara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wanne katika ngazi ya Shahada ya pili na muda mfupi wafanyakazi sita katika nyanja za kiuchumi ndani na nje ya nchi; na

xii. Kufanya uchambuzi na kutoa mapendekezo juu ya kasi ya mfumko wa bei kwa kutumia mfumo wa kuondoa bidhaa zinazopanda na kushuka katika mkoba wa bei za bidhaa (*CPI basket*) ujulikanao kwa jina la *"Core Inflation"*.

Mhe. Naibu Spika, ili Idara ya Ukuzaji Uchumi iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 463.7 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi 100 milioni kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

IDARA YA MIPANGO NA MAENDELEO YA WATENDAKAZI

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi iliidhinishiwa Shilingi 149.1 milioni kwa kazi za kawaida na Shilingi 342 milioni kwa matumizi ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi 2014, Idara hii iliingiziwa Shilingi 195.1 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida sawa na asilimia 130.9 ya makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi 147.1 milioni sawa na asilimia 43 ya makadirio ya kazi za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi imekamilisha utafiti juu ya umakini wa mafunzo ya amali katika ajira na ripoti yake imewasilishwa katika majadiliano ya mikutano ya wadau Unguja na Pemba. Idara imewajengea uwezo watendaji wake kwa kudhamini mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi wawili juu ya masuala ya Utawala wa Sheria na Uchumi nchini Singapore na China.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo, idara imeratibu ushiriki wa Maofisa wake katika mikutano ya Kikanda na Kimataifa inayohusiana na Masuala ya Idadi ya Watu nchini Ethiopia na Marekani. Maazimio yaliyopitishwa katika mikutano hiyo, yatasaidia katika matayarisho ya Malengo ya Kimataifa baada ya mwaka 2015 (*Post 2015 Sustainable Development Goals*) kufuatia kukamilika kwa malengo ya awali ya millenia (*MDGs*).

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuratibu shughuli za Watendakazi, Idadi ya Watu na Ustawi wa Mama na Mtoto katika ngazi mbalimbali;

ii. Kuandaa mafunzo kwa Maofisa Utumishi wa Taasisi za Serikali na binafsi juu ya usimamizi na taratibu za ustaafu ili kuimarisha utekelezaji wa masuala ya ustaafu katika sehemu za kazi;

iii. Kuibua maeneo ya tafiti kuhusiana na Rasilimali Watu ya Zanzibar, kutayarisha maandiko ya awali na kuratibu utekelezaji wa tafiti hizo;

iv. Kufanya mapitio ya taarifa za msingi za Wilaya (*updating of district profiles*) ili ziendane na wakati;

v. Kutoa mafunzo ya maandalizi ya mipango ya Shehia kwa kutumia fursa na changamoto za kimaendeleo zinazobainika kutokana na tathmini zinazofanyika; na

vi. Kuendelea na ufuatiliaji wa utekelezaji programu ya *YCSPD* katika ngazi ya Wilaya na Shehia za Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, ili Idara ya Mipango na Watendakazi iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 243.8 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi 161.9 milioni kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

DIVISHENI YA UTUMISHI NA UENDESHAJI

Mhe. Naibu Spika, jukumu kuu la Divisheni ya Utumishi na Uendeshaji ni kusimamia shughuli zote za utendaji na utumishi ndani ya Tume ya Mipango pamoja na kuimarisha mazingira bora ya kazi. Katika kuimarisha shughuli za ununuzi na uuzaji wa mali za Serikali, Divisheni imeanzisha Kitengo cha Manunuzi ili kusimamia na kuratibu manunuzi yote ya Tume ya Mipango. Aidha, Bodi ya Zabuni imeanzishwa na tayari imekutana mara mbili.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo, Divisheni pia imeratibu na kusimamia mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi wawili katika fani za ukatibu Mukhtasi. Vile vile, Divisheni imewapatia wafanyakazi likizo na stahiki zao, kutengeneza makisio ya Mishahara (*Nominal Roll*) ya wafanyakazi wa Tume ya Mipango kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Divisheni ya Utumishi na Uendeshaji imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuwajengea uwezo wa kiutendaji wafanyakazi wawili wa Tume ya Mipango kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu katika fani za uchumi na mipango;
ii. Kuwapatia watendaji 13 mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi katika fani zinazohusiana na kazi zao;
iii. Kuandaa mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi wa Tume ya Mipango kuhusu Kanuni ya Tume ya Mipango na kuwapatia miongozo ya kazi;
iv. Kuratibu na kuwezesha vikao vya Tume ya Mipango pamoja na vikao vya Kamati ya Wataalamu;
v. Kuendesha vikao 12 vya Bodi ya Zabuni na vikao 5 vya Kamati ya Ukaguzi wa Ndani;
vi. Kulipia gharama mbali mbali za uendeshaji Ofisi na kutoa huduma za Kiutawala;
vii. Kuijengea uwezo Ofisi ya Uratibu Tume ya Mipango Pemba kwa kuimarisha upatikanaji wa nyenzo na vifaa vya kiutendaji; na
viii. Kutoa mafunzo Pemba juu ya kuainisha masuala mtambuka (jinsia, mabadiliko ya tabia nchini, Virusi vya Ukimwi na Ukimwi).

Mhe. Naibu Spika, ili Divisheni ya Utumishi na Uendeshaji iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 810.1 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 1,300 milioni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi 2,350 milioni kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi 2014, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeingiziwa Shilingi 971.5 milioni sawa na asilimia 70.4 ya makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi 1,973.2 milioni sawa na asilimia 84 ya makadirio ya matumizi ya kazi za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeendelea na ukusanyaji wa Takwimu za Ofisini (*Routine data*) ambazo huwa zinatumika katika kupanga maendeleo na kufanya tathmini ya hali ya uchumi na kijamii nchini. Aidha, ofisi hii imekusanya takwimu za utafiti wa hali ya uchumi na jamii, uajiri na mapato, faharisi za bei, takwimu za pato la Taifa kwa kila robo mwaka pamoja na kukusanya takwimu kati ya Zanzibar na Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri bado dakika tano.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika. Ahsante. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea na zoezi la ukusanyaji wa takwimu za Ofisini (*Routine data*);
ii. Kukusanya takwimu katika tafiti za Hali ya Uchumi na Jamii, Uajiri na Mapato, ukusanyaji wa takwimu za Faharisi ya bei na ukusanyaji wa takwimu za pato la taifa kwa robo mwaka; na
iii. Kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, ili Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 1,380 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida na Shilingi 6,700 milioni kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imetekeleza Programu na Miradi ifuatayo:-

i. Mradi wa Uimarishaji wa Nyumba za Viongozi na Nyumba za Serikali (*State Lodges)*;
ii. Mradi wa Kuimarisha Mawasiliano – Ikulu;
iii. Mradi wa Uimarishaji wa Juhudi za Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar;
iv. Mradi wa Kuratibu Utekelezaji wa *MCA-T;*
v. Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini yenye Kuleta Matokeo ya MKUZA II;
vi. Programu ya Kujenga Uwezo wa Utekelezaji kwa Taasisi za Serikali;
vii. Mradi wa Kuratibu Utekelezaji wa MKURABITA;
viii. Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko na Kuimarisha Tume ya Mipango;
ix. Mradi wa Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;
x. Mradi wa Utafiti wa Hali ya Utumishi Nchini;
xi. Mradi wa Kuoanisha Masuala ya Idadi ya Watu, Afya ya Uzazi, Jinsia na Umasikini;
xii. Programu ya Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Mama na Mtoto (*YCSPD*);
xiii. Mradi wa Uimarishaji wa Takwimu; na
xiv. Mradi wa Uimarishaji Takwimu Tanzania (*STATCAP*).

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ilitengewa jumla ya Shilingi 6,109.8 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotajwa hapo juu. Hadi kufikia Machi 2014, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi iliingiziwa Shilingi 3,840.1 milioni sawa na asilimia 62.9 ya fedha zilizoidhinishwa.

MRADI WA UIMARISHAJI WA NYUMBA ZA VIONGOZI NA NYUMBA ZA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mradi wa Uimarishaji wa Nyumba za Viongozi na Nyumba za Serikali uliidhinishiwa jumla ya Shilingi 600 milioni. Hadi kufikia Machi 2014, Mradi huu uliingiziwa Shilingi 300 milioni sawa na asilimia 50 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Naibu Spika, Ikulu Kuu ya Mnazi Mmoja imefanyiwa matengenezo sehemu za madirisha na milango ili kurejesha uhalisia wake. Aidha, ujenzi wa nyumba mbili za wafanyakazi pamoja na sehemu ya mapokezi katika Ikulu ya Laibon Dar-es-Salaam unaendelea. Sambamba na hayo, kazi za ujenzi wa uzio (*Fence*) katika pande tatu zinazoizunguka Ikulu ya Mkoani umekamilika na ujenzi wa nyumba ya wafanyakazi pamoja na sehemu ya "*Dining room"* Mkoani umefikia hatua ya kuezekwa. Aidha, ujenzi wa mlango mkuu wa kuingilia Ikulu ya Mkoani umekamilika. Kadhalika, matengenezo ya paa la Ikulu ya Chake Chake yamefanyika kwa kuweka "*Water proofing membrane*".

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mradi wa Uimarishaji wa Nyumba za Viongozi na Nyumba za Serikali umetengewa jumla ya Shilingi 530 milioni na umepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i Kufanya matengenezo makubwa katika Ikulu ya Kibweni;
ii Kujenga nyumba ya wafanyakazi na sehemu ya Mapokezi katika Ikulu Ndogo ya Dodoma;
iii Kuifanyia matengenezo nyumba ya Ikulu ya Mazizini I;
iv Kufanya matengenezo ya Ikulu Kuu ya Mnazi Mmoja na Ikulu ya Migombani;
v Kuendelea na ujenzi wa nyumba ya mapumziko ya Micheweni; na
vi Kujenga uzio nyumba ya mapumziko Bwefumu na Mkokotoni.

MRADI WA KUIMARISHA MAWASILIANO - IKULU

Mhe. Naibu Spika, mradi huu maelezo yake yanasomeka katika kifungu cha 111. Nataka kusema tu kwamba mradu huu utatekelezwa kupitia programu ya kujenga uwezo na utekelezaji kwa Taasisi za Serikali unaofadhiliwa na *UNDP*.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mradi wa Kuimarisha Mawasiliano – Ikulu uliidhinishiwa jumla ya Shilingi 150 milioni. Hadi kufikia Machi 2014, mradi huu uliingiziwa jumla ya Shilingi 150 milioni sawa na asilimia 100 ya fedha zilizoidhinishwa ambazo zilitumika kwa ununuzi wa gari moja la matangazo (*Mobile Public Address System*) pamoja na vifaa vyake. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, mradi huu utatekelezwa kupitia Programu ya Kujenga Uwezo wa Utekelezaji kwa Taasisi za Serikali unaofadhiliwa na *UNDP*.

MRADI WA UIMARISHAJI WA JUHUDI ZA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mradi wa Uimarishaji wa Juhudi za Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar uliidhinishiwa jumla ya Shilingi 480 milioni. Hadi kufikia Machi 2014, mradi huu uliingiziwa Shilingi 229.9 milioni sawa na asilimia 47.9 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Naibu Spika, kupitia Mradi wa Uimarishaji wa Juhudi za Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar unaofadhiliwa na Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa *UNDP* umeweza kununua gari moja, samani za Ofisi, vitendea kazi vya Ofisi (kompyuta, mashine ya kurudufia) na kuunganisha huduma za Simu na *Internet* katika jengo linalotumiwa na Mamlaka.

Mhe. Naibu Spika, kupitia mradi huu, imetolewa elimu juu ya rushwa na uhujumu wa uchumi kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Viongozi Waandamizi wa Serikali wakiwemo Maofisa Tawala wa Mikoa na Wilaya, Makamishna wa Polisi, Wakurugenzi Uendeshaji na Utumishi wa Wizara za SMZ, Wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika ya Umma na Wakuu wa Taasisi zinazojitegemea. Aidha, mradi pia umesaidia kuwapatia mafunzo ya muda mfupi ya uchunguzi na uandishi wa ushauri wa kisheria kwa Wafanyakazi wa

Mamlaka. Sambamba na hayo, mradi umeiwezesha Mamlaka kuadhimisha Siku ya Kuzuia Rushwa Duniani ambayo hufanyika mwezi wa Disemba ya kila mwaka.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mradi wa Uimarishaji wa Juhudi za Kuzuia Rushwa Zanzibar umetengewa jumla ya TZS. 621.7 milioni na umepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuandaa Mpango Mkakati wa Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi pamoja na Mpango Kazi;
ii. Kufanya Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo pamoja na kuandaa Mpango wa Mafunzo wa Mamlaka (*Capacity Needs Assessment and Training Programme*);
iii. Kuandaa Kanuni ya Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi;
iv. Kuanzisha na kuendeleza Tovuti (*Website*) ya Mamlaka;
v. Kuwajengea uwezo wafanyakazi 20 kwa kuwapatia mafunzo ya vitendo pamoja na kuwapeleka wafanyakazi wanne nje ya nchi kuhudhuria mkutano wa Kimataifa juu ya rushwa;
vi. Kuelimisha jamii juu ya mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu wa uchumi kwa kutumia vyombo vya habari, vipeperushi na mikutano ya hadhara; na
vii. Kununua vifaa vya uchunguzi na kutoa mafunzo ya namna ya kuvitumia.

MRADI WA KURATIBU UTEKELEZAJI WA CHANGAMOTO ZA MILENIA *MCA-T*

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mradi wa Kuratibu Utekelezaji Changamoto za Milenia – *"Millenium Challenge Account Tanzania" (MCA–T)* uliidhinishiwa jumla ya TZS 50 milioni. Hadi kufikia Machi 2014, mradi huu uliingiziwa TZS. 15.5 milioni sawa na asilimia 31.1 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Naibu Spika, Kupitia mradi huu, vikao vitatu vimefanyika ambavyo vimepokea tathmini ya utekelezaji na kujadili maendeleo ya mradi. Utekelezaji wa mradi huu umekamilika katika mwaka 2013/2014. Mradi huu umekamilika kwa mafanikio makubwa ambapo wananchi mbali mbali wamefaidika na ujenzi barabara za Kipangani - Kangagani, Chwale - Likoni, Mzambarau Takao – Pandani – Finya, Mzambarau Karim – Mapofu na Bahanasa – Daya – Mtambwe.

MPANGO WA UFUATILIAJI NA TATHMINI YENYE KULETA MATOKEO YA MKUZA II

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini yenye Kuleta Matokeo ya MKUZA II uliidhinishiwa jumla ya TZS. 750 milioni. Hadi kufikia Machi 2014, mpango huu uliingiziwa TZS. 264.8 milioni sawa na asilimia 35.3 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Naibu Spika, kupitia Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini yenye Kuleta Matokeo ya MKUZA II umewezesha kufanyika kwa warsha tatu za kujadili matokeo ya ukusanyaji wa taarifa za mifumo iliyopo ya ufuatiliaji na tathmini ndani ya sekta za serikali kwa ajili ya mfumo wa kisasa wa ufuatiliaji wa MKUZA II. Aidha, mafunzo ya siku mbili juu ya majukumu na uandaaji wa mpango kazi yamefanyika kwa Kamati za Ufuatiliaji na Tathmini, kazi ya mapitio ya Sekta ya Fedha imekamilika na nakala 300 za ripoti zimechapishwa. Aidha, ripoti ya utekelezaji wa MKUZA II kwa mwaka 2012/2013 imekamilika na ipo katika hatua ya uchapishaji.

Mhe. Naibu Spika, mafunzo ya dhana ya ufuatiliaji na tathmini kwa Maofisa Mipango 30 yametolewa. Aidha, mafunzo juu ya utayarishaji wa malengo, Shabaha, viashiria vya ufuatiliaji na uandishi wa ripoti yamefanyika kwa upande wa Unguja na vikao vya Kamati za ufuatiliaji na utekelezaji wa MKUZA *Technical Working Groups (TWGs)* pia vimefanyika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, ningekushauri kwamba ungesema sehemu iliyobakia iingie kwenye *Hansard* umalizie ukurasa wa 77 wenye Mapato yale unakusanya na umalizie na kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa maelezo yako.

Mhe. Naibu Spika, kuanzia kifungu namba 118 mpaka 151 viingie kwenye *Hansard* kutokana na muda wingi unajua wizara yetu kubwa na mambo mengi muhimu. Kwa hiyo, naomba radhi, lakini naomba sana mambo yote yaingie kwenye *Hansard* na yanaweza kusomeka vizuri kwenye kitabu chetu cha Bajeti.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini yenye Kuleta Matokeo ya MKUZA II umetengewa jumla ya TZS. 768.3 milioni na umepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kukamilisha kazi ya uandaaji wa mfumo wa Kitaifa wa kisasa wa ufuatiliaji na tathmini;
ii. Kufanya mapitio ya sekta ya Kilimo na Nishati;
iii. Kuandaa Ripoti ya Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo ya Millenia (*MDG*);
iv. Kuandaa Ripoti ya Maendeleo ya Watu wa Zanzibar (*ZHDR*);
v. Kuandaa vikao vya Kamati za Ufuatiliaji wa MKUZA II (*TWGs*);
vi. Kutoa mafunzo kwa Maofisa Mipango na Maofisa Ufuatiliaji na Tathmini wa Wizara na Taasisi za Serikali; na
vii. Kuandaa Ripoti ya Utekelezaji wa MKUZA II (MKUZA AIR).

PROGRAMU YA KUJENGA UWEZO WA UTEKELEZAJI KWA TAASISI ZA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Programu ya Kujenga Uwezo wa Utekelezaji kwa Taasisi za Serikali iliidhinishiwa jumla ya TZS. 915 milioni. Hadi kufikia Machi 2014, Programu hii iliingiziwa TZS. 658.5 milioni sawa na asilimia 72 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Naibu Spika, kupitia Programu hii Idara imeweza kufanya tathmini ya mahitaji ya kiutendaji ya Taasisi na Idara ziliopo chini ya Tume ya Mipango kwa lengo la kuainisha mahitaji halisi ya vifaa, mafunzo kwa watendaji na muundo wake katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Aidha, kikao kimoja cha Bodi ya mradi kilichojadili utekelezaji wa kazi za Programu kilifanyika. Sambamba na hayo, kazi ya uwekaji wa mtandao wa ndani wa mawasiliano wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na uwekaji wa Tovuti imefanyika.

Mhe. Naibu Spika, kupitia Programu hii, Idara imeweza kukamilisha Mpango Mkakati wa mwaka 2014/2020 na Mpango Mkuu wa Utafiti wa mwaka 2013/2018 unaozingatia Jinsia kwa Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais na malipo ya mwisho ya Washauri elekezi kutoka "*ECOM Research Group"* kwa utayarishaji wa kazi hiyo yamefanyika. Aidha, ripoti ya Tathmini ya Mahitaji ya Uratibu na Usimamizi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imekamilika na vikao katika ngazi ya Makatibu Wakuu vimefanyika. Sambamba na hayo vifaa vya mawasiliano kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais vimenunuliwa na ufungwaji wake umekamilika.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Programu ya Kujenga Uwezo Taasisi za Serikali imetengewa jumla ya TZS 769.8 milioni na imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kutoa mafunzo kwa watendaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwenye fani mbali mbali zikiwemo Uchambuzi wa Sera, Mfumo wa Ufuatiliaji wa kazi kwa matokeo ya Utafiti na Uandishi wa ripoti;
ii. Kutayarisha mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;
iii. Kukusanya maoni kwa jamii kuhusu utaratibu wa usambazaji wa taarifa mbali mbali za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ili hatimae maoni hayo yaweze kutumika katika kuimarisha mfumo wa mawasiliano kwa wananchi kwa ujumla;
iv. Kuanzisha mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, ikiwemo ununuzi wa vifaa vya TEKNOHAMA na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi;
v. Kutoa mafunzo kwa Wakurugenzi wa Idara za Mipango, Sera na Utafiti pamoja na maofisa wengine wa Mawizara kuhusu uratibu wa shughuli za Serikali chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;
vi. Kuimarisha utendaji wa Tovuti (*Website*) ya Serikali chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;
vii. Kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais;
viii. Kutayarisha Mpango Mkakati wa Tume ya Mipango;
ix. Kukamilisha Kanuni ya Tume ya Mipango;
x. Kukamilisha Mpango wa Utekelezaji wa Tume ya Mipango ili kuiwezesha Tume hiyo kufanya kazi zake kwa ufanisi ikiwemo uratibu wa Mipango ya Kitaifa, Ufuatiliaji na Tathmini;
xi. Kutoa mafunzo maalum kwa Maofisa 30 wa Tume ya Mipango Unguja na Pemba kwa lengo la kuwajengea uwezo katika fani mbalimbali ikiwemo Uchambuzi wa Sera;

xii. Kuikarabati Maktaba ya Tume ya Mipango na kuipatia vifaa vya kisasa;
xiii. Ununuzi wa vifaa vya Ofisi za Unguja na Pemba.

MRADI WA KURATIBU UTEKELEZAJI WA MKURABITA

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mradi wa Kuratibu Utekelezaji wa MKURABITA uliidhinishiwa jumla ya TZS 262.8 milioni. Hadi kufikia Machi 2014, mradi huu uliingiziwa jumla ya TZS. 59.3 milioni sawa na asilimia 22.6 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Naibu Spika, kupitia Mradi wa Kuratibu Utekelezaji wa MKURABITA, umewezesha kuwatambua wafanyabiashara wadogo wadogo 587 na kupewa mafunzo ya Ujasiriamali kwa Wilaya ya Kaskazini 'B'.Aidha, vikao viwili vya Kamati ya Uongozi ya MKURABITA - Zanzibar vimefanyika na kutoa maamuzi mbali mbali ya utekelezaji wa mradi pamoja na kuidhinisha bajeti na kuwajumuisha Mrajis wa Ardhi na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mradi wa Kuratibu Utekelezaji wa MKURABITA umetengewa jumla ya TZS. 200 milioni na umepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kurasimisha Ardhi Mijini na Vijijini kwa Wilaya ya Kaskazini "B" eneo la Mahonda kwa Unguja na Kijiji cha Limbani kwa Pemba;
ii. Kuwatambua wafanyabiashara wadogo wadogo 1,000 na kuwajengea uwezo kwa Wilaya za Unguja na Pemba; na
iii. Kuratibu vikao vya Kamati ya Uongozi na Kamati ya Wataalamu.

MRADI WA KUIFANYIA MABADILIKO NA KUIMARISHA TUME YA MIPANGO

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko na Kuimarisha Tume ya Mipango uliidhinishiwa jumla ya TZS 60 milioni. Hadi kufikia Machi 2014, mradi huu uliingiziwa TZS. 31.7 milioni sawa na asilimia 52.8 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Naibu Spika, kazi ya utayarishaji wa Kanuni ya Tume ya Mipango inaendelea na imefikia hatua za kumalizia kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa kwenye kikao cha Watendaji Wakuu kilichojadili Rasimu ya Kanuni hiyo. Aidha, Rasimu ya awali ya Mpango Mkakati wa Tume ya Mipango imetayarishwa na inatarajiwa kuwasilishwa katika kikao cha Kamati ya Uongozi wa Tume kwa majadiliano. Sambamba na hayo, kupitia mradi huu, wafanyakazi wa Tume ya Mipango wamejengewa uelewa juu ya Sheria ya Tume ya Mipango.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko na Kuimarisha Tume ya Mipango umetengewa jumla ya TZS. 150 milioni na umepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuanzisha mfumo wa usimamizi wa programu na miradi ya maendeleo (*Database Management System*);
ii. Kuanzisha Tovuti (*Website*) ya Tume ya Mipango; na
iii. Kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo watendaji wa Tume ya Mipango juu ya mfumo wa programu ya usimamizi wa miradi ya maendeleo (*Project Management System*).

MRADI WA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mradi wa Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ulitengewa jumla ya TZS. 150 milioni. Hadi kufikia Machi 2014, mradi huu uliingiziwa TZS. 10 milioni sawa na asilimia 6.7 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Naibu Spika, kupitia mradi huu, umewezesha kuimarisha mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa kuwajengea uwezo wafanyakazi wanne wa kitengo ambao wameshiriki katika mafunzo ya vitendo huko Tanzania Bara. Aidha, kwa kushirikiana na Washauri Elekezi kutoka Benki ya Dunia wametembelea Taasisi mbali mbali za Serikali na Sekta Binafsi kwa ajili ya matayarisho ya Sera ya Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na

Sekta Binafsi (*PPP*). Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, mradi huu fedha zake zimetengwa katika Programu ya upatikanaji wa Rasilimali Fedha iliyopo Wizara ya fedha.

MRADI WA UTAFITI WA HALI YA UTUMISHI NCHINI

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mradi wa Utafiti wa Hali ya Utumishi Nchini uliidhinishiwa jumla ya TZS. 150 milioni. Hadi kufikia Machi 2014, mradi huu uliingiziwa TZS. 91 milioni sawa na asilimia 60.6 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Naibu Spika, kupitia Mradi huu, taarifa za Watendakazi kutoka Taasisi mbali mbali Unguja na Pemba zimekusanywa. Aidha, taarifa zilizokusanywa zimefanyiwa uchambuzi pamoja na kutayarishwa jadweli ambazo zitatumika wakati wa maandalizi ya ripoti.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2014/2015, Mradi wa Utafiti wa Hali ya Utumishi Nchini umepangiwa kutumia jumla ya TZS. 61.9 milioni na umepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kukamilisha hatua za utafiti wa hali ya utumishi nchini kwa kuwasilisha ripoti kwa wadau Unguja na Pemba;
ii. Kufanya mapitio ya vipaumbele vya mahitaji ya wataalamu nchini; na
iii. Kuandaa Sera ya Maendeleo ya Rasilimali Watu Zanzibar.

MRADI WA KUOANISHA MASUALA YA IDADI YA WATU, AFYA YA UZAZI, JINSIA NA UMASIKINI

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mradi wa Kuoanisha Masuala ya Idadi ya Watu, Afya ya Uzazi, Jinsia na Umasikini uliidhinishiwa jumla ya TZS. 140 milioni. Hadi kufikia Machi 2014, mradi huu uliingiziwa TZS. 38.5 milioni sawa na asilimia 27.5 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Naibu Spika, kupitia Mradi huu Rasimu ya ripoti ya mwaka 2013 juu ya masuala ya idadi ya watu yenye ujumbe wa "Uzazi Salama" imetayarishwa na tayari imejadiliwa na kikundi cha wataalamu ili kuimarisha ubora wake. Mradi pia umewezesha kushiriki kikamilifu katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Idadi ya Watu Duniani yaliyofanyika Dar-es-Salaam ambayo yalifanyika sambamba na uzinduzi wa Ripoti ya Dunia ya Masuala ya Idadi ya Watu.

Mhe. Naibu Spika, kwa kushirikiana na *UNFPA*, Mradi umewezesha kufanyika kwa zoezi la majaribio la Daftari la Shehia lililoandaliwa upya katika Wilaya mbili za Wete na Kaskazini "A" Unguja. Majaribio hayo yalitanguliwa na uchapishaji wa madaftari mapya na mafunzo kwa watendaji wa Shehia 30 za Wilaya hizo. Aidha, Rasimu ya awali ya andiko la kitaalamu (*Thematic Paper*) juu ya athari za idadi ya watu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii imetayarishwa pamoja na kuwezesha kufanyika kwa mikutano mitatu ya Wadau wa Masuala ya Idadi ya Watu.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Mradi wa Kuoanisha Masuala ya Idadi ya Watu, Afya ya Uzazi, Jinsia na Umasikini umepangiwa kutumia jumla ya TZS. 100 milioni na umepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kushiriki katika maandalizi na maadhimisho ya Siku ya Idadi ya Watu Duniani pamoja na uzinduzi wa ripoti ya masuala ya idadi ya watu duniani 2014/2015;
ii. Kutayarisha ripoti ya mwaka 2014 juu ya Masuala ya Idadi ya Watu Zanzibar;
iii. Kuandaa mikutano minne ya watekelezaji wa masuala ya Idadi ya Watu Zanzibar;
iv. Kuifanyia mapitio Sera ya Idadi ya Watu na Maendeleo ya Zanzibar ili iendane na wakati;
v. Kuratibu michakato ya kujengea uwezo Shehia katika utekelezaji wa Daftari la Shehia; na
vi. Kuratibu uanzishaji wa *Database* za Wilaya zitakazopokea mihutasari ya takwimu kutoka ngazi ya Shehia.

PROGRAMU YA UHAI, HIFADHI NA MAENDELEO YA MAMA NA MTOTO (*YCSPD*)

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Programu ya Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Mama na Mtoto iliidhinishiwa jumla ya TZS. 52 milioni. Hadi kufikia Machi 2014, Programu hii iliingiziwa TZS. 17.7 milioni sawa na asilimia 33.9 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Naibu Spika, Programu ya Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Mama na Mtoto imewezesha kufanyika kwa tathmini juu ya mapungufu ya hali na ustawi wa mama na mtoto katika Shehia 25 kwenye Wilaya mbili za Pemba na tatu za Unguja. Aidha, mkutano mmoja wa wataalamu uliojadili mafanikio na changamoto za Programu ya *YCSPD* umefanyika.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hayo, ufuatiliaji wa utekelezaji wa Programu katika Wilaya za Mkoani, Wete na Chake Chake umefanyika. Tafsiri ya viashiria vya takwimu za kijamii pamoja na fomu za ukusanyaji wa taarifa za magonjwa kwa lugha ya Kiswahili ambayo itatumika katika ngazi ya jamii vimeandaliwa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kupitia Kitengo cha Kusimamia Mfumo wa Taarifa za Afya (*Health Management Information System*). Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Programu hii haikutengewa fedha na shughuli zake zimehamishimiwa katika kazi za kawaida.

MRADI WA UIMARISHAJI TAKWIMU ZANZIBAR

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mradi huu ulitengewa jumla ya TZS. 250 milioni. Hadi Machi 2014, Mradi uliingiziwa TZS. 92.5 milioni sawa na asilimia 37 ya fedha zilizotengwa.

Mhe. Naibu Spika, Mradi umewezesha ukusanyaji wa takwimu za Ofisini (*Routine data*) ambazo huwa zinatumika katika kupanga maendeleo na kufanya tathmini ya Hali ya Uchumi na Kijamii nchini. Mradi pia umewezesha kufanyika kwa utafiti wa Hali ya Uchumi na Kijamii wa mwaka 2013. Aidha, Mradi umekusanya takwimu za uajiri na mapato, faharisi za bei, takwimu za Pato la Taifa kwa kila robo mwaka. Sambamba na hayo, Mradi umewawezesha wafanyakazi kushiriki katika mikutano ya Kitaalamu ndani na nje ya nchi pamoja na kushiriki katika makongamano na semina mbali mbali zinazohusu masuala ya takwimu.

Mhe. Naibu Spika, kwa msaada wa Washirika mbali mbali wa maendeleo na kwa mashirikiano na Ofisi ya Taifa ya Takwimu Tanzania, Mradi umesaidia kutekeleza Mpango wa Uchambuzi wa Takwimu za Sensa ya Watu na Makaazi ya Mwaka 2012 na kutoa taarifa zake katika kila hatua. Aidha, tafiti mbali mbali zikiwemo Utafiti wa Sekta Isiyo Rasmi (*2013/2014 Zanzibar Informal Sector Survey*), Utafiti wa Hali ya Nguvu Kazi Zanzibar (*2014 Zanzibar Integrated Labour Force Survey*), Utafiti wa Viashiria vya Kiuchumi na Kijamii (*2013 Tanzania Panel Survey*) na Utafiti wa Sekta ya Biashara, Usafiri na Ujenzi 2013/2014 (*Integrated Survey on Trade, Transport and Communication*) zimefanyika. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, shughuli za mradi huu zitatekelezwa kupitia bajeti ya kazi za kawaida.

MRADI WA UIMARISHAJI TAKWIMU TANZANIA (*STATCAP*)

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mradi wa Uimarishaji Takwimu Tanzania uliidhinishiwa jumla ya TZS. 2,100 milioni. Hadi kufikia Machi 2014, Mradi huu uliingiziwa TZS. 1,880.7 milioni sawa na asilimia 89.6 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Naibu Spika, Mradi wa Uimarishaji Takwimu Tanzania umewezesha kuandaliwa kwa *"Zanzibar Statistical Abstract"* ambayo imejumuisha taarifa mbali mbali za Takwimu za Kiuchumi na Kijamii za mwaka 2012. Aidha, kupitia Mpango huu wafanyakazi 11 wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali wamejengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Shahada ya Pili, Shahada ya Kwanza na Stashahada katika fani za Takwimu, Uchumi na Fedha, *"Gegraphical Information System" (GIS)* na Utawala. Wafanyakazi wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali pia wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani ya Takwimu, uandishi wa ripoti, uchambuzi wa takwimu, utawala na uongozi, fedha, ukaguzi wa hesabu na manunuzi.

Mhe. Naibu Spika, katika kuweka mazingira bora ya utendaji kazi, Mradi wa Uimarishaji Takwimu Tanzania umewezesha kukamilika kazi za usanifu na uchoraji wa ramani ya jengo la Makao Makuu ya Ofisi ya Mtakwimu

Mkuu wa Serikali. Mifumo ya uwekaji na utoaji wa takwimu rasmi kwa sekta za elimu, afya, vyuo vya mafunzo, polisi, jinsia, utalii pamoja na utoaji wa takwimu za vizazi na vifo, ndoa na talaka imeimarishwa. Aidha, kazi za uwekaji na utoaji wa takwimu katika ngazi za Wilaya zimeanza. Sambamba na hayo, mifumo ya utoaji na uhifadhi wa takwimu kwa kutumia mitandao ya *"Tanzania Socio-economic Database" (TSED)* na *"National Data Achieving"* (*NADA*) imeimarishwa.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Mradi wa Uimarishaji Takwimu Tanzania umetengewa jumla ya TZS. 6,700 milioni na umepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kufanya utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (*HBS*) wa mwaka 2014/2015;
ii. Kuendelea na kazi ya utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi (*ILFS*) wa mwaka 2013/2014;
iii. Kukuza taaluma ya Maofisa Takwimu kwa kuendelea kugharamia mafunzo kwa Maofisa wanane wanaondelea na masomo yao katika ngazi za Shahada ya Kwanza na Maofisa wawili katika Shahada ya Pili;
iv. Kuandaa Kanuni ya Sheria ya Takwimu ya Zanzibar;
v. Kufanya mapitio ya miongozo ya kazi kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu;
vi. Kuongeza uelewa na ufahamu juu ya umuhimu na matumizi ya takwimu kwa wadau mbali mbali;
vii. Kushiriki katika Mikutano, Warsha na Makongamano ya kitakwimu ndani na nje ya nchi;
viii. Kuendelea na kazi za ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji wa takwimu za Kiuchumi na Kijamii za mwaka 2014; na
ix. Kuanza kazi za ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Ofisi ya Mtakwimu Mkuu Zanzibar.

MRADI WA KUIMARISHA KITENGO CHA UTAFITI

Mhe. Naibu Spika, Mradi wa Kuimarisha Kitengo cha Utafiti ni mradi mpya ambao unatarajiwa kuanza kutekelezwa katika mwaka 2014/2015. Lengo la mradi huu ni kuimarisha kitengo cha tafiti mbali mbali za kiuchumi Zanzibar. Aidha, mradi huu una azma ya kushirikiana na Taasisi mbali mbali katika kuibua na kusimamia tafiti.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Mradi wa Kuimarisha Kitengo cha Utafiti umetengewa jumla ya TZS. 100 milioni na umepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kutoa mafunzo kwa watendaji juu ya dhana ya utafiti wa Uchumi;
ii. Kutayarisha muongozo wa ufanyaji wa tafiti kwa Taasisi za Serikali; na
iii. Kuandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini za tafiti za kiuchumi.

JUMLA YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilipangiwa kukusanya jumla ya TZS.15 milioni. Hadi kufikia Machi 2014, jumla ya TZS. 13.2 milioni zimekusanywa sawa na asilimia 88 ya makadirio ya ukusanyaji.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatarajia kukusanya jumla ya TZS.18 milioni.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi iliidhinishiwa matumizi ya jumla ya TZS. 18,807.7milioni. Kati ya hizo, TZS 12,697.9 milioni ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na TZS. 6,109.8 milioni kwa matumizi ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2014, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeingiziwa jumla ya TZS. 12,305.4 milioni sawa na asilimia 65.4. Kati ya hizo, TZS. 8,465.3 milioni ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida sawa na asilimia 66.7 na TZS. 3,840.1 milioni kwa matumizi ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 62.9 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mhe. Naibu Spika, ili Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya TZS. 23,552.9 milioni. Kati ya hizo TZS. 13,551.2 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida na TZS. 10,001.7 milioni kwa matumizi ya miradi ya maendeleo.

HITIMISHO

Mhe. Naibu Spika, kwa kumaliza hotuba yangu, naomba kuchukua fursa nyengine tena kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake makini wa kusimamia Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kuendelea kunipa dhamana ya kuingoza Ofisi hii. Aidha, natoa shukurani zangu za dhati kwa wananchi wa Zanzibar kwa kuendeleza hali ya amani na utulivu iliyopo. Siku zote Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kulisimamia suala hilo kwa nguvu zake zote na kuwaunga mkono Wananchi katika jitihada hizo.

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, napenda kuwashukuru kwa dhati Washirika wa Maendeleo wanaoshirikiana nasi katika kutekeleza Programu na Miradi mbali mbali katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, hususan Serikali ya Marekani, China, India, Uingereza, Mashirika na Taasisi za Kimataifa za Jumuiya ya Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Mipango na Maendeleo (*UNDP*), Shirika la Kuhudumia Watoto Ulimwenguni (*UNICEF*), Shirika la Kimataifa linaloshughulikia Masuala ya Idadi ya Watu Ulimwenguni (*UNFPA*), Shirika la Uhamiaji la Kimataifa (*OIM*), *UNHCR*, *ACP* na Benki ya Dunia pamoja na wengine wote ambao kwa bahati mbaya nimesahau kuwataja hapa.

Mhe. Naibu Spika, mwisho, nawashukuru Viongozi, Watendaji na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ushirikiano wao wa karibu wanaoendelea kunipa kila siku. Kwa mara nyengine tena, napenda kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Dimani kwa ushirikiano wanaonipa katika kuliletea maendeleo Jimbo letu pamoja na ustahamilivu wao kwa muda wote ninaoshughulikia majukumu ya Kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hotuba hii nimejumuisha viambatanisho mbali mbali. Naomba viambatanisho hivyo vichukuliwe kuwa ni vielelezo vya hoja hii. Aidha, Hotuba hii itapatikana pia katika Tovuti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa anwani ya *www.ikuluzanzibar.go.tz***.**

Mhe. Naibu Spika, nawashukuru wote kwa kunisikiliza kwa makini wakati nikiwasilisha hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, natanguliza shukurani zangu kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwa michango mtakayoitoa katika kuijadili na hatimae kuipitisha hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, Naomba kutoa hoja.

Kiambatanisho Nambari 1: Programu Kuu na Programu Ndogo kwa Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora

PROGRAMU	**PROGRAMU NDOGO**
Programu 101: Kuimarisha Shughuli za Mheshimiwa Rais na Mawasiliano	**Programu Ndogo 10101**: Uratibu wa Shughuli za Mheshimiwa Rais. **Programu Ndogo 10102**: Uimarishaji wa Mawasiliano baina ya Mheshimiwa Rais na Wananchi.
Programu 102: Kuimarisha Utawala Bora, Haki za Binaadamu na Usalama wa Watumishi wa Umma	**Programu Ndogo 10201**: Utawala Bora na Haki za Binaadamu. **Programu Ndogo 10202**: Usimamizi wa Usalama wa Watumishi wa Umma.
Programu103: Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora	

Kiambatanisho Nambari 2: Programu Kuu na Programu Ndogo kwa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi

PROGRAMU	**PROGRAMU NDOGO**
Programu 081: Usimamizi wa Majukumu ya Kikatiba na Kisheria ya Baraza la Mapinduzi	**Programu Ndogo 08101**: Utayarishaji wa Vikao vya kawaida na vya Dharura. **Programu Ndogo 08102**: Tathmini ya Utekelezaji wa Malengo ya Robo mwaka na Mwaka ya kila Wizara (Bango Kitita).

Programu 082: Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi	

Kiambatanisho Nambari 3: Programu Kuu na Programu Ndogo kwa Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje

PROGRAMU	**PROGRAMU NDOGO**
Programu 071: Kuwakilisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mikutano ya Kikanda na Kimataifa**.**	
Programu 072: Uratibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala ya ushirikiano wa Kimataifa na Diaspora	
Programu 073: Utawala na Uendeshaji wa Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nchi za Nje	

Kiambatanisho Nambari 4: Programu Kuu na Programu Ndogo kwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi

PROGRAMU	**PROGRAMU NDOGO**
Programu 501: Uchunguzi na Operesheni	
Programu 502: Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi	
Programu 503: Utawala na Uendeshaji wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi	

Kiambatanisho Nambari 5: Programu Kuu na Programu Ndogo kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

PROGRAMU	PROGRAMU NDOGO
Programu 111: Uthibiti wa Fedha za Umma	
Programu 112: Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali	

Kiambatanisho Nambari 6: Programu Kuu na Programu Ndogo kwa Tume ya Mipango

PROGRAMU	PROGRAMU NDOGO
Programu 491: Kusimamia Mipango ya Kitaifa	**Programundogo 49101**: Uratibu maendeleo ya kisekta, ufuatiliaji na tathmini na upunguzaji umaskini **Programundogo 49102**: Maendeleo ya Mipango ya Watendakazi na Idadi ya Watu
Programu 492: Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Sera za Kodi	
Programu 493: Utoaji waTakwimu	
Programu 494: Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Mipango	

Kiambatanisho Nambari 7: Wageni Waliofika na Kuonana na Mheshimiwa Rais Ikulu Zanzibar kwa Kipindi cha Julai - Machi 2013/2014

NAMBA	TAREHE	JINA
1.	10.07.2013	Mhe. Kang Chang Hee, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Korea Kusini
2.	13.07.2013	Bwana Mark Simonds, Waziri wa Uingereza anaeshughulikia masuala ya Afrika.
3.	16.07.2013	Mama Francisca Morandini, Mkuu wa *UNICEF*, Ofisi ya Zanzibar
4.	30.07.2013	Mhe. Pierluigi Velardi Balozi wa Italia Nchini Tanzania
5.	01 .08.2014	Dk. Elmi Duale, Balozi Maalum wa Umoja wa Mataifa nchini Somalia
6.	07.08.2014	Mhe. Saleh Suleiman Al- Harith, Balozi Mdogo wa Oman
7.	07.08.2014	Mheshimiwa Mutinda Mutiso, Balozi wa Jamhuri ya Kenya
8.	16.08.2013	Mheshimiwa Bibi Chen Qiman, Balozi Mdogo wa china
9.	20.08 .2013	Mhe. Jaap Frederiks, Balozi wa Uholanzi nchini Tanzania
10.	19.09.2013	Dr. Stergomona L. Tax. Katibu Mtendaji wa *SADC*
11.	25.09.2013	Ujumbe wa *IFAD* Mr. Perin Sain *Age – Regional Director East Africa and South African Division*(*ROME*) 1. Mr. Adolf Bizzi *Director Technical Division* (*ROME*) 2. Mr. Geofrey Livingstone *Economist* (*ROME*) 3. Mr. Fransisco Pichan, *Country Director* (Tanzania) 4. Ms. Merian Okongo, *Country Programme Manager* (Tanzania)
12.	30.09.2013	Mhe. Alfonso E. Lenhardt, aliyekuwa Balozi wa Marekani nchini Tanzania.
13.	30.09.2013	Mhe. Jaap Frederiks, Balozi wa Uholanzi nchini Tanzania.
14.	30.09.2013	Mhe. Xie Yunlian Balozi mdogo mpya wa China – Zanzibar.
15.	04.10.2013	Bibi Harriet Mathews, Mkuu wa Idara ya Afrika ya Mashariki na Magharibi kutoka Uingereza.
16.	10.10.2013	Prof. Steiner Krinsland. Mkuu wa Chuo cha Haukland nchini Norway.
17.	04.11.2013	Ndugu Mali Nilson, Mwakilishi mpya wa Save the Children pamoja na Ndugu Steve Thorne, Mkurugenzi Mkaazi mpya katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
18.	04.11.2013	Mheshimiwa Ingonn Klepsvik, Balozi wa Norway nchini Tanzania.
19.	08.11.2013	Mhe. Alexander A. Rannikh, Balozi wa Shirikisho la Urusi nchini Tanzania.
20.	08.11.2013	Mhe. Saleh Suleiman Al Harith Balozi mdogo wa Oman, Zanzibar.
21.	14.11.2013	Mhe. Ittiporn Boonpracong, Balozi wa Thailand nchini Tanzania.
22.	05.12.2013	Ujumbe wa Idara ya Afya ya Jimbo la Nanjing China.

NAMBA	TAREHE	JINA
23.	04.01.2014	Bwana H. Keck 'Engineer' kutoka Ujerumani aliyesimamia ujenzi wa nyumba za Maendeleo Kikwajuni.
24.	20.01.2014	Mhe. Luigi Scotto, Balozi wa Italy nchini Tanzania
25.	28.01.2014	Bwana Joe Ricketts wa "*Opportunity Education Foundation*", Mwakilishi na Mtendaji Mkuu wa Taasisi inayoshughulikia Fursa za Elimu yaMarekani.
26.	28.01.2014	Bwana Pawan Kumar, Balozi Mdogo wa India aliyepo Zanzibar
27.	28.01.2014	DK. Pierre Kahozi - Sangwa, Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani (*WHO*) hapa Zanzibar.
28.	13 .02.2014	Mhe. Marcel Escure, Balozi wa Ufaransa nchini Tanzania
29.	20.02.2014	Mhe. Bibi Lilianne Ploumen, Waziri wa Biashara za nje wa Uholanzi pamoja na Wawekezaji 50 kutoka Uholanzi
30.	21.02.2014	Ujumbe kutoka Kampuni ya Mahindra & Mahindra *LTD* kutoka India
31.	24.02.2014	Mhe. Dk. Azizi Ponary Mlima, Balozi wa Tanzania nchini Malaysia
32.	24.02.2014	Mhe. Bibi Flossie Asekanao Gomale –Chidyaonga Balozi wa Malawi Nchini Tanzania (Marehemu)
33.	24.02.2014	Mhe. Bi. Judith Kangoma Kapijimpanga, Balozi wa Zambia nchini Tanzania
34.	24.02.2014	Mhe. Soud Ali Mohamed, Balozi wa Oman nchini Tanzania
35.	27.02.2014	Mstahiki Osby Davis, Meya wa jiji la Vilejo Jimbo la Califonia Marekani pamoja na ujumbe wake
36.	31.03.2014	Mhe. Balozi Filiberto Ceriani Sebregondi, Kiongozi Mkuu wa Umoja wa Ulaya nchini Tanzania pamoja na Mabalozi wa nchi za Jumuiya ya Ulaya nchini Tanzania.
37.	31.03.2014	Mabalozi wa nchi za Jumuiya ya Ulaya nchini Tanzania
38.	15.05.2014	Kuonana na Ujumbe wa *IFAD* ukiongozwa na Bwana Pèrin Saint Ange, Mkurugenzi wa *IFAD* Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika.
39.	16.05.2014	Kuonana na Katibu Mkuu wa Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (*ICAO*) Bw. Raymond Benjamin.

Kiambatanisho Nambari 8: Orodha ya Sera na Sheria zilizojadiliwa na Baraza la Mapinduzi kwa kipindi cha Julai 2013 – Machi 2014

NAMBA	SHERIA/SERA ZILIZOJADILIWA
1	Mswada wa Sheria ya Makampuni
2	Mswada wa Sheria ya Kusimamia Mageuzi ya Mfumo wa Utoaji Leseni za Biashara
3	Mswada wa Mapendekezo ya Rasimu ya Sheria ya UKIMWI
4	Mswada wa Sheria ya Kuunda Baraza la Vijana la Zanzibar
5	Mswada wa Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Barabara Zanzibar
6	Mswada wa Kanuni za Sheria ya Utumishi wa Umma Nambari 2/2011
7	Mswada wa kufuta Sheria Nambari 9 ya Mwaka 1986 ya Wauguzi na Wakunga na Kuanzisha Sheria mpya ya Baraza la Wauguzi na Wakunga Zanzibar
8	Mswada wa Sheria ya Uanzishaji wa Shirika la Nyumba la Zanzibar
9	Mswada wa Sheria ya Maendeleo ya Karafuu Zanzibar
10	Mswada wa Sheria ya Hakimiliki ya Wagunduzi wa Mbegu za Mimea (*PBR*)
11	Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma
12	Rasimu ya Sera ya Hifadhi ya Jamii Zanzibar

Kiambatanisho Nambari 9: Wafanyakazi Waliopatiwa Udhamini wa Masomo ya Muda Mrefu na Mfupi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015

NAMBA	KIWANGO CHA ELIMU	FANI	IDADI YA WAFANYAKAZI
1	Shahada ya Uzamili	Mawasiliano na Habari, Sheria, Maendeleo ya Mipango,Takwimu, na Rasilimali watu, Biashara, Sayansi na Mipango.	27
2	Stashahada ya Uzamili	Utawala, Miradi na Kompyuta, Biashara	13
3	Shahada	Maendeleo ya Sera, Utatuzi wa Migogoro, Uongozi wa Biashara na Utaalamu wa Kompyuta.	17
5	Stashahada	Uongozi wa Utalii na Ukarimu, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Ukatibu muhtasi, Manunuzi, Ukatibu Muhtasi, Rasilimali Watu, Utunzaji Kumbukumbu, Chakula, Utawala na vinywaji.	17
6	Cheti	Utunzaji wa nyumba, Ukatibu muhtasi	7

NAMBA	KIWANGO CHA ELIMU	FANI	IDADI YA WAFANYAKAZI
7	Mafunzo ya Muda Mfupi	Ufuatiliaji na Tathmini, Manunuzi, Takwimu, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Uongozi, Sheria mpya za kazi na kanuni zake, Mbinu za Kupambana na Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Uandaaji wa Mipango, Utayarishaji wa Malengo na Elimu ya database ya utengenezaji wa taarifa za kitaalamu za fedha na uchambuzi pamoja na Umuhimu, Uandaaji na Uchambuzi wa Sera.	142
	Jumla		**223**

Kiambatanisho Nambari 10: Orodha ya Taasisi Ambazo Watumishi Wake Wamefanyiwa Upekuzi wa Kiusalama (*Security Vetting*) kwa Kipindi cha Julai - Machi 2013/2014

NAMBA	JINA LA TAASISI	IDADI YA WATUMISHI
1	Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora	35
2	Wizara ya Mifugo na Uvuvi	13
3	Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi	38
4	Wizara ya Fedha	76
5	Wizara ya Afya	443
6	Wizara ya Katiba na Sheria	30
7	Ofisi ya Baraza la Wawakilishi	15
8	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege	11
9	Wizara Ustawi wa Jamii, Uwezeshaji, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto	15
10	Shirika la Umeme (*ZECO*)	94
11	Benki ya Watu wa Zanzibar	25
12	Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi	46
13	Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma	2
14	Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ	5
15	Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (*ZSTC*)	24
16	Chuo cha Uandishi wa Habari	1
17	Shirika la Magazeti ya Serikali	12
18	Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (*ZSSF*)	5
	Jumla	**890**

Kiambatanisho Nambari 11: Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Mapendekezo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015

Idara	**Matumizi Yaliyoidhinishwa Mwaka 2013/2014**	**Fedha Zilizopatikana Hadi Machi 2014**	**Asilimia ya Fedha Zilizopatikana Hadi Machi 2014**	**Mapendekezo ya Bajeti ya Mwaka 2014/2015**
Ofisi ya Faragha	2,197.2	1,589.0	72.3	2,446.8
Ofisi ya Baraza la Mapinduzi	1,379.0	909.7	66.0	1,458.2
Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	522.4	262.9	50.3	428.3
Idara ya Mawasiliano - Ikulu	242.7	131.7	54.3	225.8
Idara ya Utumishi na Uendeshaji	1,274.6	764.7	60.0	1,131.8
Ofisi ya Usalama wa Serikali (*GSO*)	61.6	25.8	41.9	47.1
Ofisi ya Ofisa Mdhamini - Pemba	645.8	377.8	58.5	599.9
Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibar Wanaoishi Nchi za Nje	873.0	348.8	40.0	808.2
Idara ya Utawala Bora	216.5	143.5	66.3	227.7
Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi	810.0	353.9	43.7	815.4
Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali	1,911.0	1,549.3	81.1	2,023.0
Idara ya Mipango ya Kitaifa, maendeleo ya Sekta na Kupunguza Umasikini	688.2	504.0	73.2	441.4
Idara ya Ukuzaji Uchumi	426.7	337.5	79.1	463.7
Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi	149.1	195.1	130.9	243.8
Divisheni ya Uendeshaji na utumishi ya Tume ya Mipango				810.1
Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali	1,300.0	971.5	74.7	1,380.0
Jumla	**12,697.9**	**8,465.3**	**66.7**	**13,551.2**

Kiambatanisho Nambari 12: Matumizi ya Programu na Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa fedha 2013/2014 na Mapendekezo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015

Jina la Mradi/Programu	Matumizi Yaliyoidhinishwa Mwaka 2013/2014	Fedha Zilizopatikana Hadi Machi 2014	Asilimia ya Fedha Zilizopatikana Hadi Machi 2014	Mapendekezo ya Bajeti ya Mwaka 2014/2015
Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ikulu na nyumba za Serikali (*State Lodges*)	600.0	300.0	50.0	530
Mradi wa Kuimarisha Mawasiliano Ikulu	150.0	150.0	100.0	
Mradi wa Uimarishaji wa Juhudi za Kuzuia Rushwa Zanzibar	480.0	229.9	47.9	621
Kuratibu Utekelezaji wa *MCA-T*	50.0	15.5	31.1	
Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini yenye Kuleta Matokeo ya MKUZA II	750.0	264.8	35.3	768
Kujenga Uwezo wa Utekelezaji kwa Taasisi za Serikali	915.0	658.5	72.0	769
Kuratibu Utekelezaji wa MKURABITA	262.8	59.3	22.6	200
Mradi wa kuifanyia Mabadiliko na Kuimarisha Tume ya Mipango	60.0	31.7	52.8	150
Mradi wa Mashirikiano Baina ya Sekta za Umma na Sekta Binafsi	150.0	10.0	6.7	
Mradi wa Utafiti wa Hali ya Utumishi Nchini	150.0	91.0	60.6	61
Mradi wa Kuoanisha Masuala ya Idadi ya Watu, Afya ya Uzazi, Jinsia na Umasikini	140.0	38.5	27.5	100
Program ya Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Mama na Mtoto (*YCSPD*)	52.0	17.7	33.9	
Mradi wa Uimarishaji wa Takwimu	250.0	92.5	37.0	
Mradi wa Uimarishaji Takwimu Tanzania (*STATCAP*).	2,100.0	1,880.7	89.6	6,700
Kujenga Uwezo wa Kitengo cha Utafiti				100
Jumla	**6,109.8**	**3,840.1**	**62.9**	**10,001**

Kiambatanisho Nambari 13: Ahadi Zilizotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora Wakati wa Kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014

S/N	AHADI	UTEKELEZAJI	MAELEZO
1	Kuhakikisha majengo yote ya Ikulu na nyumba nyengine yanapatiwa Hati Miliki kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.	Jengo la Ikulu ya Mnazi Mmjoa tayari limeshapatiwa Hati Miliki	Hati Miliki za majengo mengine ziko katika hatua za utekelezaji
2	Kuhusu kuandaa Sera juu ya miongozo ya kurahisisha baadhi ya maeneo na kupunguza gharama zenye mianya ya fedha kwa Wazanzibari wanaoishi Nchi za Nje.	Mshauri Elekezi tayari amepatikana na anaendelea na kazi kwa mashirikiano ya Maofisa wa Idara	Hatua za awali za utayarishaji wa Sera hiyo zilihusisha ukusanyaji wa wadau mbali mbali Zanzibar na Tanzania Bara na hatua inayofuata ni kuonana na Wazanzibari ana kwa ana katika maeneo waliyopo nchi za nje
3	Ahadi ya kuandaa vipindi vya Rais kwa njia ya *Documentary* (kupitia studio ya Ofisi).	Matengenezo ya awali ya chumba kwa ajili ya studio yamefanyika	Matengenezo hayo yamehusisha uwekaji wa boriti mpya, kugonga na kutomea kuta pamoja na uwekaji wa linta katika sehemu za madirisha
4	Kufuatilia suala la ukuta Ikulu ya Mkokotoni.	Ujenzi wa ukuta na matengenezo ya Ikulu ya Mkokotoni yatafanyika baada ya kukamilika kwa mazungumzo na Idara ya Usalama wa Taifa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.	
5	Ahadi ya kuhakikisha kuwa elimu ya Uraia inatolewa kupitia Redio Jamii Micheweni badala ya ZBC Redio peke yake.	Elimu ya Uraia kwa kutumia Redio Jamii ya Micheweni itatolewa katika robo ya pili ya mwaka wa fedha wa 2013/2014.	
6	Ahadi ya kuwafanyia Semina Waheshimiwa Wawakilishi juu ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa kupitia Mradi wa miaka mitatu (3).	Semina kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi imepangwa kufanyika katika robo ya tatu	

S/N	AHADI	UTEKELEZAJI	MAELEZO
7	Suala la kushughulikia maslahi ya watumishi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ili kuwawezesha watendaji wa Taasisi hiyo kufanya majukumu yao kwa uhakika na kujiamini zaidi.	Mbali na mshahara, Serikali inawapatia posho maalum la mazingira magumu watendaji wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi.	Serikali inaendelea kufanya mapitio ya mishahara na maslahi kwa wafanyakazi wake

Kiambatanisho Nambari 14: Utekelezaji wa Maagizo Yaliyotolewa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Wakati wa Kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014

S/N	AGIZO	UTEKELEZAJI	MAELEZO
1	Tuwatumie Wazanzibari walioko Nchi za nje ili kutusaidia kutuunganisha na Wawekezaji, Wahisani na Mashirika mbali mbali ili kusogeza maendeleo ya Nchi yetu	Idara imeendelea na mchakato huo kwa kufanya mazungumzo na Jumuiya za Wazanzibari waliopo Canada, Marekani na *UK*	Wazanzibari waliopo katika maeneo hayo wanaendelea na juhudi za kutafuta wawekezaji na misaada kwa ajili ya Zanzibar
2	Kutafuta jengo au Ofisi ambayo itakuwa nje ya jengo la Ikulu ili kurahisisha Diaspora kupata fursa ya kuitembelea Ofisi yao kiurahisi zaidi	Ushauri huu unafanyiwa kazi	
3	Kuratibu kikamilifu shughuli za Wazanzibari wanaoishi nje ya Nchi	Uratibu unafanywa kwa mujibu wa mpango kazi wa Idara na ni endelevu	
4	Uingizwaji wa fedha za Ofisi ya Usalama wa Serikali hauridhishi	Juhudi za makusudi zimeanza kufanyika ambapo kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Ofisi hii imepangiwa bajeti ya TZS. 61.6 milioni kutoka TZS. 54.9 milioni za mwaka 2012/2013 sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 12.2	
5	Kuharakisha upatikanaji wa Hati miliki ya Majengo ya Ikulu pamoja na yale ya Serikali	Jengo la Ikulu ya Mnazi Mmjoa tayari limeshapatiwa Hati miliki	Hati miliki za majengo mengine ziko katika hatua za utekelezaji

S/N	AGIZO	UTEKELEZAJI	MAELEZO
6	Matengenezo madogo na makubwa ya Idara ya Utumishi na Uendeshaji yawekwe pamoja na sio yatenganishwe	Matengenezo hufanywa kwa mujibu wa mahitaji na vifungu husika	
7	Kumualika Mheshimiwa Mbarouk Wadi Mussa kuja kuliona jengo la *ZIPA*	Ofisi imefanya mawasiliano na Mheshimiwa Mbarouk Wadi Mussa kwa barua yenye kumbukumbu namba AR/IKL/B.90/5.VOL.IV/78 iliaweze kuja kuliona jengo hilo	Mawasiliano ya simu pia yalifanyika ambapo Mheshimiwa Mbarouk ameahidi tuwasiliane nae wakati Vikao vya kawaida vya Baraza la Wawakilishi vitakapokuwa vinaendelea
8	Ukarabati wa jengo la Ikulu ya Kibweni	Ofisi tayari imewasilisha waraka Serikalini (Baraza la Mapinduzi) ili kuomba kuwa na mradi maalum wa matengenezo ya majengo yote ya urithi ambayo ni *gazzetted*.	
9	Kufanyiwa ukarabati wa hali ya juu Ikulu ya Mkoani	Ikulu ya Mkoani tayari imeshafanyiwa matengenezo makubwa yaliyojumuisha jengo litakalotumiwa na walinzi ambapo kwa sasa Ikulu hiyo ipo katika hali ya kuridhisha. Hivi sasa matengenezo yanayoendelea ni ya ukamilishaji wa nyumba ndogo ya askari Polisi pamoja na ukuta unaoizunguka Ikulu hiyo.	
10	Kuandaa vipindi maalum "*Documentaries*" ambazo zitaonesha kazi za Mheshimiwa Rais alizozifanya katika sekta mbali mbali na baadae zioneshwe katika Shirika la Utangazaji Zanzibar	Vipindi 7 vya *TV* na 12 vya Redio vimeandaliwa na kurushwa hewani na *ZBC*. Vipindi vya *TV* pia vimeoneshwa kwa njia ya Sinema katika vijiji 15 vya Unguja.	Kupitia vipindi hivyo, wananchi wamekuwa wakipata taarifa ya shughuli ambazo Mheshimiwa Rais amekuwa akizitekeleza siku hadi siku

Kiambatanisho Nambari 15: Utekelezaji wa Malengo kwa Miezi Tisa (Julai – Machi 2013/2014)

1. OFISI YA FARAGHA KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2013/2014

MALENGO YA MWAKA 2013/2014	UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KWA MIEZI TISA
1. Kuimarisha huduma za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi	i. Jumla ya maagizo 23 ya Mheshimiwa Rais yamefuatiliwa katika Mikoa mitano Unguja na Pemba
	ii. Ziara mbili za nje za Mheshimiwa Rais nchini Uholanzi na India zimeratibiwa
	iii. Kwa upande wa Unguja maeneo yaliyokaguliwa ni Marumbi, Michamvi, Mangapwani, Tunguu, Kidoti Bondeni, Mazizini, Amani, Hoteli ya Bwawani, Kiembesamaki, Kisonge, Kibandamaiti, Tunguu, Beit el Ras, Kajengwa na Michenzani. Aidha, kwa upande wa Pemba ni Kangagani, Likoni, Bahanasa Gombani, Ukunjwi na Utaani.
	iv. Ufuatiliaji na tathmini kwa wananchi wenye matatizo katika maeneo ya Bumbwini, Pangatupu, Kidoti, Chaani, Muwange, Jang'ombe, Tomondo, Shingwi, na Pitanazako umefanyika.
	v. Wageni wa Mheshimiwa Rais waliofika Ikulu wamepatiwa huduma ipasavyo
	vi. Wageni wa Wasaidizi wa Mheshimiwa Rais wamepatiwa viburudishaji
	vii. Wageni wa Mheshimiwa Rais wamepatiwa zawadi zikiwemo makasha, milango, viungo, jahazi na vitabu vya Zanzibar.
	viii. Malipo ya posho la kujikimu kwa Wasaidizi wawili wa Mheshimiwa Rais waliokwenda DSM na wawili waliokwenda Pemba kikazi yamefanyika. Aidha, malipo ya posho maalum kwa Wasaidizi wawili wa Mheshimiwa Rais waliokwenda masomoni nchini China nayo yamefanyika.
	ix. Nakala 800 za Hotuba ya Eid El Fitri, nakala 2,000 za hotuba ya miaka 50 ya Mapinduzi Zanzibar na kadi 500 za mialiko zimechapishwa. Aidha, nakala 300 za taarifa ya Mheshimiwa Rais kwa waandishi wa habari pamoja na nakala 1,000 za utengenezaji wa madaftari ya kunakili muhutasari zimechapishwa.
	x. Huduma katika Ikulu ndogo ya Laibon zimeimarishwa kwa kufanya malipo ya huduma ya DSTV, umeme, maji pamoja na ununuzi wa vifaa vya usafi.
	xi. Huduma za Dodoma zimeimarishwa kwa kupatiwa vifaa na huduma muhimu za umeme, maji, ununuzi wa vifaa vya usafi na bustani yamefanyika. Aidha, matengenezo makubwa ya vyoo vitano na sehemu ya kufulia yamefanyika.
	xii. Huduma za Ikulu Ndogo ya Migombani zimeimarishwa kwa kupatiwa huduma muhimu.
2. Kuimarisha mazingira ya kazi	i. Mazingira ya kazi yameimarishwa kwa ofisi kupatiwa vifaa muhimu vya kazi ikiwa ni pamoja na vifaa vya mawasiliano, vifaa vya kuandikia, matengenezo na ununuzi wa vyombo vya usafiri yamefanyika, huduma za umeme zimeimarishwa.
3. Kuendeleza matengenezo madogo madogo ya Ikulu Zanzibar	i. Upakaji rangi ukuta na baadhi ya sehemu ya jengo la Ikulu Kuu ya Mnazimmoja na matengenezo ya mlango wa Ofisi ya *PSU* yamefanyika.

MALENGO YA MWAKA 2013/2014	UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KWA MIEZI TISA
4. Kujenga uwezo kwa wafanyakazi 6 (Cheti 3 na 3 Diploma)	i. Wafanyakazi wawili waliomaliza Stashahada ya Uongozi wa Utalii na Ukarimu na wawili wanaoendelea katika ngazi ya Stashahada na Cheti katika Chuo cha Utalii Maruhubi wamelipiwa ada zao.
5. Kuongeza ufanisi wa kazi na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao	i. Wafanyakazi wamelipwa mishahara yao kwa wakati
	ii. Gharama za Mfuko wa (*ZSSF*) zimelipwa kwa wakati
	iii. Wafanyakazi 21 wamelipwa fedha za likizo

2. OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2013/2014

MALENGO YA MWAKA 2013/2014	UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KWA MIEZI TISA
1. Kuhakikisha kuwa Baraza la Mapinduzi na kamati ya Makatibu Wakuu vinatekeleza ipasavyo majukumu yao ya Kikatiba na Kisheria.	i. Vikao 18 vya kawaida vya BLM na 32 vya Makatibu Wakuu vimeandaliwa.
	ii. Jumla ya vikao viwili vya dharura vya BLM na vitatu vya Kamati ya Makatibu Wakuu vimeandaliwa.
	iii. Kikao kimoja cha Kamati ya Fedha na Uchumi ya Baraza la Mapinduzi kimeandaliwa.
	iv. Mkutano mmoja (Bango Kitita) wenye vikao 17 umeandaliwa.
2. Kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi kwa Wajumbe wa BLM na wafanyakazi wake.	i. Matengenezo Jengo la "People Palace" katika sehemu ya koridoo ya chini pamoja na vyumba vya chini yamekamilika.
	ii. Ofisi imenunua kompyuta mpya 4 kwa ajili ya kuendeshea shughuli za Kiofisi
	iii. Waheshimiwa Mawaziri wasio na Wizara Maalum, Katibu, Naibu Katibu na watendaji wengine wamewezeshwa kufuatilia shughuli mbalimbali za Ofisi ndani na nje ya nchi.
	iv. Ofisi imepatiwa huduma hizo kwa kulipia gharama za simu na mtandao (*Internet*).
	v. Ofisi imenunua jumla ya lita 5,200 za mafuta pamoja na kulipia huduma za vilainisho kwa ajili ya matumizi ya gari za Ofisi.
	vi. Ofisi imepatiwa vifaa vya kuandikia pamoja na kulipia huduma za maji, umeme, vifaa vya usafi, magazeti na machapisho mbalimbali ya kazi za Ofisi.
	vii. Ofisi imefanya matengenezo ya gari na mashine za fotokopi.
3. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wake kupitia mafunzo mbalimbali, kuhifadhi nyaraka muhimu za Baraza na kusaidia shughuli za kijamii.	i. Wafanyakazi 5 wamelipiwa gharama za masomo ya muda mrefu na wafanyakazi wawili wamelipiwa mafunzo ya muda mfupi.
	ii. Ofisi imelipa gharama za kusaidia shughuli mbalimbali za kijamii kwa Waheshimiwa Mawaziri watatu wasio na Wizara Maalum.
	iii. Wafanyakazi wamepatiwa taaluma ya kujikinga na maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI.

MALENGO YA MWAKA 2013/2014	UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KWA MIEZI TISA
	iv. Ofisi imetengeneza nakala 12 za vitabu vya kumbukumbu za Baraza la Mapinduzi na kuvihifadhi kwa njia ya elektroniki pamoja na kutia kava nakala 36 za vitabu vilivyotengenezwa awali.
4. Kuhakikisha kuwa Wafanyakazi wanawajibika ipasavyo kwa umakini, ari, nidhamu na moyo wa kujituma.	i. Ofisi imelipa mishahara kwa wafanyakazi wake wote kwa wakati.
	ii. Ofisi imelipa gharama za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa wafanyakazi wanaostahiki kwa wakati.
	iii. Jumla ya wafanyakazi 15 wamepatiwa sare.
	iv. Wastaafu wawili wa Baraza la Mapinduzi wamezawadiwa jumla ya mabati 75 ya kuezekea kila mmoja.
	v. Ofisi imesaidia kulipa gharama za mazishi kwa mfanyakazi mmoja.
	vi. Ofisi imelipa fedha za likizo kwa Mheshimiwa Waziri asiekuwa na Wizara Maalum na wafanyakazi watatu.

3. IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2013/2014

MALENGO YA MWAKA 2013/2014	UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KWA MIEZI TISA
1. Kuimarisha uwezo wa Idara katika kupanga, kuandaa na kuchambua Sera, kuandaa na kufanya tafiti pamoja na kuratibu shughuli za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi	i. Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi umefanyiwa mapitio.
	ii. Mikutano mitatu ya robo mwaka kwa watendaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imefanyika.
	iii. Idara imefanya mkutano wa siku 2 uliowajumuisha Wakuu wa Idara na Maofisa wa kufanya mapitio ya *MTEF* wa mwaka 2014/2015.
	iv. Taarifa za utekelezaji wa malengo ya bajeti ya mwaka 2013/2014 kwa robo mwaka ya kwanza, ya pili na ya tatu zimeandaliwa na kuwasilishwa kunakohusika. Aidha, taarifa ya utekelezaji wa malengo ya bajeti kwa mwaka 2012/2013 nayo ilitayarishwa.
	v. Mikutano ya kila mwezi kwa Maofisa mipango ya kutathmini utekelezaji wa malengo ya bajeti imefanyika.
	vi. Maandalizi ya Sherehe za Miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar zimeratibiwa ipasavyo pamoja na kuandaa, kuchapisha na kusambaza nakala 800 za kitabu maalum cha Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kinachoitwa "Taarifa ya Miaka 50 ya Maadhimisho ya Sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar", kalenda za ukutani nakala 6,000, kalenda za mezani nakala 4,000, Toleo Maalum la Jarida la miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar nakala 4,000 kalamu 4,000, mikoba 4,000, fulana pamoja na kofia zake 200, seti 1 ya televisheni na vipeperushi vya aina mbili 8,000.
	vii. Idara imefanya warsha ya wafanyakazi 28 juu ya kujadili na kuandaa vipaumbele vya maeneo ya kufanyia utafiti kwa kuwahusisha Wakuu wa Idara pamoja na Maofisa mbalimbali kutoka kwenye Idara ziliopo chini ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

MALENGO YA MWAKA 2013/2014	UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KWA MIEZI TISA
	viii. Taarifa zimeshakusanywa kupitia madodoso pamoja na kuingizwa kwenye database na zinafanyiwa uchambuzi.
2. Kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini	i. Ufuatiliaji na Tathmini kwa Taasisi zilioko Pemba tayari umefanyika.
3. Kuimarisha uwezo wa watendaji wa Idara	i. Wafanyakazi watano wanaendelea na masomo yao katika ngazi ya Shahada ya Pili, Shahada ya Kwanza na Stashahada wamelipiwa gharama za masomo.
	ii. Wafanyakazi watano wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi katika fani za Uandaaji na Usimamizi wa Bajeti pamoja na usimamizi na uendeshaji wa Tovuti (*Website Management*).
	iii. Maofisa 25 kutoka Ofisi na Idara za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wamepatiwa mafunzo ya siku 4 juu ya matumizi ya Programu ya "*Excel*".
4. Kuimarisha huduma za Mawasiliano ya Habari (TEKNOHAMA)	i. Ofisi tayari imenunua anti-virus huku ikisubiri kukamilika uungaji wa Mkonga wa Taifa ili kukamilisha Mfumo wa ulinzi wa Mtandao (*Network Security System*) wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
	ii. Rasimu ya awali ya Muongozo wa matumizi ya *TEKNOHAMA* imekamilika.
	iii. Mtandao wa Mawasiliano wa ndani umefanyiwa matengenezo pamoja na ununuzi wa jumla ya vifaa 33 vikiwemo Kompyuta 8, *Projector 3, Server 3, Juniper Switch* 3, Fotokopi kubwa, *Moving* Camera, Still Camera, Switch mbalimbali na waya uliotumika kuweka mtandao mpya wa Internet.
5. Kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi kwa kununua vitendea kazi vya kisasa vya Ofisini na Samani ili kutoa huduma bora	i. Vifaa kwa matumizi ya Ofisi vimenunuliwa na matengenezo yake yamefanyika vikiwemo fotokopi, projekta, wino, modemu, vifaa vya usafi, vifaa vya kuandikia pamoja na malipo ya magazeti yamefanyika. Aidha, Gari la Idara limefanyiwa matengenezo.
6. Kuongeza ufanisi kazini ikiwemo kuwapatia watendaji stahiki zao.	i. Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi yamelipwa kwa wakati
	ii. Malipo ya *ZSSF* kwa wafanyakazi yamelipwa kwa wakati

4. IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2013/2014

MALENGO YA MWAKA 2013/2014	UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KWA MIEZI TISA
1. Kuongeza ufanisi wa kazi kwa kuimarisha mazingira ya utendaji kazi na maslahi ya wafanyakazi	i. Idara imelipa Mishahara, posho maalum na kuwasilisha michango *ZSSF* kwa wakati
	ii. Ununuzi wa Vespa 2, Compyuta 6 pamoja na zana na spea umefanyika
	iii. Matengenezo makubwa ya jengo lililokua likitumiwa na *ZIPA* yamefanyika, uwekaji wa madirisha ya aluminium na mbao kwenye ngazi katika jengo la Utawala Ikulu, matengenezo ya stoo ya kuwekea majalada na matengenezo madogo ya gari 11, vipoza hewa vitatu, vifaa vya kuzimia moto, samani za Ofisi (meza 7 na viti 7) na simu 2 za mezani vimenunuliwa.
	iv. Huduma mbalimbali zimetolewa zikiwemo malipo ya simu, ununuzi wa mafuta, umeme, vifaa vya kuandikia, magazeti, viburudishaji na vifaa vya usafi.
	v. Stahiki mbalimbali zimetolewa zikiwemo malipo ya likizo kwa wafanyakazi 11, posho la kujikimu kwa safari za kikazi Pemba, Dar-es-salaam na Dodoma wakiwemo Viongozi watano na Maofisa 13 na malipo baada ya saa za kazi kwa wafanyakazi 10.
2. Kutekeleza Sheria ya Fedha na Sheria ya Manunuzi kwa kufanya ukaguzi wa ndani, kuendesha vikao 12 vya Bodi ya Zabuni na vikao 4 vya kamati ya Ukaguzi wa Ndani.	i. Vikao 9 vya Bodi ya Zabuni vimefanyika
	ii. Mpango wa Manunuzi wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wa mwaka 2013/2014 umeandaliwa
	iii. Vikao vinne vya Kamati ya Ukaguzi wa ndani vimefanyika
	iv. Mipango yote ya ukaguzi imetayarishwa ambayo ndio muongozo wa kitengo cha ukaguzi wa ndani wanaofuata katika kufanya kazi za ukaguzi
	v. Hesabu za mwisho wa mwaka zimepitiwa na kugundulika kuwa taratibu na sheria za fedha zimefuatwa kama zinavyoelekeza
	vi. Kazi ya kufanya ukaguzi wa ndani kwa ORMBLM ilifanyika na kutoa ushauri kwa uongozi juu ya kasoro zilizojitokeza
	vii. Kazi ya kufanya uhakiki ilifanyika na kutolewa ushauri kwa kasoro zilizogundulika
	viii. Kazi ya kupitia mikataba, kuangalia thamani, viwango na ubora wa huduma na bidhaa zilizonunuliwa imefanyika
	ix. Hoja zote za ukaguzi zilizojitokeza zimefanyiwa kazi na tayari zimeshajibiwa
3. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya nchi.	i. Wafanyakazi 7 wamesomeshwa wawili katika ngazi ya shahada ya uzamili, wawili ngazi ya stashahada, mmoja cheti na mmoja masomo ya muda mfupi nchini India na Dar es Salaam
	ii. Mafunzo ya matayarisho ya kazi kwa waajiriwa wapya 10 yamefanyika
4. Kua na mpango wa makisio ya mishahara na mpango wa matumizi ya Rasilimali watu	i. Makisio ya mishahara na mipango ya matumizi ya Rasilimali Watu yamefanyika na kuwasilishwa Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma.
5. Kusimamia utendaji na uwajibikaji wa Wafanyakazi	i. Mkutano mmoja wa Kamati ya Uongozi na Vikao vitano vya Kamati Tendaji vimefanyika

5. IDARA YA MAWASILIANO - IKULU KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2013/2014

MALENGO YA MWAKA 2013/2014	UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KWA MIEZI TISA
1. Kulinda na kuendeleza taswira ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi	i. Vipindi 31 vya Televisheni na 13 vya redio vimeandaliwa na kurushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji la *ZBC* na sinema za maonesho vijijini zimefanyika.
	ii. Mahusiano yameimarika. Idara imeendelea kuwashirikisha Wadau mbalimbali wa nje ya Ofisi katika kufanikisha majukumu ya Ofisi
	iii. Kalenda za Ikulu nakala 4,000 zimechapishwa na kusambazwa katika Taasisi zote za Serikali na Taasisi binafsi.
	iv. Jarida la Ikulu Toleo Namba 011, 012, 013 limechapishwa na kusambazwa katika Taasisi zote za Serikali na Binafsi Unguja na Pemba.
2. Kuimarisha mazingira ya kazi katika Idara ili iweze kutoa huduma nzuri	i. Vifaa vya Ofisi vimepatikana kwa wakati vikiwemo vifaa vya kuandikia, petrol pamoja na vifaa vya kompyuta.
3. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Idara ya Mawasiliano	i. Wafanyakazi wawili wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika utaalamu wa kompyuta katika chuo cha Bagamoyo na Mawasiliano ya Habari katika chuo cha *Sreekantha First Grade Collage*, Mysore India.
4. Kuimarisha ufanisi kazini kwa kuwapatia wafanyakazi stahiki zao	i. Mishahara imelipwa kwa wakati
	ii. Gharama za *ZSSF* zimelipwa kwa wakati

6. OFISI YA USALAMA WA SERIKALI (*GSO*) KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2013/2014

MALENGO YA MWAKA 2013/2014	UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KWA MIEZI TISA
1. Kuimarisha shughuli za upekuzi kwa watumishi kabla na baada ya kuajiriwa.	i. Ofisi ya Usalama wa Serikali (*GSO*) imepokea maombi (932) kutoka Taasisi na Wizara mbalimbali za Serikali. Maombi hayo yameshafanyiwa kazi na ushauri umeshapelekwa katika Taasisi na Wizara husika.
2. Kuimarisha ukaguzi wa majengo, miundombinu na mali za Serikali	ii. *GSO* imefanya ukaguzi katika Wizara/Taasisi zifuatazo: Tume ya Uchaguzi Zanzibar (*ZEC*), Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (*ZAECA*), Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Visima vya maji Bumbwini Kidanzini na Makoba, Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*), Tume ya Kurekebisha Sheria, Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa Mchangamdogo Pemba, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano Zanzibar.
3. Kuwajengea uwezo watumishi juu ya utunzaji na udhibiti wa siri za Serikali	i. Mafunzo ya utunzaji na udhibiti wa siri za Serikali kwa watumishi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi, wanafunzi wa Chuo cha Utumishi wa Umma (*IPA*) na watumishi wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (*ZEC*) yamefanyika.
4. Kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi	i. Vitendea kazi (*Stationeries*) pamoja na huduma za usafiri ikiwemo *Petrol* vimenunuliwa.

7. IDARA YA UTAWALA BORA KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2013/2014

MALENGO YA MWAKA 2013/2014	UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KWA MIEZI TISA
1. Kuweka mifumo ya kuinua uelewa wa wananchi juu ya Misingi ya Utawala Bora katika ngazi zote	i. Mpango wa mafunzo kwa ajili ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa na Utawala Bora umetayarishwa.
	ii. Elimu juu ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa imetolewa kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Maofisa Wadhamini, Maofisa Tawala wa Mikoa na Wilaya pamoja na Wawakilishi wa Jumuia za Kiraia
	iii Kamati moja ya Shehia ya Donge Mnyimbi imepatiwa mafunzo juu ya Haki za Binadamu
2. Kuandaa viashiria vya Utawala Bora vya kitaifa na kuratibu uandaaji wa viashiria vya Utawala Bora kisekta	i. Viashiria vya kitaifa vya Utawala Bora vimekamalika.
	ii. Mikutano mitatu ya namna ya kuandaa viashiria vya Utawala Bora imefanyika kwa Maofisa viungo (*Focal Person*) wa Utawala Bora
3. Kuandaa na kusambaza ripoti ya Utawala Bora	i. Idara imeanza matayarisho ya kufanya Utafiti mdogo wa Utawala Bora kwa kuandaa muongozo juu ya namna utafiti huo utakavyofanywa
4. Kutoa elimu ya uraia juu ya Haki za Binaadamu	i. Programu ya elimu ya uraia imeandaliwa
	ii. Jumla ya vipindi 24 vimerushwa hewani na Shirika la Utangazaji Zanzibar kwa njia ya redio na vipindi viwili vimerushwa hewani kupitia redio Coconut na Chuchu *FM*. Aidha, jumla ya shehia 15 zimepatiwa elimu ya uraia juu ya misingi ya Utawala Bora na Haki za Binaadamu.
	iii. Matangazo mafupi ya Utawala Bora yamerushwa hewani na Shirika la Utangazaji Zanzibar.
	iv. Elimu ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora imetolewa kwa Waandishi wa Habari na Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu.
	v. Idara imefanya ziara ya kikazi huko Pemba.
5. Kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi	i. Idara imenunua vifaa mbalimbali vikiwemo *fotokopi* 1, *printa* 1, *laptop* 1, *Antivirus* 2, *extension* 1, *modem* 3, *wireless mouse* 1 na *USB HAB* 1.
	ii. Idara imenunua mafuta ya uendeshaji wa shughuli za Ofisi.
	iii. Wafanyakazi watatu wamelipiwa ada za masomo.
6. Kuwapatia wafanyakazi stahiki zao	i. Wafanyakazi wamelipwa mishahara na stahiki zao.
	Michango ya *ZSSF* imewasilishwa kwa wakati.

8. OFISI YA OFISA MDHAMINI – PEMBA KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2013/2014

MALENGO YA MWAKA 2013/2014	UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KWA MIEZI TISA
1. Kuwajengea uwezo wafanyakazi 6 katika mafunzo ya muda mfupi na mrefu	i. Wafanyakazi 6 wamelipiwa gharama za mafunzo, mmoja katika ngazi ya cheti, 4 katika ngazi ya Stashahada na mmoja katika ngazi ya Shahada ya Uzamili
	ii. Jumla ya wafanyakazi 35 wamepatiwa mafunzo juu ya sheria mpya za kazi na kanuni zake
2. Kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi	i. Ofisi imeratibu ziara za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kisiwani Pemba, pia imeweza kuratibu na kufuatilia shughuli nyengine za Wizara kwa ufanisi
	ii. Malipo ya umeme, maji vifaa vya kuandikia, vifaa vya kompyuta na matengenezo ya magari, pamoja na bima yamelipwa.
	iii. Mawasiliano ya simu, mtandao, magazeti na huduma za posta yamepatikana kwa wakati
	iv. Maofisa sita wameshiriki katika mikutano na vikao mbali mbali Unguja, pia mfanyakazi 1 amelipwa likizo na wafanyakazi wanne wamelipiwa malipo ya saa za ziada
	v. Mikutano minne ya Kamati ya Maofisa wadhamini imefanyika.
	vi. Matengenezo ya miundombinu ya maji machafu na usafishaji wa mashimo ya maji machafu kwa Ikulu ya Chake umefanyika.
	vii. Huduma za umeme, maji, vifaa vya usafi na mafuta ya jenereta yamepatikana kwa wakati. Aidha, uwekaji wa taa eneo la Ikulu Chake na ukataji miti Ikulu ya Mkoani umefanyika
3. Kuimarisha utoaji wa huduma bora na kukuza amani na utulivu	i. Mpango wa mafunzo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa umetayarishwa.
	ii. Mafunzo ya siku moja yametolewa juu ya Utawala Bora na Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa Maofisa wadhamini, Maofisa Tawala wa Mikoa na Wilaya na Asasi za Kiraia Pemba.
	iii. Mafunzo kwa kamati nne za Shehia ya Ng'ambwa, Mkoroshoni, Piki na Mzambarauni juu ya athari za uvunjwaji wa Haki za Binaadamu yametolewa.
	iv. Mpango wa elimu ya uraia umetayarishwa.
	v. Elimu ya uraia imetolewa kwa Shehia za Wilaya ya Mkoani na Wilaya ya Wete.
	vi. Vipindi 6 vya elimu ya uraia vimetayarishwa na kurushwa kupitia Redio jamii Micheweni.
4. Kuimarisha ukondoeshaji wa masuala mtambuka ikiwemo UKIMWI, Jinsia na Mazingira	i. Mkutano wa kuhamasisha wafanyakazi kupima afya zao umefanyika
	ii. Mkutano mmoja juu ya umuhimu wa jinsia umefanyika kwa wafanyakazi
5. Kuimarisha ufanisi kazini kwa kuwapatia wafanyakazi stahiki zao	i. Mishahara kwa wafanyakazi 53 imelipwa kwa wakati
	ii. Michango ya asilimia 10 ya *ZSSF* kwa wafanyakazi imelipwa kwa wakati

9. IDARA YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA NA URATIBU WA WAZANZIBARI WANAOISHI NJE KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2013/2014

MALENGO YA MWAKA 2013/2014	UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KWA MIEZI TISA
1. Kuhakikisha kuwa Zanzibar inashiriki katika mikutano ya majadiliano ya kikanda	i. Idara imewawezesha Wataalamu 15 kushiriki katika Mikutano ya mashauriano ya kikanda *(country consultative meeting*) Dar-es -salaam.
	ii. Idara imewawezesha Wataalamu 23 kushiriki katika Mikutano ya Kikanda ndani ya nchi Arusha, Dar-es-salaam na Zanzibar.
	iii. Idara imewawezesha wataalamu 12 kushiriki katika mikutano ya kikanda Malawi, Rwanda, Australia, Uganda, Sri Lanka na Burundi.
	iv. Idara imeendelea na utaratibu wa kuelimisha jamii kupitia vyombo vya Habari (*ZBC* Redio) juu ya umuhimu wa soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki.
02. Kuandaa mazingira bora yatakayowawezesha Wazanzibari wanaoishi nchi za nje kuweza kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya Zanzibar.	i. Idara imekutana na Wazanzibari wanaoishi nchini Oman, Uingereza na Denmark kwa lengo la kukusanya taarifa muhimu katika mchakato wa uundaaji wa sera ya Diaspora Zanzibar pamoja na kuwahamasisha kuwekeza na kuchangia maendeleo ya nchi yao.
	ii. Idara imemuwezesha mtaalamu mmoja kushiriki katika mkutano uliyotayarishwa na Idara ya Diaspora katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Dar-es-salaam.
	iii. Idara imekutana na kufanya mazungumzo na wadau wa Diaspora Unguja na Pemba.
	iv. Vipindi vya kuitangaza dhana ya Diaspora vimetayarishwa na kurushwa na Shirika la Utangazaji (*ZBC*).
	v. Vijarida mbalimbali vinavyohusiana na mambo ya Diaspora na Ushirikiano wa Kikanda vimechapishwa
	vi. Ofisi kwa kushirikiana na mshauri elekezi mzalendo tayari imekusanya taarifa muhimu kutoka kwa wadau ndani na nje ya nchi na tayari imeshakamilisha Rasimu ya awali ya Sera ya Diaspora ya Zanzibar.
	vii Mkutano mmoja uliowashirikisha wadau muhimu wa Diaspora wakiwemo Sekta binafsi na Asasi za kiraia umefanyika.
03. Kuongeza ufanisi pamoja na kuwaongezea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu	i. Malipo ya ada kwa mfanyakazi mmoja yamefanyika
	ii. Idara imefanya mazungumzo na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara Dar-es-salaam kuhusu mbinu za majadiliano ili kuwajengea uwezo wataalamu wa Idara na kukubaliana kwamba mafunzo hayo yafanyike katika mwezi wa Mei.
04. Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi katika Idara pamoja na kufanikisha maadhimisho ya Sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar	i. Malipo ya ununuzi wa vifaaa vya kutendea kazi pamoja na malipo ya huduma yamefanyika ikiwemo malipo ya mafuta, ununuzi wa vifaa vya gari, vifaa vya kompyuta, vifaa vya kuandikia, umeme, vifaa vya usafi na Magazeti
	ii. Idara imechapisha vipeperushi 2,500 ambavyo vimeonesha shughuli zinazotekelezwa na Diaspora katika ushirikiano wa Kikanda, Kimataifa na Diaspora ambavyo vilitolewa kwa wananchi.
5.Kuendeleza na kuimarisha juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kukuza uhusiano mwema na nchi marafiki na Taasisi za Kimataifa	i. Idara imeratibu ziara za ujumbe kutoka California – Marekani, Thailand na India ambapo makubaliano ya awali ya mashirikiano katika nyanja mbalimbali yalifikiwa.
6. Kuimarisha ufanisi kazini kwa kuwapatia wafanyakazi stahiki zao	i. Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi yamelipwa kwa wakati
	ii. Malipo ya michango ya mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) kwa wafanyakazi imelipwa kwa

MALENGO YA MWAKA 2013/2014	UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KWA MIEZI TISA
	wakati
	iii. Jumla ya wafanyakazi 6 wamepatiwa malipo ya likizo

10. MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2013/2014

MALENGO YA MWAKA 2013/2014	UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KWA MIEZI TISA
1. Kuweka Mfumo mzuri wa uendeshaji wa Mamlaka ya Rushwa na Uhujumu Uchumi	i. Shughuli ya kusarifu programu ya kujenga uelewa kwa wananchi imefanyika.
	ii. Jumla ya vipindi 48 vimetayarishwa na kurushwa hewani.
	iii. Elimu ya kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi imetolewa kwa shehia 15 za Unguja na Shehia 6 – Pemba pamoja na skuli za Ben bella, Lumumba, Mkwajuni, Kwerekwe C, Dunga, Fujoni, Tumekuja, Fumba na Makunduchi zilifaidika na elimu hiyo.
	iv. Vipeperushi vyenye ujumbe wa mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu wa uchumi viliandaliwa na kusambazwa.
	v. Mamlaka ilishiriki kikamilifu katika maonesho ya sherehe za Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar
2. Kuijengea uwezo Mamlaka ya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi	i. Mafunzo ya awali ya uchunguzi kwa watumishi wapya 28 na mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo watumishi yamefanyika.
	ii. Ununuzi wa vifaa vya kuandikia, usafi, mafuta, umeme na vipoza hewa umefanyika.
	iii. Ununuzi wa vifaa vya kiuchunguzi umefanyika.
	iv. Muundo wa Mamlaka na wa utumishi imeshatayarishwa na kuwasilishwa katika Taasisi husika kwa kufanyiwa kazi.
3. Kuimarisha ufanisi kazini kwa kuwapatia wafanyakazi stahiki zao	i. Mishahara ya wafanyakazi imelipwa kwa wakati.
	ii. Michango Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) imetolewa.

11. OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2013/2014

MALENGO YA MWAKA 2013/2014	UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KWA MIEZI TISA
1. Kusimamia matumizi mazuri ya fedha kwa uwazi na uwajibikaji katika Sekta za Umma.	i. Mipango ya awali ya ukaguzi kwa Wizara zote imeandaliwa na imekamilika.
	ii. Mafunzo ya muongozo wa ukaguzi (*Regulatory Audit Manual*) na ujazaji wa "*Working paper*" yalitolewa kwa wakaguzi.
	iii. Mipango mikakati ya ukaguzi imeandaliwa na working paper zimejazwa.
	iv. *Working papers za pre plan na strategic plan* zimepitiwa katika ngazi ya *Chief resident, Zonal* na *Directors.*
	v. Vikao vitano vya Bodi ya utumishi vimeandaliwa.
	vi. Wafanyakazi11 walishiriki katika mafunzo yaliyotolewa na *INTOSAI,* na *SADCOPAC.*
	vii. Mafunzo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo yametolewa kwa wakaguzi 55 na miradi 12 ya maendeleo imekaguliwa.
	viii. Mipango ya kina ya ukaguzi kwa Mawizara yote na Mashirika imeandaliwa na imekamilika
	ix. Mafunzo ya muongozo wa ukaguzi (*Regulatory Audit Manual*) na ujazaji wa "working paper" yalitolewa kwa wakaguzi kwa kushirikiana na *National Audit Office (NAOT*)
	x. Mipango Mikakati ya kina ya ukaguzi imepitiwa katika ngazi tofauti.
	xi. Ukaguzi wa Mawizara na Mashirika umekamilika
	xii. Ufuatiliaji wa maeneo mbalimbali ya ukaguzi umefanyika.
	xiii. Ripoti za awali za ukaguzi zimetolewa kwa Mawizara na Taasisi zake
	xiv. Majibu ya hoja yamefuatiliwa kwa Mawizara na Taasisi zake.
	xv. Ubora wa Ripoti ya Ukaguzi umefanyiwa tathmini
	xvi. Uandishi wa Ripoti ya Ukaguzi ya Mwaka umekamilika.
	xvii. Ripoti za Ukaguzi zipo katika hatua ya uchapaji
	xviii. Tathmini ya awali ya changamoto zilizojitokeza zimeainishwa na kufanyiwa marekebisho
2. Kuimarisha uwezo wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (kuongeza uwezo wa watendaji, vitendea kazi na kuimarisha mazingira ya Ofisi)	i. Wanafunzi 24 wanaoendelea na masomo wameshalipiwa ada na stahiki zao
	ii. *Sever* na vifaa vyake vimenunuliwa na vimeshafungwa.
	iii. Programmu ya ukaguzi imenunuliwa.
	iv. Vifaa na huduma za kiutawala na uendeshaji zimenunuliwa
	v. Jengo la Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Pemba limekamilika
3. Kuimarisha ufanisi kazini kwa kuwapatia wafanyakazi stahiki zao.	i. Wafanyakazi wamelipwa mishahara na stahiki zao kwa wakati
	ii. Gharama za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) zimelipwa.

12. IDARA YA MIPANGO YA KITAIFA, MAENDELEO YA KISEKTA NA KUPUNGUZA UMASIKINI KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2013/2014

MALENGO YA MWAKA 2013/2014	UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KWA MIEZI TISA
1. Kuratibu na kuimarisha Ufuatiliaji wa Programu/ Miradi ya Maendeleo	i. Vikao vimefanyika na washiriki wameweza kujadili utekelezaji wa programu na miradi kwa kipindi cha miezi sita. Aidha ripoti ya matokeo ya mapitio ya programu na miradi ya maendeleo imejadiliwa kwa lengo la kuweka mazingira mazuri ya utekelezaji wa programu na miradi kwa mwaka 2014/2015.
	ii. Jumla ya vitabu 200 vya Mapitio ya Hali ya uchumi na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2012/2013 pamoja na vitabu 100 vya Muelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2013/2014 vimechapishwa
	iii. Kazi ya ukusanyaji wa taarifa kwa ajili ya Bajeti ya mwaka 2014/2015 imeanza pamoja na uandishi wa vitabu vya mpango wa maendeleo (Kitabu cha kwanza na kipindi cha pili)
	iv. Mafunzo ya siku mbili yamefanyika Pemba kwa Maofisa mipango 30 wa Taasisi za Serikali juu ya uandaaji wa mipango, ufuatiliaji na tathminii. Aidha kwa v. Unguja yamefanyika mafunzo juu ya utayarishaji wa malengo, shabaha, viashiria vya ufuatiliaji na uandishi wa ripoti kwa Wakurugenzi Mipango na Maofisa Mipango Wakuu kwa Taasisi za Serikali.
	vi. Ziara mbili za ufuatiliaji wa program na miradi ya maendeleo zimefanyika ambapo jumla ya program 20 na miradi 36 ilitembelewa kwa Unguja na Pemba
	vii. Jumla ya vipeperushi 1,000 vya ushajihishaji vimechapishwa na kusambazwa pamoja na kufanya mikutano ya majadiliano na wananchi wa maeneo ya Bumbwisudi na Kiembesamaki katika Wilaya ya Magharibi.
	viii. Maandalizi ya mafunzo ya uchambuzi wa miradi yamekamilika
	ix. Mafunzo ya siku nne yalifanyika kwa maafisa Mipango na Sera na Utafiti juu ya uaandaaji na uchambuzi wa Sera.
	x. Mapitio ya Programu na miradi ya maendeleo yamefanyika na ripoti imeshatayarishwa. Miradi imeandaliwa kwa mashirikiano na sekta na kuwasilishwa nchi mbali mbali kwa lengo la kupata ufadhili zikiwemo Kuwait, Ras- el Khaimah, Oman na India.
	xi. Maabara za Utalii, Mazingira Bora ya Biashara na Upatikanaji wa Rasilimali Fedha zimefanyika kwa lengo la kuendeleza sekta hizi ikiwemo uibuaji wa programu na miradi inayotekelezeka kwa haraka na kuleta matokeo mazuri kwa ustawi wa wananchi.
	xii. Kalenda 1000 za ukutani na 500 za mezani zimechapishwa na kusambazwa
	xiii. Vikao viwili vya kamati ya wataalamu ya Tume ya Mipango na kikao kimoja cha Tume ya Mipango vimefanyika.
	xiv. Gharama za makisio ya kila study zimetayarishwa. Aidha kazi ya kuandaa dhana *(Concept note*) na hadudi rejea ya utafiti wa hali ya umasikini na fursa zilizopo kwa vijiji vitano imetayarishwa katika maeneo ya Kaskazini Unguja.
	xv. Idara imegharamia safari za ndani na nje ya nchi zikiwemo Semina, Mikutano ya Kikanda, Mafunzo, Warsha na Makongamano kwa Watendaji Wakuu na Maafisa wa Idara zote zilizochini ya Tume ya Mipango.
2. Kuimarisha ufanisi kazini kwa kuwapatia wafanyakazi stahiki zao	i. Mishahara ya wafanyakazi imelipwa pamoja na Michango ya ZSSF imetolewa kwa wakati.

13. IDARA YA MIPANGO NA MAENDELEO YA WATENDAKAZI KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2013/2014

MALENGO YA MWAKA 2013/2014	UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KWA MIEZI TISA
1. Kusimamia Mipango ya Watendakazi, Idadi ya Watu na Ustawi wa Mama na Mtoto Kitaifa	i. Ripoti ya stadi imeandaliwa na kuwasilishwa kwa wadau Unguja na Pemba.
	ii. Uratibu umefanyika kwa Maofisa wa Idara kushiriki katika mikutano ya kikanda na kimataifa juu ya masuala ya idadi ya Watu na Maendeleo nchini Ethiopia na Marekani. Aidha, Maofisa 2 wameshiriki mafunzo juu ya masuala ya Utawala wa Sheria na Uchumi nchini Singapore na China.
	iii. Safari za kikazi kwa ajili ya uratibu wa kazi za Idara Tanzania Bara na Pemba zimefanyika.
2. Kuimarisha ufanisi kazini kwa kuwapatia wafanyakazi stahiki zako	i. Mishahara ya wafanyakazi imelipwa kwa wakati.

14. IDARA YA UKUZAJI UCHUMI KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2013/2014

MALENGO YA MWAKA 2013/2014	UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KWA MIEZI TISA
1. Kufanya uchambuzi wa Pato la Taifa kila Robo mwaka.	i. Ripoti ya Pato la Taifa kwa robo ya nne (Oktoba - Disemba 2013) ilijadiliwa katika kamati ya kujadili mwenendo wa uchumi kwa kila robo mwaka. Kamati ilihusisha sekta husika, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu, *BOT* na Wajumbe kutoka Vyuo Vikuu nchini
2. Kufanya uchambuzi wa Mfumko wa Bei kila mwezi.	i. Kamati ya kujadili na kutoa mapendekezo juu ya kasi ya mfumko wa bei ilikutana mara 9 katika mwezi Julai – Machi 2013/2014 na mapendekezo yaliwasilishwa katika kikao cha ukomo cha Wizara ya Fedha
3. Kuanzisha Database ya utengenezaji wa taarifa za kitaalamu za kifedha na uchambuzi (*Finacial Programming*)	i. Jumla ya wafanyakazi 8 kutoka Tume ya Mipango, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu, *TRA, ZRB* na *BOT* waliounda kikosi kazi ambacho kilipatiwa mafunzo chini ya Wataalamu kutoka *IMF*
4. Kuandaa tafiti za uchumi	i. Ripoti juu ya uhusiano juu ya bei za samaki na misimu ya Utalii nchini inatarajiwa kukamilika
5. Kushiriki katika vikao vya kikanda	i. Wafanya kazi 3 walishiriki katika vikao vya kikanda *EAC, SADC, COMESA, TRIPATITE* na *AU*
6. Kuimarisha ufanisi kazini kwa kuwapatia wafanyakazi stahiki zao	i. Mishahara ya wafanyakazi imelipwa kwa wakati.
	ii. Michango ya *ZSSF* imetolewa kwa wakati.

15. OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2013/2014

MALENGO YA MWAKA 2013/2014	UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KWA MIEZI TISA
1. Kuweka mazingira mazuri kazini kwa kuwapatia wafanyakazi stahiki zao	i. Mishahara ya wafanyakazi imelipwa kwa wakati
	ii. Michango ya wafanyakazi ya *ZSSF* imewasilishwa kwa wakati.
	iii. Wafanyakazi 16 wamelipwa malipo ya fedha za likizo.
2. Kuongeza kiwango cha upatikanaji na ubora wa Takwimu zinazozalishwa na *OCGS*	i. Takwimu za *CPI* zimekusanywa na kutolewa kwa wakati katika kipindi cha robo ya kwanza.
3. Kuendeleza uwezo wa *OCGS* katika kutoa takwimu kwa ajili ya mipango ya maendeleo, ufuatiliaji na tathmini ya mwenendo wa kiuchumi	i. Ofisi imelipa gharama za huduma za habari na mawasiliano.
	ii. Mafuta yamenunuliwa kwa ajili ya kazi za Ofisi zikiwemo ukusanyaji wa takwimu katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar na baadhi ya Taasisi zilizoko Tanzania Bara
	iii. Malipo ya huduma za umeme na maji yamefanyika
	iv. Vifaa mbalimbali vya kuandikia vimenunuliwa
	v. Vifaa vya kusafishia vimenunuliwa
	vi. Ukarabati umefanywa kwenye majengo na miundombinu ya Ofisi
	vii. Vespa moja imenunuliwa kwa matumizi ya Ofisi
	viii. Maofisa watano wamesafiri kwa ajili ya kufuatilia upatikanaji wa takwimu ndani ya Zanzibar na Tanzania Bara
	ix. Ofisi imefanya vikao vitatu vya Bodi ya Takwimu

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa tutaanza kuchangia na ataanza Mwenyekiti wa Kamati ya Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, baadaye atafuatia Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* na nna Mjumbe mmoja tu alioleta kuchangia. Kwa hiyo, mwenye nia ya kuchangia mlete majina ya maombi.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: (Kny) Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa: Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana kwa mara nyengine tena tukiwa hai na wazima wa afya ambayo ni neema kubwa kwetu kwa lengo la kujadili bajeti mwaka 2014/2015 kwa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, pia, napenda kukushukuru wewe binafsi kuweza kunipatia nafasi hii mbele ya Baraza lako tukufu kuweza kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya utekelezaji wa Bajeti kwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, tatu Kamati yangu inamshukuru sana Mhe Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa jinsi anavyoliongoza Taifa letu hili huku tukiwa tunaendelea kula matunda ya Amani,utulivu, mshikamano na maendeleo tunawaomba wananchi wetu kumpa mashirikiano ili kuweza kufikia yale malengo aliyojipangia.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuwasilisha maoni ya Kamati pia napenda kumshukuru Mhe Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na watendaji wa Ofisi hii kwa utendaji mzuri wa kazi zao ambao unaipelekea Kamati kuweza kutekeleza majukumu ya kazi zake za kila siku kwa ufanisi mzuri. Hata hivyo,

napenda kuishukuru Ofisi hii kuweza kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Bajeti ya Wizara yao kwa mwaka 2014/2015 kwa umahiri mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, aidha nitakuwa mwizi wa fadhila nisipowashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa kazi kubwa walioifanya kwa muda wote na ushirikiano wao pamoja na moyo wa dhati katika kutekeleza majukumu yao katika kufanikisha kazi za Kamati ikiwemo hii ya kuchambua na kuijadili Bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, sasa kwa rukhsa yako, naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati yangu kama ifuatavyo:-

1.	Mhe Hamza Hassan Juma	Mwenyekiti
2.	Mhe. Saleh Nassor Juma	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Ali Mzee Ali Mjumbe	Mjumbe
4.	Mhe. Ashura Sharif Ali	Mjumbe
5.	Mhe.Shadya Mohammed Suleiman	Mjumbe
6.	Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Mjumbe
7.	Mhe. Subeit Khamis Faki	Mjumbe
8.	Ndg.Rahma Kombo Mgeni	Katibu
9.	Ndg.Makame Salim Ali Katibu	Katibu

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba kutoa maoni ya Kamati kwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa bajeti hii ya mwaka 2014/2015 kama ifuatavyo:-

TUME YA MIPANGO

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati yetu tunapeleka pongezi za pekee kwa Rais wa Zanzibar na Mweneyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dr. Ali Muhammed Shein ambae ndiye Mwenyekiti wa Tume ya Mipango kwa uongozi wake makini uliombatana na hekima pamoja na busara.

Mhe. Naibu Spika, Kamati pia inatoa pongezi kwa Waziri anaeongoza Wizara hii Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame kwa uwasilishaji wake mzuri wa taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2013 na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2014 / 2015 katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa hiyo iliyowasilishwa na Mhe. Waziri, hali ya uchumi Zanzibar inaonesha kuongezeka ambayo kwa mwaka huu wa 2013 umefikia wastani wa asilimia 7.4 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.1 kwa Mwaka 2012.

Mhe. Naibu Spika, licha ya kuongezeka kwa pato la Taifa ambalo linasababisha kukuwa kwa hali ya Uchumi wa nchi yetu, lakini bado hali ya kimaisha ya watu wa Zanzibar inahitaji kuangaliwa kwa uangalifu zaidi kwani kilio cha umasikini bado kinaendelea kuwaliza Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa miongoni mwa dhamira za Tume hii ni kupunguza umasikini na kukuza uchumi wa nchi yetu Zanzibar, bado Serikali ina kazi kubwa ya kuelekeza nguvu zake katika kuipa kipaombele Tume hii katika bajeti yake ili kuhakikisha kwamba malengo yake yanafanikiwa kwa ajili ya kumkomboa mwananchi wa Zanzibar katika umasikini.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu inaitaka Tume ya Mipango kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kuhakikisha inafanya mapendekezo ya Bajeti ya Serikali mapema ili kuipeleka kwenye Kamati ya Wenyeviti wa Baraza lako tukufu la Wawakilishi la Wananchi wa Zanzibar, ili kuweza kutoa maoni ya awali hasa katika kupanga vipaumbele kwa miradi na taasisi muhimu zaidi ili kuleta wepesi wa kuchangia na kuipitisha Bajeti Kuu ya Serikali pamoja na Mawizara, kwani inaonekana kwa utaratibu tulionao ni kwamba Baraza la Wawakilishi halina nafasi ya kufanya marekebisho yeyote muhimu kwani bajeti ikiletwa inakua tayari imeshapangwa kila Wizara, mfumo ambao katika Mabunge ya Jumuiya ya Madola Bajeti Kuu ya Serikali hupangwa pamoja kwa mashirikiano na Serikali, Bunge na wengine kama vile Uganda wao hushirikisha na Mahakama katika kupanga Bajeti.

Mhe. Naibu Spika, sasa nadhani wakati umefika sasa na sisi tuweze kubadilika tusiende kwa mazowea, lakini pamoja na hayo, hivi sasa Tume inajitahidi kufanya kazi zake kwa ufanisi kiasi kwani hata kwa bajeti ya mwaka huu

imejaribu kupanga Bajeti za Mawizara kwa kuzingatia uhalisia, kitu ambacho kinaweza kutoa vigezo vya kazi ilyopangwa na gharama halisi zinazohitajika kwa kulingana na uwezo wa serikali.

MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMI UCHUMI

Mhe. Naibu Spika, Kamati inapoongeza Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi (*ZAECA*) ambayo kwa sasa tayari imefanya uchunguzi kwa tuhuma 21 zinazohusiana na makosa ya kutoa na kupokea rushwa, matumizi mabaya ya ofisi, ulanguzi wa tiketi za kusafiria, ukwepaji wa kodi, kughushi nyaraka na ukiukwaji wa taratibu za manunuzi. Vile vile, mamalaka tayari imeshawasilisha jadala moja kwa uchunguzi katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashataka kwa ajili ya kuomba kibali cha kuwafikisha watuhumiwa Mahakamani.

Mhe. Naibu Spika, ni ukweli usio pingika kuwa mamlaka hii inafanya kazi zake katika wakati na mazingira magumu sana. Kwa hivyo, serikali inapaswa kuingalia taasisi hii vizuri sana kwani mazingira yao ya kazi ni magumu, sasa ipo haja kwa serikali kuiwezesha taasisi hii kwa hali zote ili waweze kutekeleza majukumu yao vizuri bila ya kuingiliwa na taasisi au mtu yeyote kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, mamlaka hii bado inaendelea kukabiliana na changamoto nyingi katika kutekeleza majukumu ya kazi zake. Kwa hivyo, serikali haina budi kuiongezea bajeti taasisi hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Hasa ukizingatia kuwa taasisi yenyewe ni *change* inahitaji kijijenga na kuweza kutoa mafunzo kwa watumishi wao ambao wanahitaji kuwa na taaluma kubwa zaidi kuliko hao wanaokwenda kuwachunguza.

Mhe. Naibu Spika, pia, inahitajika taasisi hii watumishi wake wote kupatiwa usafiri wa uhakika kulingana na mazingira magumu ya kazi yao kwani hawatakiwi kuomba lifti ya mtu yeyote, mazingira ya kazi zao ni sawa wako vitani muda wote. Aidha, suala la maslahi ya wafanyakazi akiwemo Mkurugenzi mwenyewe, pamoja na vitendea kazi kwa taasisi hii ni jambo la kuangaliwa sana kulingana na mazingira yao ya kazi. Kamati yangu haikuridhika na asilimia 47 ya fedha iliyoingizwa katika robo tatu ya mwaka huu. Kwa hiyo, tunaitaka serikali kuona umuhimu wa kazi za idara hii kwani wakifanya kazi zao vizuri, basi hata udokozi serikalini utapungua na mapato yataongezeka mara dufu.

Mhe. Naibu Spika, mpaka sasa hivi Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumu imepatiwa gari moja tu kutoka serikalini, mbali na jitihada ambazo zinachukuliwa na serikali katika kuipatia vitendea kazi taasisi hii, lakini tunaiomba seriakli kuu kwa mwaka huu wa fedha itenge fedha maalumu katika bajeti yake ili kuipatia gari nyengine taasisi hii.

OFISI YA FARAGHA

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu bado inaendelea kusikitishwa na hali ya baadhi ya majengo yetu ya Ikulu kwani baadhi yao yapo katika hali mbaya kiasi ambacho hayaridhishi kufikia kwa kiongozi wa nchi.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na jitihada kubwa ambayo wizara hii inazifanya na ufinyu wa bajeti tuilionao, lakini bado ipo haja kwa bajeti yetu ya mwaka huu kutenga fungu kwa ajili ya kufanya ukarabati kwa baadhi ya majengo yetu ya Ikulu hasa yalioko kwenye Wilaya za Zanzibar ili yawe na hadhi ya kuwa Ikulu. Aidha, Kamati inashauri serikali ijipange na sio kufanya matengenezo kwa Ikulu tulizonazo tu, bali kuangalia mazingira ya kujenga Ikulu mpya na za kisasa.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inaendelea kusisitiza juu ya umuhimu wa matengenezo ya Ikulu zetu kwa ajili ya kuwawekea mazingira mazuri viongozi wetu pamoja na wageni wanaowatembelea, seriakali haina budi kulipa kipao mbele suala hili katika bajeti zetu. Pia, kama Mkurugenzi wa Idara hii kuwa Ikulu ya Kibweni ingelianza kutumika kuanzia mwezi Juni mwaka huu, basi tunaomba ahadi hiyo itekelezwe kama tulivyokubaliana. Pia, Kamati yangu inaitaka serikali kuhakikisha ujenzi wa Ikulu ndogo kule Micheweni inakamilishwa. Pia, kama tulivyoahidiwa na Waziri kwa mwaka huu wa bajeti unaokuja.

IDARA YA MAWASILIANO YA IKULU

Mhe. Naibu Spika, pamoja na ufinyu wa bajeti tulionao, lakini bado Kamati inatoa pongezi katika idara hii kwa jitihada kubwa wanazozifanya katika kuimarisha mawasiliano baina ya Ikulu na Umma kwa kutoa elimu na taarifa kupitia vyombo mbali mbali vya habari pamoja na kuchapisha majarida tofauti.

Mhe. Naibu Spika, kitengo cha mawasiliano cha Ikulu ni kitengo ambacho pia kinahusika na utunzaji wa nyaraka, Kamati inashauri kuwa kwa mda huu sasa ipo haja ya kuanzisha "*Archaive***"** ya Ikulu ili kuhakikisha kumbukumbu zote za viongozi wetu zinakuwa katika mazingira mazuri na ni zenye kupatikanwa kwa pale inapohitajika.

Mhe. Naibu Spika, kufanya hivyo, kutasaidia sana kwani bado kuna tatizo la upatikanaji wa taarifa za kumbukumbu za viongozi wetu, jambo ambalo linasababishwa na kutokuwepo kwa utunzaji wa uhakika wa kumbukumbu za viongozi wetu, lakini pia, katika kumbukumbu hizo kuhakikisha zile kumbukumbu zote muhimu tangu baada ya Mapinduzi yetu matukufu, basi zinatafutwa na kuhifadhiwa ili ziweze kutumika pale zinapohitajika.

OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu inaipongeza ofisi hii katika utekelezaji wa majukumu yake ili kuhakikisha kuwa kunakuwepo na matumizi mazuri ya rasilimali za serikali pamoja na Mashirika kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na utekelezaji mzuri wa majukumu yake katika ofisi hii, lakini bado inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti jambo ambalo pia linasababisha kwa baadhi ya vitengo kuwa na upungufu wa wafanyakazi na vitendea kazi.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu haijaridhika hata kidogo kuwa *Scheme of Service* ya Afisi hii leo zaidi ya miaka mitano tangu ilipopendekezwa bado Tume ya Utumishi Serikalini haijaiidhinisha.

Mhe. Naibu Spika, inaonesha hii Tume ya Utumishi hawajui nini wanachokifanya kwani wanashindwa kujua ukubwa na uzito wa taasisi hii, kwani inaonesha wao wanadhani Afisi hii kuwa ni sawa na idara nyingine ya serikali, jambo ambalo sio sahihi na hii ni kuidhalilisha na kumdharau *CAG.* Jambo hili sisi kama Wajumbe wa Kamati hii hatulikubali hata kidogo na tunaitaka serikali kuliona hili.

Mhe. Naibu Spika, leo inashangaza sana kumuona Mkuu wa Idara au Mkurugenzi katika Afisi hii ya *CAG* ambae anasimamia *Vote* zaidi ya nne za Wizara tofauti, lakini mshahara wake ni mdogo zaidi ya mara tatu ya Mkurugenzi au Mkuu wa idara serikalini ambae anasimamia *Vote* moja tu. Jambo ambalo hata wenzetu majirani wanatushangaa kwa namna tunavyowalipa watumishi wetu hawa.

Mhe. Naibu Spika, sasa Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Kamati yangu tuhakikishe tunasimama kidete ili kuwalipa watumishi wa Afisi hii maslahi yao yanayopaswa kulipwa mara moja ili kuendelea kuchapa kazi ipasavyo, kwani mazingira yao ya kazi ni fitna tupu na wakati mwengine hupungukiwa sana na marafiki, kwani kazi zao ni mauti kwa wenzao. Kazi ya kuwachunguza watu namna walivyotumia pesa na kuwatolea aibu zao sio jambo rahisi, lakini kwa kuwa ndio wajibu wao, basi hutekeleza wajibu wao bila ya hata huruma yeyote.

Mhe. Naibu Spika, kukua kwa mapato ya serikali katika kipindi hiki cha karibuni kinatokana na kazi kubwa inayofanywa na Afisi hii ya *CAG* hasa kwa kufanya ukaguzi wa kina kwa kasi sana na umakini wa ripoti wanazoziwasilisha kwa Mhe. Rais na pia kuzileta kwako na pia Kamati yetu ya *PAC,* uone uzito wa kazi ya Afisi hii inavyokuwa na uzito wa aina yake katika nchi.

Mhe. Naibu Spika, nimeamua kuchukua muda mrefu kuelezea suala hili kwani linauma na linaidhalilisha Afisi hii na mkuu wake.

Mhe. Naibu Spika, vijana hawa wanafanya kazi ya kizalendo ni lazima walipwe haki zao wanazostahili, kwani wanaweza wakarubuniwa na wabadhirifu ili kuficha ukweli wa uhalisia na kuikosesha mapato serikali.

Mhe. Naibu Spika, ofisi hii kulingana na mazingira yake ya kazi kuna kila haja kwa serikali kuifanya ofisi hii ni yenye kujitegemea na kuwekewa fungu lao maalum na isiwe pamoja na Wizara, Tume ya Uchaguzi kwa kila kitu, ili kuhakikisha ufanisi mzuri katika kutekeleza majukumu ya kazi zake kisheria.

Mhe. Naibu Spika, suala la kuongezewa bajeti katika ofisi hii ni jambo muhimu sana ambalo serikali wanatakiwa kuliangalia vizuri kwa kuzingatia mazingira yao ya kazi zake.

IDARA YA USHIRIKIANO NA URATIBU WA WAZANZIBARI WANAOISHI NJE YA NCHI (DIASPORA)

Mhe. Naibu Spika, Kamati inaipongeza Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia idara hiyo kwa kuandaa Sera ya Diaspora ambayo sasa hivi ipo katika maandalizi ili kuleta mashirikiano mazuri kwa Wazanzibari waliopo nje ya nchi kwa ajili ya maslahi ya nchi yao.

Mhe. Naibu Spika, ifahamike kuwa ili Ofisi hii ifanikiwe malengo yake iliyojipangia ni lazima watoke na waende nje ya nchi ili kuimarisha mahusiano mazuri kwa Wazanzibari waliopo nje ya nchi na kuwapa elimu ya kutosha kwa ajili ya kuisaidia nchi yao ili isonge mbele kimaendeleo.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu bado haijaridhika na bajeti ya idara hii kwani ina jukumu kubwa sana katika kuhakikisha kuwa Wazanzibari waliopo nje ya nchi wanakuwa na msaada wa kutosha katika kupiga hatua ya maendeleo ndani ya nchi yao.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu inaendelea kusisitiza kuongezewa bajeti katika idara hii ili kuiwezesha kuwa na uwezo mzuri wa kutekeleza majukumu yao kwa ajili ya maslahi ya Zanzibar. Aidha, Kamati inaishauri serikali katika bajeti yetu ya mwaka huu bado tunayo nafasi ya kuiangalia idara hii ili kuiongezea fungu lake kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa majukumu yao.

IDARA YA UTAWALA BORA

Mhe. Naibu Spika, pamoja na ufinyu wetu wa bajeti tulionao, lakini Kamati yetu inaipongeza idara hii kwa juhudi kubwa wanazofanya katika kutekeleza majukumu ya kazi zao.

Mhe. Naibu Spika, bado ipo haja kwa serikali kuu kuiongezea bajeti idara hii kwani wanayo kazi kubwa sana katika jamii yetu ya kuhakikisha kuwa jamii inapata elimu ya kutosha juu ya suala zima la Utawala Bora pamoja na Haki za Binadamu. Kupitia elimu hiyo, wanajamii watapata kujua haki zao pamoja na umuhimu wa kuwa na amani katika nchi yetu jambo ambalo ni faraja kubwa kwa Wazanzibari ambalo tunajivunia mpaka sasa hivi.

Mhe. Naibu Spika, idara hii inakabiliwa na changamoto kubwa ya usafiri. Kwa hiyo, Kamati inaendelea kuishauri serikali kutenga fungu maalum katika bajeti yetu ya mwaka huu ili kuipatia gari idara hii.

HITIMISHO

Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine tena kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa mbele ya Baraza lako tukufu. Pia, naomba Waheshimiwa Wajumbe waichambue, waijadili, waiboreshe na mwishowe waipitishe bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza, kwa niaba ya Kamati naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI NA MASHIRIKA *(P.A.C)* KUHUSIANA NA BAJETI YA AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI, KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika): Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye

ametuwezesha kukutana leo hii ndani ya Baraza lako tukufu katika hali ya uzima na afya njema. Aidha, nakushukuru wewe binafsi Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii adhimu na muhimu ili niwasilishe maoni ya Kamati ya *P.A.C* kuhusu Bajeti ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa niingie moja kwa moja kwenye uchanganuzi wa Bajeti ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2014/2015 ambayo imegawika katika sehemu kuu mbili (mapato na matumizi).

MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Afisi ya Mdhibiti inatarajiwa kukusanya jumla ya shilingi 18,000,000 ambazo kwa kiasi kikubwa zitatokana na malipo ya ada ya ukaguzi wa hesabu *(Audit fees).* Ingawa mapato hayo yameongezeka kwa mwaka huu wa fedha ikilinganishwa na mwaka uliopita ambayo yalikuwa ni jumla ya shilingi milioni 15. Kamati inaishauri Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kujitahidi kuongeza ufanisi wa huduma hii kwa kuzivuta taasisi nyingi zaidi kupatiwa huduma hiyo kutoka Afisi yao.

Aidha, kwa upande wa Taasisi za Serikali, Kamati inazitaka taasisi ambazo haziwasilishi hesabu zao kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya hivyo, kwani kuwasilisha taarifa zao ndio kunampa Mdhibiti nafasi ya ukaguzi na hivyo, kuongeza mapato ya Afisi yake.

MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imetengewa jumla ya shilingi 2,023,000,000/=. Bajeti hii ni kubwa kwa asilimia 106 ikilinganishwa na ya mwaka uliopita ambapo Afisi hii ilitengewa shilingi 1,911,000,000/=. Hata hivyo, kutokana na umuhimu wa kazi za Afisi ya Mdhibiti na hali yake hivi sasa, Kamati inatoa wito kwa serikali kutoa kipaumbele maalum kwa Afisi hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa kwa maslahi ya Taifa kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na kuongezeka kwa bajeti hiyo ukilinganisha na mwaka jana, Kamati inapongeza kwa juhudi zinazochukuliwa na serikali katika kuzingatia matumizi ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, lakini inaitaka serikali hii kuongeza zaidi fedha kwa Afisi ya Mdhibiti ili kwenda sambamba na mahitaji halisi ya Afisi hii katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, ili kuweka mazingira bora ya kufanyia kazi katika Afisi ya Mdhibiti, ni vyema mambo yafuatayo yakazingatiwa kwa umuhimu wake:-

Mhe. Naibu Spika, kuongeza maslahi ya Wakaguzi na watendaji wengine wa Afisi ya Mdhibiti ili kuziba mianya ya rushwa.

Mhe. Naibu Spika, ukaguzi wa hesabu ni kazi hatari sana kwani inagusa moja kwa moja maslahi ya mtu binafsi na hivyo, inaweza kuleta chuki na uadui baina ya mkaguzi na mkaguliwa au kuzaa mahusiano yasiyokubalika kwa pande mbili hizi kugawana kile kinachokaguliwa. Kwa maana, tusipowawezesha wakaguzi wetu kimshahara na stahiki mbali mbali, tunahatarisha ufanisi wa kazi za ukaguzi na hivyo, hali ya matumizi mabaya ya fedha za umma itaendelea.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na hali hii, Kamati inaishauri serikali kuwekeza kwenye maslahi yanayostahiki kwa Wakaguzi wetu ili kuokoa fedha nyingi za serikali kwa ajili ya matumizi mengine yanayostahiki, kwani ni imani yetu kuwa tukiacha kuuona umuhimu wa Afisi ya Mdhibiti, tutaendelea kupoteza fedha nyingi sana kwa udhaifu wa Wakaguzi wetu mbele ya Wahasibu ambao ndio wakaguliwa.

Mhe. Naibu Spika, aidha, Kamati imesikitishwa sana na kitendo cha Kamisheni ya Utumishi kuikataa *Scheme of servcse* ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa madai kua haitekelezeki. Ni dhahiri kuwa kitendo cha kuikataa *scheme* hiyo ni kuendelea kuwa na Wakaguzi walio duni mbele ya wale wanaowakagua (Wahasibu) na hivyo, kuwafanya Wakaguzi hao kukosa vishawishi chanya (*Positive motivations*) vya kufanya kazi zao kwa uadilifu na uaminifu.

Mhe. Naibu Spika, changamoto kuu inayowakabili Wakaguzi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni kukosekana kwa vielelezo vya matumizi kwenye taasisi nyingi za serikali. Kamati imebaki katika wakati mgumu na kujiuliza kimezidi nini hata vielelezo vya matumizi vikosekane wakati wa ukaguzi wa Mdhibiti, lakini vipatikane kwa ukamilifu wake wakati wa ziara ya Kamati ya *PAC?* Ni dhahiri kuwa kuna dharau ya wazi iliyojengeka kwa wakaguzi wetu na hii ndio sababu ya kutowekwa kumbukumbu vizuri.

Mhe. Naibu Spika, aidha, Kamati imeshangazwa na tabia hii na kuitaka Afisi ya Mdhibiti kufanya ufuatiliaji wa vielelezo *(Follow up program for supporting documents)* ili kujiridhisha juu ya uhalali wa vielelezo hivyo wananvyopatiwa Wajumbe wa Kamati hii. Ni wajibu wa serikali kulifahamu hili na kuliwekea mikakati madhubuti kwani Mdhibiti ni sehemu ya serikali na kumdharau kwake ni kuidharau serikali.

Mhe. Naibu Spika, ni muhimu tukafahamu kuwa kazi za ukaguzi zinakabiliwa na changamoto ya kukua kila uchao. Hii inasababishwa na mabadiliko ya mifumo ya teknolojia katika eneo la matumizi, malipo na mifumo mengine inayohusiana na taratibu za kibenki za ndani na za Kimataifa. Mbali na mabadiliko ya mifumo hiyo, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar, kama ofisi nyengine katika *AFROSAI* na *INTOSAI,* zinakabiliwa na changamoto ya kufanya ukaguzi katika maeneo mapya ya *VFM, ENVIRONMENTAL AUDITING* na Ukaguzi wa Sera mbali mbali za Serikali, mbali ya ukaguzi wa kawaida kwa taasisi zote za umma nchini. Pia, Ofisi ya Mdhibiti inapaswa kufanya ukaguzi maalum kila haja inapohitajika.

Mhe. Naibu Spika, kwa msingi huo, kuwezeshwa kibajeti pamoja na wakaguzi kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni kitu kisichoepukika kwa nia ya kuchunga kodi za wananchi wetu wanyonge na kulinda mapato mengine ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, kifungu 220500 cha Vifaa na Huduma za Ofisi ya Mdhibiti kimepungua kutoka shilingi 110,396,000 /= mwaka 2013/2014 hadi kufikia shilingi 65,100,000/= kwa mwaka huu wa fedha. Kamati imebaini kuwa mapungufu ya shilingi 45,296,000/= yaliyojitokeza ni kutokana na kwamba mwaka 2013/2014 Afisi ya Mdhibiti ilifanya manunuzi ya *server.*

Mhe. Naibu Spika, Kamati inatoa pongezi kwa Afisi ya Mdhibiti kwa kufanya manunuzi hayo kwani *server* hiyo itazifanya takwimu za Afisi ya Mdhibiti ambazo ni nyaraka nyeti za serikali kubakia kwenye mamlaka ya Mdhibiti mwenyewe.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imekadiriwa kutumia mafuta ya petroli yenye jumla ya shilingi 27,110,000/= fedha ambazo ni mapungufu ya shilingi 1,770,000/= ya bajeti ya mwaka uliopita ambayo ilikuwa ni jumla ya shilingi 28,880,000/=. Kutokana na mapungufu hayo, ni dhahiri kuwa shughuli za ufuatiliaji na ukaguzi zitapungua kwa kiwango kama hicho. Kamati inaiona changamoto hii ni kubwa kwani ilitegemea Afisi ya Mdhibiti kujengewa uwezo zaidi badala ya kuanza kupunguzwa. Matokeo ya mapungufu ya ufuatiliaji ni kutoa mwanya kwa wale wasiokuwa na nia njema na nchi yetu na watu wake kuzitumia fedha za umma kwa maslahi yao binafsi huku wakijua kwamba Mdhibiti hana uwezo mzuri wa kufuatilia na kufanya ukaguzi unaostahiki kwenye taasisi zote za umma.

Mhe. Naibu Spika, Kamati imepokea kwa mara nyengine tena kilio cha Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali cha upungufu mkubwa wa wataalamu waliobobea katika fani adimu kama ujenzi wa majengo, ujenzi wa barabara na kadhalika. Mapungufu haya ya wataalamu kwa kiasi kikubwa yanachangiwa na Afisi ya Mdhibiti kuwa na mishahara midogo ambayo haiwavutii wataalamu wa fani hizo ambazo ni adimu nchini. Jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba, Afisi ina upungufu mkubwa wa wataalamu, lakini kwa mwaka wa fedha 2013/2014 haikufanya uajiri kabisa kutokana na kukosekana kibali cha uajiri.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Afisi ya Mdhibiti imeomba tena ruhusa ya kuajiri ili kuziba mapengo waliyonayo. Majibu ya ombi hilo ni ya kukatisha tamaa kwani walitakiwa wasiajiri wafanyakazi wapya, bali watapatiwa watendaji kutoka taasisi nyengine za serikali ili kuungana nao katika majukumu yao ya kila siku.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na unyeti wa kazi ya ukaguzi na mazingira yake ni vyema serikali ikaipatia Afisi ya Mdhibiti kibali cha uajiri wa wataalamu kutoka popote pale (ndani na nje ya serikali) ili kukidhi mahitaji ya Afisi

katika utekelezaji wa majukumu yake. Kutokana na hili, Kamati inashauri utoaji wa vibali vya uajiri uzingatie hali halisi na mahitaji ya uajiri iliyonayo ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, utalii ni sekta inayokua kwa kasi hapa Zanzibar na inategemewa kuchangia zaidi kwenye pato la Taifa kwa miaka ijayo. Hivyo, Kamati inatoa wito kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalum (*Special audit*) katika eneo hili. Katika kutekeleza hilo, ni vyema Mdhibiti akawekewa mazingira mazuri ya upatikanaji wa wadau wote wa Sekta ya Utalii wanaostahiki kufanyiwa uchunguzi. Aidha, mahusiano ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar na Idara ya Uhamiaji ya Tanzania yanapaswa kuimarishwa ili kuchangia upatikanaji wa takwimu za watalii wanaoingia nchini ili kuruhusu ukaguzi kufanyika kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, Tukijikita katika vyanzo vyetu vya mapato, Baraza liliona haja kubwa ya kumtaka Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu kufanya ukaguzi katika chanzo chetu cha mapato cha *Zanzibar Meritime Authority (ZMA)* na hatimaye kuwasilisha ripoti ya ukaguzi huo mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inahoji hatma ya ukaguzi maalum ulioagizwa na ni lini ripoti yake italetwa Barazani, ili Baraza na wananchi kujiridhisha kwamba mapato yanayotokana na taasisi hiyo yanakusanywa na kutumika kwa mujibu wa sheria ya fedha na Kanuni tulizojiwekea.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati, naomba kwanza nimpongeze Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kujenga jengo jipya na la kisasa katika Kisiwa cha Pemba. Ujenzi uliochukua muda wa miezi tisa na kutumia jumla ya shilingi milioni mia mbili na tisini hadi kumalizika hadi fanicha, fedha ambazo zilitokana na fungu la *Other Charges (OC).* (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kukamilika kwa ujenzi huo, uliofanywa katika mazingira haya ni kielelezo tosha kwamba kila kitu kinawezekana, kinachohitajika ni utashi na uzalendo. Kama kila mtendaji angekuwa na utashi na uzalendo kama huo wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu hapana shaka hatua kubwa ya kimaendeleo tungelifikia ndani ya kipindi kifupi, seuze miaka 50 ya Mapinduzi yetu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu hii walishirikiana bega kwa bega katika kutekeleza majukumu yao ya msingi ambayo yameainishwa katika Kanuni ya 118 (2) ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi Toleo la 2012. Hatua hiyo, jasiri na uzalendo wa hali ya juu kwani ni ukweli usiopingika kuwa muda huu wa lala salama ni muhimu sana kwa Wajumbe na wanasiasa kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa niwatambue Wajumbe wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Mahesabu ya Serikali kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Omar Ali Shehe	Mwenyekiti
2.	Mhe. Fatma Mbarouk Said	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Shamshi Vuai Nahodha	Mjumbe
4.	Mhe. Rufai Said Rufai	Mjumbe
5.	Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Mjumbe
6.	Mhe. Salma Mussa Bilali	Mjumbe
7.	Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Mjumbe
8.	Mhe. Salim Abdalla Hamad	Mjumbe

Mhe. Naibu Spika, aidha, ninatoa pongezi za dhati kwa Makatibu wa Kamati ambao kwa kiasi kikubwa wamesaidia sana Kamati yetu katika kufikia malengo yao ambao ni:-

1.	Ndg. Asma Ali Kassim	Katibu
2.	Ndg. Othman Ali Haji	Katibu

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa na taadhima iliyopita kiasi, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*. Sasa tunaingia kwenye michangio ya jumla. Nina wachangiaji wawili; wa kwanza atakuwa ni Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na wa pili, ni Mhe. Hija Hassan Hija. (*Makofi*)

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: *Bismillahi Rahman Rahim.* Mhe. Naibu Spika, kwa jina nimeanza jina tukufu kabisa na hasa leo kidogo nina mafua naomba munistahamilie na kwa kuwa leo tupo kidogo naomba unistahamilie mpaka saa saba, maana yake hii wizara kubwa sana, ijapokuwa tuweke Kanuni kando.

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi leo kunipa nafasi hii kuweza kuichangia. Naomba sana na kama Rais wetu yupo huko Ikulu, naomba sana anisikilize kwa makini sana, kwa sababu nina *modern* siku hizi ya kuchangia. Hata hiyo, nimeamua kwa makusudi kujitolea wala sitaki mfadhili kutoka nje.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu kama hatukusema hivi, basi na kazi zinakwenda zinarotesha kwa jamii wetu ambao waliotupigia kura. Mimi ninataka tushinde na kiendelee kushinda kwa chama changu kupitia kwa mawaziri ambao tulikuwa tumewachagua.

Mhe. Naibu Spika, niingie kwenye ukurasa huu ambao ni wa 24, "Kitengo cha *GSO*". Kutembelea ni kuona mengi katika dunia, lakini kitengo hichi mimi naona bado, niseme labda kina upungufu wa kitaaluma au niseme kuwa hakina *supporting* kubwa kwa serikali au niseme kwa lugha nyengine kuwa bajeti inakuwa kwao ni ndogo.

Mhe. Naibu Spika, lakini hichi kitengo si mchezo ni roho ya nchi, kama hatukuwa na *serious* nacho kitengo hichi ni hatari kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, tuna mengi sana, ikiwa labda hiyo sheria imekaa upande kidogo, basi ningeomba hiyo sheria tuirekebishe, kwa sababu sheria ndio inayompa mtu nguvu utekelezaji wake kuwa wa ufanisi kabisa.

Mhe. Naibu Spika, unajua *GSO* kazi yao kubwa kwa wafanyakazi wanaotaka kufanya kazi serikalini, ikiwa wanawafanyia upekuzi, wanafanya kuwafuatilia ambao ni wa ndani hao kufuatilia. Sijui kama sheria ipo ya wa nje nao kuwafuatilia, kama sheria ipo, basi *okay*, kama hakuna hiyo ni tatizo. Ni lazima sheria hiyo *doctor* alete, tuweze kuirekebisha ili tuwape nguvu kwa kuweza kufanya kazi zao, kwa sababu unamtizama wa ndani, lakini wa nje humjui.

Mhe. Naibu Spika, ndio maana tunapata taabu sana kwa haya makampuni ya nje wanaokuja hapa nchini kwetu, wana-*forge* hata vyeti.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, nikuomba jambo moja karibuni lilitokea wimbi lile kama kweli sijui kama kweli lile la vijana wetu tumeambiwa wame-*forge* vyeti na wanarejeshwa wakati Polisi wameshamaliza mafunzo.

Mhe. Naibu Spika, sijui kama kweli, lakini kama kweli Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hili suala au Rais mwenyewe tunawaombeni kuwa hilo lililopita ndio limeshapita, sasa wale wa ndani na isitoshe wale wameshapata *training* mafunzo makubwa sana na ni ya hatari.

Mhe. Naibu Spika, sasa ili tuseme ndio yameshapotea. Kwa hivyo, ndio mara ya pili tujifanyia *correction*, tukisema wale tuwaachie, hili suala litakuwa kuwa kubwa sana. Naomba sana Mhe. Waziri mumpelekee Rais na Makamu wa Rais. Naomba hili suala alifuatilie kwa huruma kabisa, wale ni watoto wetu tumeshawafundisha mafunzo makubwa sana na si kitu cha mchezo. Mimi naomba hili tukazungumze hili na wenzetu, tukawalilie ili tuweze kufanya nini.

Mhe. Naibu Spika, lakini wa nje ni wa hatari. *Forgery* zipo nyingi na wanaachiwa tu, hata mapato yetu ya *foreign* tunayokosa. Wanakuja kwenye mahoteli, vyeti vyenyewe havilingani na uwezo wao wa kufanya kazi, lakini almuradi tu wanajua hili ni shamba la bibi huko Zanzibar wanakuja kuchukua mapato. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi nipo *serious*, si kitu cha mchezo ninakwambieni kabisa na siku zote ninasema tuwe mawaziri wasilete mizigo kwa serikali wawe mawaziri wazuri kutokana na utendaji wao, makatibu wao wasiwe mzigo kwa serikali, wawe watendaji wazuri ili serikali iweze kufanya kazi, ipate kazi ifuatilie mambo mazuri.

Ninaamini *Doctor* wangu Dkt. Mwinyihaji sio mzigo, Katibu wangu ninaamini sio mzigo, kabisa ninaamini hivyo, kwa sababu nikiwapa kazi, baadae waniambie ndio nitawaambia nyinyi mzigo, wala sitoona taabu kuwaambia, nitamwambia Mhe. Rais Ali Mohammed Shein ondoa hao, mzigo tu, tunawapa serikali bure, lakini hivi sasa sio mzigo kwa sababu tokea tumeanza hiyo *plan* ya kuweza kuwaambia watu kama hao.

Mhe. Naibu Spika, naomba tuletewe sheria ya *GSO,* itanuliwe kwa mujibu wa kisekta, kwa sababu ninatoa *example* mmoja, nimekwenda Austria. Austrilia kuna mtu ali-*forge* cheti, ni mtu wa nchi nyengine, alikwenda kufanya kazi pale mambo ya hoteli, lakini kwa kuwa kuna vitengo vyao vinafanya kazi, vilimgundua yule mtu, hatimaye akafungiwa mpaka ile hoteli, ndio sheria zao walivyoweka.

Mhe. Naibu Spika, sasa na sisi watu wengi jamani wimbi hili. Sasa naomba sana hii sheria kama imekuwa ndogo tuifanye *modern* sasa hivi wawe na meno ya kuweza kufanya hivyo kuingia mpaka kwenye Makampuni ili wasije kuchukua nafasi za watu wetu. Vijana tumewasomesha, serikali imejitahidi kuwasomesha vijana, lakini chuo nao ni jambo la kuchekesha kweli, wanam-*training* mtu ndani ya nchi na yeye anaambiwa ana vyeti babu kubwa, vyeti vikubwa utaona, lakini anafanyiwa *training* na yule yule Mtanzania ndani ya nchi yake, hatimaye anaondoka na pesa zetu, yule analala maskini au yule yule anazunguka anamtia ushawishi, afukuzwe, anamtukana.

Mhe. Naibu Spika, sasa tuamke, ninashukuru sana hichi kitengo kifanye kazi zake kwa bidii. Naomba fedha ulizoleta hizi, basi naona kidogo twende na wakati kwa sababu hawa wanatakiwa waenee wapate, wawe wana *programme* za kufuatilia haya mambo. Mara utaambiwa hawana mafuta, hawana nini.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende kwenye ukurasa wa 36. Rushwa ni adui wa haki. Hapa nimeona tunakwenda semina wanakwenda kwenye Jimbo la Kitope kwenda kufanya semina. Aah! kuna nini? Unajiuliza huyu mtu unakwenda kumfanyia semina Jimbo la Kitope, kuna nini? Hebu tuzielekeze semina kule kunakohusika kwenda kule kunakoliwa hasa. Unakwenda katika Jimbo la Kitope wanajuaje mambo haya?

Mhe. Naibu Spika, lakini huyu huyu wa Jimbo la Kitope ndiye aliyeliwa zile rushwa, nyinyi hamjui kwa sababu ana haki yake huyu anataka aipate, haipati mpaka aelekeze rushwa. Sisi ndio tunaosababisha rushwa, tupewe semina sisi, viongozi sisi ndio tupewe semina, mawaziri wapewe semina, makatibu wakuu, wakurugenzi wapewe semina, ndio huko kunakotakiwa bwana. Yule mtu wa chini afanye nini? (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, *Wallahi* mtu wa Kitope hajui hata kusema, ukimwambia hebu tukae pembeni bwana, yeye hawezi kusema kwa sababu anachojua yeye kupata haki yake. Wapo Masheha wanauza eka. Wapeni semina hao kwa sababu wanauza eka kinyume na utaratibu, maana yake ni rushwa. Hayo ndio maeneo ya kufanyiwa semina, hebu tupeni semina sisi, sisi ndio wenyewe bwana, tunaanzisha rushwa, sio yule mtu wa Kitope.

Mhe. Naibu Spika, kesho anafuatilia ardhi yake kishanyang'anywa anateseka kule kwenye kupata haki, kishafukuzwa kazini anahangaisha maskini wa Mungu, wewe utafuatilia mpaka utachoka zungumza, haiondoki rushwa kwa misingi hiyo kwa kwenda kuwapa semina watu wale wa chini kule. Tusidanganyane haki ya Mungu tusidanganyane, mimi ninakwambieni kweli ulivyo.

Mhe. Naibu Spika, nimekwambieni mapema leo Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kwamba Mshimba anazungumza sasa, ndio ninayazungumza haya, haiondoki rushwa, tusimdanganye Mhe. Rais. Mimi angeniita siku moja ningemwambia ukweli, lakini haniti bahati mbaya, mimi ninataka nikae tuzungumze hali hii, kwa sababu ningemwambia usidanganyike kwenye *tables* tu Mhe. Rais, haiondoki ng'o kama sisi hatukudhibitiwa juu, sisi ndio tunaotoa rushwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli inasikitisha. Hichi kitengo tumekiunda, lakini kwa kweli *just bortion* tu, hatupo *serious* nacho kitengo hichi. Kwa kweli sisi tunataka na jina la kikosi cha kuzuia rushwa, tunawapa taabu maskini ya Mungu, jamaa yule na elimu tunampotezea muda tu. Mimi niseme ukweli maskini ya Mungu, hana njia hata siku moja atakayoifanya hivyo.

Mhe. Naibu Spika, nani akamkamate Mshimba yule, masihara nini, hamkamati hata siku moja, kwa sababu ana *limit*, ana mpaka. Kuna mpaka ambao unaonesha *original* na kuna mpaka ambao hauoneshi, yeye mwenyewe atakuwa na nadharia tu.

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi naomba tusikifanyia masihara kitengo hichi, tuwape zana za kutosha, bajeti zake ziwe za kutosha, tuwe huru, sheria iongezwe. Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa unani-*interfere*, sipati kuzungumza uzuri.

Mhe. Naibu Spika, hiki kitengo ni kizuri sana, kitengo hichi ambacho kitamuwezesha yule maskini angalau aijue haki yake bila ya kutoa rushwa, lakini hatutofikia *stage* hiyo kutokana na hali hiyo, tunawabana sana. Naomba sana kitengo hichi kiweze kusaidiwa kwa hali na mali.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye ukurasa wa 38, hii mimi siwezi kutoa *comments* sana, isipokuwa ninatoa ushauri wangu tu. Siibani wizara hii kwa sababu mimi mwenyewe ni kamanda, isipokuwa ninataka niuze hapa, ninauza hapa *idea* yangu, ikiwa umeipata sawa, hakupata basi, lakini ipo siku atanitafuta, ni bure kwa sababu mimi sitaki *foreign*, ni bure, huo ndio ushauri wangu.

Mhe. Naibu Spika, sasa niingie kwa Mdhabiti, mimi simsifu mtu isipokuwa ninamsifu kwa kazi yake. Huyu mama jasiri naye, mama huyu ni mjasiri sana na ndio maana ninatoa pendekezo. Sheria bado ingali *weak* kwake yeye inampa taabu sana na hii mara nyingi sana ninasema. Hebu jamani tukisema kaeni na wataalamu. Nimemsikia Mwenyekiti anasema Dkt. Omar pale, anasema kuwa kuna watu wengine wanashindwa kupata vielelezo. Mdhibiti anashindwa kufanya kazi yake, ndio ana sheria gani ya kumwambia yule mtu jambo jengine pale, kenda hakufuata, basi anaondoka, lakini hebu mpeni sheria uone, amekuta suala kama lile mtu hana vielelezo anashindwa kufanya hesabu zake au mambo yake anayokusudia tia ndani uone kama hatofanya kazi.

Mhe. Naibu Spika, anaweza mama, ni jasiri kweli sikufichi haogopi, mpeni sheria muone hapa, masihara! Lakini leo anafanya kazi zake, anafanya mahesabu yake, anadhibiti ndani ya *briefcase* tu, mchezo umekwisha, anazipeleka wapi? Huko anakozipeleka ndio yule yule mlaji, niambieni itahukumiwa wapi hiyo kesi? Si vichekesho hivyo.

Mhe. Naibu Spika, lakini mpeni sheria ambayo itakayomuwezesha aende nayo sheria ile, uone kama mapato ya serikali yatavuja na yataibiwa upuuzi upuuzi hapa.

Mhe. Naibu Spika, hii ni *serious* kweli, sheria hii bado ni nyepesi, tafuteni wanasheria wapo, waulizeni nini tufanye sheria itatupiga vipi tukimpa meno haya? Tusione taabu wapo hapa kibao wazee wetu wa kuwauliza sheria hizo, lakini tunakaa tunazungumza, inasikitisha kila siku Mwenyekiti wa *PAC* anazungumza yale yale kila siku tu.

Mhe. Naibu Spika, leo ninataka uniambie Mhe. Naibu Spika, baada ya kudhibiti wizara ngapi zimekamatwa na matatizo. Mbona hujaja kuniambia sasa hapa? Utuambie wizara kadhaa zimekuta mapungufu ya fedha kiasi kadhaa na sheria imefanya hivi na hivi. Leo ninataka nione hapa, njoo unijibu Mheshimiwa *doctor* hapa, nijibu na ukinijibu ninakusifu hapa wala sina tatizo na wewe. Nitaunga mkono kwa sababu ni Mjumbe tu, lakini ilikuwa wala nisiunge mkono hiyo.
Mhe. Naibu Spika, nchi za wenzetu wanakuwa na *balance* katika *programme* zao za bajeti zao za wizara kutokana na mambo kama hayo katika kitengo kama hichi, kwa sababu huyu ndiye anayeona, huyu ndiye anayejua, kasoro zote zinajulikana za utekelezaji, yeye huyu ndiye anayeona, lakini maskini ya Mungu anafuatilia, akifuatilia anakwenda kumkabidhi Katibu mwenyewe muhusika wa wizara ile.

Mhe. Naibu Spika, utapata hukumu hapo au anakwenda kumpa Waziri? Samahani Waziri wa Maji nimekuta kule wizara yako mapungufu ya bilioni mbili, hizi fedha kadhaa wa kadhaa. Niambie kenda kupelekewa Waziri mwenyewe, unafikiri atafanya nini kama pengine kapewa chochote na yeye.

Mhe. Naibu Spika, sasa apewe sheria zitakazomuwezesha awe kinara katika sheria mpaka ahakikishe yule mtu katiwa kabari, kafukuzwa kazini, amelipa mapesa ya watu. Hapo ndipo tutaamini kama kweli Mdhabiti na Muweka Hesabu wetu anafanya kazi vizuri, lakini vyenginevyo, vyovyote masuala ya posho uliyesema ninayo sababu, kwa sababu umlinde yeye kwanza kabla ya hiyo sheria imtengeneze huyu kwanza mtekelezaji sheria.

Mhe. Naibu Spika, atageuka huyo, mshahara wenyewe mdogo, ameshakuta mapungufu ya pesa bilioni ya fedha, jamaa huyo atakula tu huyo, lakini tunapomtengenezea sheria na yeye tushamtengeneza vizuri, anajua kwa mwezi na mimi ninachukua milioni tano, aah! mimi hata aje nani, basi sibabaiki hapo, kwa sababu milioni tano si mchezo nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, hapa inaonesha sehemu moja inaonesha mapungufu ya bei. Hawa wanapatana kila siku, nataka niseme hivi hebu mawaziri nawaombeni sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, nawaomba mawaziri wako, hebu sasa hivi bajeti zinazokuja tuweke jina letu katika mawizara, tuje na hadithi ya utekelezaji kwa asilimia mia pamoja na makatibu wetu, tuje na utekelezaji kwa asilimia mia. Tena nataka mumwambie namshauri na Mhe. Rais awe na kigezo cha aina hiyo, asiyeweza kufikisha amfukuze wako wengi tu, watu wengi wamesoma kina Mussa, wako wengi tu, wanautaka uwaziri wako wengi kabisa nimekuambia Mhe. Naibu Spika, awe na kigezo tena kigezo kizuri sana, hapo ndipo atakapojua kama waziri anafanyakazi, katibu ni msimamizi mzuri. Lakini vyengine vyovyote Mhe. Naibu Spika, itakuwa ni hadithi zile zile, tunazungumza kwenye kitabu, lakini utekelezaji wake unakuwa ni mdogo.

Ninatoa ushauri kumshauri Mhe. Rais wangu, aangalie vigezo tunavyovizungumza Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi. Hatuwaonei, mimi wala siwaonei shida hawa, wala siwaonei wivu kuwa mawaziri hata siku moja, mimi ni sawa sawa na wao, akinikera mtu nampiga hapa hapa mchezo umekwisha, akininunia shauri yake, akinikaribisha wizarani kwake sawa, hakunikaribisha mimi ndio nimeshapata kusema kuwa ninajisifia kuwa kaninunia na kanikimbia wizarani, ndio utekelezaji upo hapa. Lakini naamini hawafanyi hivyo, nawashukuru kwa hilo, Mwenyezi Mungu awajaze, awape baraka zote kuwa wanatusikiliza japo wengine simu hawatupokelei, lakini ndio mtindo huo sasa. Tunaambiwa *network buzz* sio tatizo. Maana yake utampigia katibu simu hapokei, utampigia waziri ndio hivyo yuko *buzz*, sio tatizo nalo hilo. Lakini wakiingia hapa na sisi ndio tuna *beep* hapa.

Kwa hivyo, mimi naomba sana Mhe. Naibu Spika, kwamba tuangalie, kwa nini nchi yetu inapanda mifumko ya bei kila leo Dkt. Mwinyihaji fuatilia, pengine kuna sababu ya msingi. Lakini mtawatilia mapesa chungu mzima vitengo hivi, hatimaye hakuna hata moja. Mimi naomba sana Mhe. Naibu Spika, wananungunika wananchi, ndio maana wananchi wanasema bora mishahara msiwapandishie lakini vyakula vishuke bei, kwa sababu itaendana na zile pesa ambazo mmewaachia wanazo hivi sasa, lakini kuliko kuwapandishia mishahara na vyakula vinazidi kupanda bei, itakuwa kazi bure tu.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mimi hii ni Wizara yangu na ni jumla ya Kamati yangu. Lakini nizungumze moja la mwisho. Juzi tu Mhe. Naibu Spika, tulikuwa kwenye maandamano yetu Nungwi, katika kutembea kwangu niliwakuta askari wanashughulika katika kisakina kubadilisha mpira. Nasema angemaliza Balozi pale kwenda kuhutumia, ingebidi tumuweke pahali kwanza tumpige *story*, kumbe hajui kisakina kinabadilishwa mpira. Jamani naomba sana tusiwaaibishe viongozi wetu. Dkt. Mwinyihaji mwambie Rais wetu Dkt. Shein ni muhimu sakina mpya jamani. Juzi ilikuwa aibu kisakina kinabadilishwa, watu walijitutumua, watu watano mpaka sita kwa kubadilisha tairi tu ile, juzi tu Nungwi kule.

Mimi nilikuwa natembea tembea nikakikuta kimelala hivi, nikacheka sana. Nasema ile simu yangu imenipotea Mhe. Naibu Spika, ningekuonesha picha kama Mhe. Jaku Hashim alivyokuonesha picha leo. Naomba sana visakina muhimu sana kuwanavyo. Mhe. Naibu Spika, naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango tena kwa ufupi, kwenye hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu Dkt. Mwinyihaji Makame, hotuba ambayo imewasilishwa asubuhi ya leo.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba nitowe mchango kwa ufupi sana leo, kwa sababu sioni la kusema zaidi baada yale ambayo tumezungumza kwa miaka mingi. Mhe. Naibu Spika, niende kwenye ukurasa wa 35 mpaka 37 kuhusu Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa na Kuhujumu Uchumi, ambayo imechukua kurasa 3 Dkt. Mwinyihaji anaelezea. Nilitegemea angetuelezea tangu Mamlaka hii iundwe ni watu wangapi wamekamatwa au kufikiwa kwa matatizo haya ya rushwa. Atakapokuja kujibu najua atasema kwamba bado mamlaka changa ndio tunaijenga, ilikuwa haina ofisi, wafanyakazi walikuwa wachache. Lakini ukweli ulivyo na naendelea kusema mimi kwa imani yangu, kwamba hatuwezi kuweka Mamlaka hizi wakati sisi wenyewe ndio tatizo la msingi. Huwezi kuweka Mamlaka kama hizi, ikiwa wewe uliyeweka Mamlaka ndio unatatizo la msingi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alisema pale na yale ni ukweli kwamba hata utembee majimbo yote kwa wananchi wa kawaida, ukaelimishe hiyo rushwa ni kuwachezea wananchi akili tu. Lakini wale ambao wanaviashiria vya rushwa, wala sio wananchi wadogo wadogo walioko chini, ni watu wenye maarifa, ni watu wenye uwezo, ni watu wenye elimu nzuri na ndio hao waliokuwa karibu sana na rushwa.

Kwa hivyo, na mimi naunga mkono ile hoja ya Mhe. Makame Mshimba, kwamba wala tusielimishwe, sijui tufanywe nini sisi ambao tuko katika nafasi muhimu, tupewe dozi ya uhakika ili tuondokane na hili tatizo la rushwa. Sasa Mhe. Waziri atakapokuja mimi na anieleze tangu tuunde mamlaka hii, pamoja na uchanga wake na kwamba najua kwamba ofisi hii bado ina vikwazo vingi, vikiwemo fedha na vitendea kazi. Lakini naamini mimi kwamba hata kama fedha atazipata, hata kama atapata vitendea kazi, madamu hatuna nia ya dhati ya kuwapa nguvu wenzetu kufanya kazi hii tuliowachagulia, bado tutaendelea kuimba wimbo huu wa rushwa, lakini hakuna ukweli utakaotekelezwa.

Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba tuwache tabia yakuwachezea wananchi, na tujuwe kwamba sisi ni dhamana ya wananchi wa Zanzibar, ni lazima tufanye wajibu wetu kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa uwezo Mwenyezi Mungu aliotujaalia. Tabia hii ya kuimba imba tu rushwa, uongozi bora, utawala bora wakati hakuna hatua, nadhani tuwache kufanya masihara hayo, tuwafanyie haki Wazanzibari na kwamba sisi ndio dhamana ya Wazanzibari wote wa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Idara ya Utawala Bora. Tayari hapa Mhe. Waziri ametuambia kwamba kuna sheria nyengine mpya inakuja, sheria ya maadili ya viongozi. Ilipokuja Sheria ya rushwa watu waliona kama Sheria ile itafanyakazi siku ya pili baada ya kupitishwa. Hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa zaidi ya kuimba wimbo ndani ya vitabu, na leo Mhe. Waziri anatuletea sheria nyengine mpya ya maadili ya viongozi. Naamini itakuja hapa na itapitishwa, lakini hakuna hatua yoyote. Kwa sababu wanaambiwa tu wananchi kuna maadili ya viongozi, lakini viongozi ndio nani, si sisi humu, ni sisi humu ndani.

Mhe. Naibu Spika, juzi hapa nilitoa mfano mdogo tu, kuhoji matumizi ya fedha za umma Baraza la Wawakilishi. Watu wote walikasirika humu, jambo dogo tu, naeleza matumizi ya fedha za humu Baraza la Wawakilishi kwamba ni nyingi katika safari za nje, wote wamekasirika humu. Leo unakuja hapa na vitabu vizuri unawadanganya wananchi maadili ya viongozi, maana yake tuko wasafi, nani kiongozi kama sio sisi humu ndani.

Mhe. Naibu Spika, tuwache kuwadanganya wananchi, Wazanzibari wana akili sawa na sisi au zaidi ya sisi, ni lazima tuwe waadilifu na tuwe waungwana kuwafanyia haki Wazanzibari wetu. Kwa hivyo, sheria hizo zinazokuja ziwe ni sheria ambazo zina meno kwa Wazanzibari ili tuwafanyie haki kama dhamana ya viongozi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 24 na 25 kuna GSO. Mimi nimekuwa nikijiuliza, unapoweka GSO na ukali huu ulioelezwa kwenye kitabu, lakini ndio hivyo askari wana-*forge* vyeti, wafanyakazi wana-*forge* vyeti na kuna *security vetting* inafanywa kila siku. GSO inakuwa likizo au kuna wengine ni sehemu ya GSO na kuna wengine hawapekuliwi.

Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa kwenye Kamati moja Pemba, nilikuwa namuona mtu anapekuliwa na *GSO*, lakini anaandikiwa kama huyu ni mwana CCM kindaki ndaki, huyu ni ndugu yake waziri fulani, huyu ni ndugu yake Mhe. Omar Ali Shehe. Sasa najiuliza hiyo ndio kazi ya *GSO*, kwamba inatafuta ukoo wa mtu. Hiyo tumegundua Pemba, mimi nilikuwa kwenye Kamati na wenzangu hao na wakatae, mtu ameandikiwa hasa kwamba huyu ni ndugu yake fulani, huyu ni mwana CCM, huyu mjomba wake wa karibu ni mwana CUF. Najiuliza hiyo *GSO* ndio kazi yake na ushahidi wa hilo ni kwamba tayari sasa linajulikana *GSO* ipo, lakini watu wanaajiriwa wakiwa hawana sifa, hatimaye wenzetu wa *nationalism* watu imewatimua kwamba hawana sifa. Unajiuliza kwamba *GSO* inafanyakazi gani?

Mhe. Naibu Spika, mimi niombe tu kwamba tusiendelee kuandika maneno matamu, lakini yakiwa hayana utekelezaji na tukawafanya kama Wazanzibari hawana maarifa au hawajui ukweli unaotendeka.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Ofisi ya *CAG* ambayo kwa kweli kwa leo itakuwa ndio mchango wangu wa mwisho, lakini nataka nieleze kwa upana katika ofisi hii. Mhe. Naibu Spika, kwenye kifungu cha 77 ukurasa wa 39 Mhe. Waziri amezungumzia kwamba ofisi ya *CAG* imeendelea na matengenezo ya jengo la Pemba na kwamba karibu watamaliza kazi na kuanza kulihamia. Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* anatuambia kwamba ofisi ya *CAG* Pemba imejenga jengo la kisasa kwa shilingi milioni 290. Nataka nione nani anatuchezea akili, huyu amejenga au ametengeneza. Lakini nilipoangalia mtandao wa simu, nimepigiwa picha Pemba sasa hivi, niliwaambia vijana

wangu wameniletea jengo la zamani la *CAG* ambalo ni kama *godown* hivi, lakini pia wameniletea jengo la sasa ambalo ni jipya kabisa la ofisi ya *CAG* la ghorofa moja na picha imo kwenye simu wamenirushia vijana wangu.

Kwa hivyo, ukweli ni kwamba *CAG* kwa ujumla wake wamejenga jengo la kisasa la ghorofa moja Pemba, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani naomba nimpongeze. Nimpongeze kwamba yeye ndio anaonesha utawala bora, yeye ndio anaonesha *value for money*, matumizi mazuri ya fedha za umma. Jengo la ghorofa moja ambalo amejenga kwa shilingi milioni 290 linanikumbusha mbali, linanikumbusha lile jengo la Wizara ya Fedha Pemba, limejengwa kwa 1.6 bilioni lakini hakuna jengo. Tena *CAG* amejenga kwa fedha za *OC*, sio mradi wa maendeleo, amejibana na kukasimu fedha zake amejenga jengo. Serikali hii inajenga majengo kwa miradi ya maendeleo hakuna yanayoendelea.

Mhe. Naibu Spika, leo jengo la Pemba la Wizara ya Fedha limewekewa miunda. Ni nani amewaambia jengo la ghorofa linawekewa mwega, ni nani aliyewaambia duniani. Kama sio mgomba wa kiguruwe au mgomba wa tembo au mkono mmoja. Watu wanatudanganya maarifa yao wanatudanganya wanaweka jengo miunda, jengo la ghorofa nne limezuiliwa kwa miunda, halafu anawaambia Wazanzibari tulieni mambo yanakwenda vizuri. *CAG* ni mfano mzuri sana na yeye ni mara ya tatu hii anajenga majengo kwa value ndogo lakini kwa thamani kubwa. Amejenga Unguja majengo mazuri mawili na leo amejenga Pemba jengo zuri la ghorofa moja kwa gharama ndogo lakini jengo la maana.

Mimi naomba Waheshimiwa Wajumbe nimpongeze sana mheshimiwa *CAG*, kwa kweli ameonesha kwamba huyu mama anaweza kufanya kazi. Unaposema haya watu wanajiuliza mbona unamsifu. Sisi kazi yetu hapa ni kusema ukweli tu, ukifurahi tutasema ukweli, ukikasirika tutasema ukweli. Aliyekuwa mzigo wa usufi tutasema huyu mzigo wa usufi na aliyekuwa ni mfanyakazi mzuri tutasema ni mfanyakazi mzuri. Huyu mama ni mfanyakazi mzuri na kwa kwali amekuwa akituonesha dalili ya utendaji kazi kwa kweli uliotukuka.

Mhe. Naibu Spika, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu huyu mama tumpe *supporter*. Najua kwa sababu watu wamezowea ukiwasifu watu wanachukia, pengine leo watakasirika, lakini ni ukweli, usipofanya ukweli hapa duniani utafanya wapi na hapa ndio pakuchuma dhambi na thawabu.

Mhe. Naibu Spika, *CAG* huyu akiendelea kubakia kwenye madaraka kama *CAG* kwa miaka 10 tu mbele, nina hakika anaweza kujenga ofisi kama hizi hata mkoa kwa mkoa, kwa sababu ana vision ambayo inatekelezeka, sio vision ya kusadikika ambayo watu wanabuni tu kwa kudanganya. Watu wamejenga Kiwanda cha Uchapaji kwa miaka 50 ya Mapinduzi. Yeye anajenga Kiwanda cha Uchapaji na nina imani kwamba miaka miwili ijayo atakamilisha kila kitu, kwa sababu ana malengo yanayotekelezeka Mhe. Naibu Spika, *CAG* huyu.

Lakini ukurasa wa 40 kifungu 79 Mhe. Waziri ametuambia kwamba *scheme of service* ya ofisi hii tayari imekubaliwa na serikali. Mwenyekiti wa *PAC* anatuambia kwamba *sheme of service* yao imekataliwa na serikali, ni nani anatuambia ukweli. Ninavyoamini mimi ni kwamba *scheme of service* ya *CAG* serikali wanaipiga danadana, wanaona kwamba labda wanawapa maslahi makubwa. Duniani kote Mhe. Naibu Spika, ofisi kama hizi ndio ofisi ambazo zinapewa vipaumbele. Unapomuezesha Jaji na unapomuezesha *CAG* maana yake unamfanya aridhike afanye kazi kwa uadilifu na bila ya vishawishi vya rushwa. Ni nani atakayevaa kanda mbili halafu akamchunguze mtu anayevaa buti.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri atekeleze kwa vitendo *scheme of service* ya *CAG*, wala asione aibu na wala asione choyo. Hawa watu wanafanyakazi nzuri na kazi ya maana, ingawa haitekelezwi, ingawa ripoti zake hazina maana hazitekelezwi lakini yeye wajibu wake anafanya ipasavyo. Naomba Mhe. Naibu Spika, waziri kaka yangu Mhe. Dkt. Mwinyihaji *scheme* hii kwa kweli itekelezwe kwa vitendo na wapewe maslahi ambayo, ofisi za *CAG* duniani kote zinafanya utaratibu huo.

Lakini mwisho Mhe. Naibu Spika, kwa sababu mchango wangu leo sio mkubwa, namuomba Mhe. Waziri atuambie. Mwaka jana kwenye Baraza hili la Wawakilishi, wawakilishi walitoa maazimio na kuagiza serikali, kwamba *CAG* akafanye ukaguzi maalum kwa (*ZMA*), yaani *Zanzibar Maritime Authority*. Tulisema kwamba makusanyo ya usajili wa meli, watu walikuwa wakipeana kama sadaka na tukasema kwamba watu walikuwa wakisafiri hapa kwenda Dubai kwa ajili ya kula fedha tu. Taarifa ambazo tunazo sio rasmi *CAG* kazi yake imekamilika, ripoti tunataka

iletwe Barazani haraka tuione, vipi *CAG* amegundua kwa uchunguzi ule ambao *ZMA* wametafuna fedha za umma. Mimi naamini hata kama nilikuwa sijaiona, lakini naamini kwamba fedha za umma zimetafunwa.

Sasa naomba sana Dkt. Mwinyihaji waziri wangu atuambie ni lini ripoti ya *CAG* itakuja hapa, ili kugundua uchunguzi ule maalum wa matumizi ya fedha za *ZMA*, ili tujiridhishe. Je, yale maneno wawakilishi waliosema mwaka jana ni sahihi, au wawakilishi waliongopea ili Wazanzibari wapate ukweli juu ya fedha zao ambazo watu wametafuna kama sadaka.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa. *CAG* huyo huyo tulimpa kazi ya uchunguzi maalum wa viinua mgongo na mishahara ambayo watu wanatafuna. Nilisema mwaka jana hapa kwamba kuna watu waliambiwa wamekufa, kumbe wako hai na bahati nzuri hadi leo wanatuuliza bado watu wako hai. *CAG* pia akafanya kazi hiyo ya kuchunguza. Naomba ripoti hii ya viinua mgongo na mishahara hewa, Dkt. Mwinyihaji waziri wangu utuambie lini utakuja hapa ili Wazanzibari wajiridhishe basi kwamba kweli hakuna ubadhirifu wa fedha za umma, ili tuweze kuona uhalali wa utawala bora uliopo kama Mhe. Waziri alivyozungumza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mimi ni miongoni mwa watu ambao wanaamini kuwa nchi hii sio maskini kiasi hicho, umaskini wetu ni wa kujitakia, kuna watu ni makabaila, kuna watu ni makupe wanatunyonya kwa mgongo wa kujificha. Sasa namuomba Mhe. Waziri atuletee ripoti hizo tuzione, ili Wazanzibari wapate kujua uwezo wetu na mapato yetu yanavyotafunwa ili hatua zichukuliwe. Hatuwezi kuwavumilia watu ambao wanatafuna mali yetu, huku wananchi wakiendelea kula ngumu maisha magumu, huku miradi ya maendeleo ikikwama na hakuna utekelezaji.

Lakini ni kwa nini Mhe. Naibu Spika, *CAG* aweze kufanya mambo hayo mazuri, lakini serikali ishindwe kutekeleza kwa wakati. Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo siungi mkono hoja hizi mpaka pale Dkt. Mwinyihaji waziri wangu atakapotuletea taarifa au atakaponijibu kwamba ni kwa nini *CAG* hajaleta ripoti, au lini ripoti za *CAG* hizi mbili zitaletwa Barazani ili wananchi wa Zanzibar waweze kujiridhisha. Mhe. Naibu Spika, ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Mjumbe, sasa nafasi tunampa Mhe. Fatma Mbarouk Said na Mhe. Mussa Ali Hassan ajiandae na kama muda utabakia Mhe. Abdi Mosi Kombo.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi nikachangia machache kwenye hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora.

Pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa Hotuba yake ya Bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, pia nichukue fursa hii nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Ofisi za Viongozi Wakuu wa Serikali, pia nimpongeze Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Mahesabu ya Serikali.

Mhe. Naibu Spika, nikisema kwa ujumla wake kwamba tunapitisha Bajeti hii na fedha hizi ni fedha za umma kwa hivyo kuna mambo muhimu ambayo ya kuyazingatia kwenye Bajeti hii, ni ukweli usiopingika kwamba baada ya kutumia fedha hizi kwa kweli fedha hizi za umma utekelezaji wake wa matumizi ya fedha hizi kwa kweli unakuwa hauendi kama unavyotakiwa, kwa sababu fedha hizi zinahitaji zifuate Sheria za manunuzi pamoja na Sheria za fedha ni kwamba fedha hizi zinatumika kinyume cha Sheria, ndio maana pale Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu akaleta ripoti zake mbali mbali ambazo zinakuwa zinakiuka Sheria hizo.

Kwanza Wizara ni lazima ziwe na mpango kazi bila ya kuwa na mpango kazi basi utekelezaji mzuri wa Bajeti hizo kunakuwa hakuna, pia mpango wa manunuzi ni lazima uwepo ili kuleta ufanisi wa bajeti hizo, pia kunakuwa hakuna *Internalcontrol* ni kwamba fedha hizo zinatumika vibaya kama anavyoleta ripoti zake Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, pia kufunga hizabu za mwisho wa mwaka ni kweli kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Serikali anapata changamoto hizi za kuona kwamba fedha za Serikali hazitumiki kama ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, jambo ambalo nalizungumzia hapa ni kwamba bila ya kuwa na mafunzo kazi zetu hazitoweza kwenda vizuri, mafunzo ni jambo la muhimu popote pale ambapo patakuwa na kazi au patakuwa na jambo lolote ambalo ni la kutaka ufanisi basi ni lazima kuwe na mafunzo, pia uwajibikaji ni jambo la msingi sana kwa sababu bila ya uwajibikaji hatuwezi kupata ufanisi tunaotaka. Katika bajeti hii Mhe. Waziri amesema katika vifungu vyake

mbali mbali kwamba kuna ushirikiano huu wa Kimataifa katika bajeti yake hii ameelezwa na hasa kwenye ile Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa sababu kuna ushirikiano wa Kimataifa kupitia zile taasisi kuu za udhibiti na uchunguzaji wa fedha za Serikali,hili ni jambo muhimu sana kwa sababu ni lazima kuwe na ushirikiano huo wa kimataifa kwa sababu kama Zanzibar ni nchi ni lazima tujue namna gani mataifa yanaendelea au kuna mabadiliko gani kimataifa basi na sisi tunatakiwa kwamba tuwe tunakwenda sambamba nao. Kwa hivyo ni lazima ushirikiano wa Kimataifa uwepo.

Mhe. Waziri amesema kuna kamisheni ya Kiswahili ya jumuiya ya Afrika ya Mashariki ambayo itaanzishwa, lakini vile vile niseme ni lazima tuwe na uwajibikaji ili tulete ufanisi kwa sababu tumezoea kwamba baada ya kupata heshima hii sijui kwa nini baada ya muda taasisi hizi zinakuwa sio endelevu, kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, niombe Serikali inapopata heshima hii basi tulinde heshima ile tunayoipata.

Mhe. Naibu Spika, rushwa ni adui wa haki na panapokuwa na rushwa basi lazima kutakuwa na uhujumu wa uchumi, nikienda kwenye Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama alivyosema Mwenyekiti wangu kwamba Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni taasisi muhimu na haiwezekani kwamba taasisi hii ya ukaguzi ikawa kweli yenyewe wafanyakazi wake hawana maslahi, anapokwenda kumkagua mtu ambaye yeye mwenyewe anayekwenda kukaguliwa ana uwezo mkubwa hebu niulize Mhe. Naibu Spika, hebu nambie kwamba wewe unakwenda kumkagua mtu ambaye uwezo wake ni mkubwa kinachoendelea ni nini. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, niombe kwamba ile *schemeofservice* ile ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali basi izingatiwe na iweze kupitishwa.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze sana *CAG* kwa ujenzi wa ofisi yake Pemba kwa kweli hapa inaonekana uwajibikaji wake na kwa sababu ni mtu ambaye anazingatia utawala bora na ile misingi yake ambayo ni misingi ya utawala bora moja ni uwajibikaji na pia na uwazi, hapa Mhe. Waziri amesema kwamba kwenye Ofisi hii ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hapa kidogo inanipa utata kwenye ukurasa wa 39 kifungu 77. Mhe. Waziri amesema Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imekamilisha matengenezo makubwa ya jengo la Ofisi hiyo iliyopo Pemba kwa asilimia 99, mapendekezo hayo yanaendana na vigezo vinavyotakiwa kwa mujibu wa sheria ya usalama na afya kazini.

Hebu Mhe. Spika, utakapokuja Mhe. Waziri aniambie tofauti ya matengenezo na ujenzi, kwa sababu yeye hapa anatwambia amekamilisha mantengenezo na mimi ninavyojua kwamba lile jengo limejengwa limeanzishwa tokea msingi na kwenda juu, kwa hivyo Mhe. Waziri atakapokuja anipe tofauti ya matengenezo na ujenzi.

Mhe. Naibu Spika, kama walivyosema wenzangu kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anahitaji kupongezwa, anakumbana na changamoto nyingi na ni ukweli kwamba kwa sababu ni mtendaji wa kazi hodari na kwa sababu ni mwanamke mwenzangu niseme kwamba nampongeza sana na wala asife moyo kwa hizo changamoto anazozipata, kwa sababu ukiwa muwajibikaji na ukakumbana na watu ambao hawataki uwajibikaji basi kwako wewe itakuwa ni tatizo, kwa hivyo akamate kamba hiyo hiyo ajitahidi na kwa sababu ni muwazi na mkweli changamoto hizo zitampata tena ni mwanamke ni jasiri kama ni kupewa nishani basi na yeye apewe, kwa sababu changamoto zote zilizokuwepo sasa hivi makero katika makero yaliyokuwepo moja ni Afisi hii ya *CAG* kwamba *CAG* mpaka hii leo kwa kweli anapata changamoto katika kero moja ya Muungano basi moja ni hiyo ilikuwa kwamba yeye mwenyewe zinamkumba changamoto hizi lakini hakuchoka hapo na wala hakukomea hapo, na wengine wangekuwa na msimamo kama wake yeye basi nchi hii tusingelia makero kwa sababu alikuwa hatambulikani kimataifa lakini kahangaika huku na kule lakini mpaka hii leo amepata nafasi hiyo anahangaika kutafuta nafasi mbali mbali za mafunzo pamoja na sisi Kamati yangu ya *PAC* pia niseme kwamba yeye ndiye anayetuwezesha, ndio mdau wetu mkubwa na tunamshukuru tuko nae pamoja.

Kwa hivyo kahangaika sehemu mbali mbali kututafutia na sisi mafunzo kwa kwenda kubadilishana uzoefu na kamati zile za *PAC*, ili tuende sambamba na wenzetu, na wala hakujali hilo na ni fahari kubwa tena sisi tunajidharau sisi wenyewe lakini kuna ripoti ambazo zinapelekwa kimatifa na zinasomeka na zikakubalika na wenzetu wakaja kusoma kwao, kwa hivyo mimi niseme kwamba afsa *CAG* ni mtu jasiri ni mwanamke mwenzangu na ingekuwa kuna [wanawake au wafanyakazi au sisi watendaji tungekuwa kama yeye basi nchi hii tungepiga hatua kubwa.

Mhe. Naibu Spika, nisisitize tena kwenye hili la kuzisimamia bajeti zetu kisheria kwa kufuata zile sheria za manunuzi, pia kwenye ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu mapungufu ambayo yanaonekana ni kwamba *fixed asset*

register zinakuwa hazipo ingawaje na Wizara ya Fedha wametoa huo mfumo wa kuwa na *fixed asset register* ambayo itakuwa inaratibu zile mali za Serikali. Na kutokuwepo *fixed asset register* kwa kweli inakuwa ni matatizo ingawaje bado tatizo lipo na hili ni lazima tulitafutie ufafanuzi ni lazima zile mali pia ziwe na *value* ingawaje kuna ukosefu wa *value* hatuna lakini vile vile hili jambo ambalo Serikali pia iliangalie, kwamba Serikali itakuwa haiwezi kufunga hesabu zake za mwaka ikiwa thamani ya mali zenyewe hazipo kwa hivyo nipongeze Serikali kwa ujumla kwa kuanzisha na hasa Wizara ya Fedha hiyo *fixed asset register.*

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuyazungumza hayo kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Amani walionichagua kwa wingi naomba kuunga mkono hotuba hii na pale Mhe. Waziri atakapokuja kunambia au kunipa ufafanuzi wa ujenzi na matengenezo. Naomba kuunga mkono. (*Makofi*).

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuweza kunipa nafasi kuchangia Wizara hii ya Ofisi ya Rais Ikulu, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kutupa nafasi ya kufika hapa tukawa salama ili kuweza kuchangia masuala yetu yote ya mambo ya bajeti hii ya Ofisi ya Rais Ikulu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri kwa mengi aliyoyaandika humu hasa sehemu kubwa ya kuweza kuzuia rushwa, kwa kweli nchi yetu hivi sasa imejaa na rushwa hasa kwa sehemu ya vitengo muhimu ambavyo ni tegemeo kwa Serikali, sehemu nyingi ambazo vipaumbele vya Serikali hivi sasa havina maendeleo ya kutosha kwa sababu sehemu kubwa imedhibitiwa na rushwa, kwa kweli sehemu nyingi ambazo Serikali imewekeza ili iwe na maendeleo lakini maendeleo hayo kwa muda wote yamekuwa finyu sana kwa kudhibitiwa na watu ambao wanapokea rushwa katika sehemu hizo za kazi. Na utakuta badala ya sehemu iingize fedha nyingi sana lakini utakuta sehemu nyingi sana zinatoa fedha kidogo kwa sababu watendaji wake wanapokea rushwa na kuisababisha Serikali kukosa mapato muda mwingi sana na kukosa maendeleo ya wananchi kwa muda ambao yanahitajika.

Tukiangalia hivi sasa tumeweka kitengo cha kudhibiti rushwa lakini utakuta kitengo hiki sijapata hasa kuhakikisha kwamba imeweza kudhibiti matokeo mabaya ambayo yanafanyika ndani ya Serikali, utakuta sehemu nyingi za matajiri wanapitisha maendeleo yao ya binafsi ni makubwa sana kuliko masuala ambayo yanapatikana kwenye Serikali, na tunasubiri sana kuona Serikali ipate maendeleo ili wananchi wahakikishe kwamba wanafanikiwa kupata maenedeleo yao hasa kutokana na mishahara bora lakini utakuta wananchi binafsi, matajiri ndio waliokamata hatamu ya kuweza kupata fedha kuliko Serikali yenyewe.

Kwa kweli ningelishauri Ofisi ya Rais Ikulu ingelifanya mabadiliko katika sehemu zake nyingi zikawa sehemu hizo watu wake wasikae kwa muda mrefu sehemu moja hiyo ndiyo inayosababisha kwamba sehemu nyingi ziwe na rushwa, kwa sababu wale watendaji wake wameshazoea kukaa katika sehemu na kuzoeya mapato hadi kufikia kwamba ukifika pale unakwenda kwa mtu fulani, lakini ingelikuwa kila baada ya miezi sita au mwaka mmoja ikawa inafanywa change lakini utakuta watu wake hawabadiliki tokea miaka hiyo ni watu hao hao sasa utakuta rushwa imeshazoeleka na haiwezi kung'oleka kirahisi.Ningelipendekeza Mhe. Waziri akija anihakikishie kwamba mwaka huu wa fedha watu wa sehemu nyingi ambao wameweza kubadilishwa ili kuweka mtandao wetu katika hali nzuri ya kibiashara.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa niendelee ukurasa 31 kuhusu Wazanzibar walioko nje ambao *dispora*kwa kweli hivi sasa Wazanzibari wengi wako nje na wanaleta maendeleo hapa Zanzibar. Lakini Mhe. Waziri, hajatueleza hivi sasa kuna Wazanzibari wangapi nchi za nje ambao wanasaidia sana Zanzibar kuleta misaada, kipindi kilichopita alituhakikishia Wazanzibari wangapi ambao wapo nje ambao wanaisaidia Zanzibar lakini kwa kipindi hiki naona kwenye kitabu chake hakutuhakikishia kwamba kuna Wazanzibari wangapi ambao wanaleta maendeleo kwao hasa katika maendeleo ya mashule na mambo mengine kama kompyuta.

Tumesikia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alienda nje ameleta sana vyombo kama hivyo ma-*computer* na mambo mengine, lakini sikujua ma-*computer* yale hayakutolewa na wazanzibari walioko nje ambao tulipata msaada tu kutoka nchi za nje lakini hatukuhakikisha kama misaada ile wameleta ndugu zetu ama wenetu walioko nchi za nje. Ninamuomba Mhe. Waziri akija anihakikishie hivi sasa kuna wazanzibari wangapi ambao wanaleta misaada ya kusaidia kwao kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu ama kwa ndugu zao wa hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo niendelee katika ukurasa namba 20 Ofisi ya Rais Ikulu, kuhusu majumba yetu ya Ikulu ambayo ni mapumziko ya wageni yaliyoko nje ya Zanzibar. Kwa kweli majengo ya Ikulu zetu hivi

yamekuwa machafu sana na sifikirii kama wageni wanafikia katika maeneo hayo hasa ukitizama Ikulu yetu iliyopo pale sehemu za Mtoni KMKM pale ile Ikulu sifikirii kama hata Rais hivi sasa hivi anafikiria kwenda kupumzika pale. Kwa sababu imepauka, imeingiliwa na majenzi ya watu binafsi ambao si tena kusema kwamba ni Ikulu ambayo inawezekana ikatembelewa na wageni kutoka nje.

Mhe. Naibu Spika, sehemu hizi za kujenga Ikulu ni muhimu sana, kwamba Rais wetu ama wageni wetu wakubwa wanapokuja katika nchi yetu, si vizuri kwamba wafikie katika mahoteli ya kitalii. Kila Mkoa ni vizuri kwamba tuhakikishe kuna sehemu ya mapumziko ya Ikulu ya Rais, lakini utakuta Mkoa wa Kusini kwa muda mrefu hivi sasa Ikulu yake sijaiona kama ipo. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze ni lini tutajengewa Ikulu mpya katika Mkoa wetu wa Kusini ili kuhakikisha Rais anapokuja katika Mkoa wetu, hawezi kufikia katika hoteli au kuomba msaada kwenye nyumba za wageni ili tusaidiwe pa kumuweka Rais wetu ama mgeni mashuhuri kutoka nchi za nje.

Kwa kweli Ikulu nyingi hivi sasa hazijakarabatiwa, kuna Ikulu ile ya Kaskazini, Mkokotoni sifikirii hata kama muuza dagaa ukimuweka atajihisi kama yuko Ikulu. Kwa kweli ile Ikulu Mhe. Waziri inatengewa pesa nyingi lakini sijaiona usafi wake. Nilipokwenda kuitembelea mimi niliikuta kwa kweli Ikulu hairidhishi na haina thamani ya kuitwa Ikulu. Kama kwa kweli fedha zote anazopewa ni afadhali ibadilishwe iwe na majengo mapya ile Ikulu ya zamani iwekewe kitengo chengine na isiwe Ikulu kwa vile haiwezi kurekebishika ni afadhali ijengwe Ikulu mpya hivyo tuhakikishe kwamba tuna nyumba ya kileo ambayo anaweza kufika Rais wetu akapata mapumziko.

Lakini hata huko Kaskazini hivi sasa anapokwenda mara nyingi anafikia katika mahoteli ya wageni wa kawaida na hiyo si jambo zuri la kuhakikisha kwamba tuna Ikulu ambayo inatajika.

Kwa kweli kuhusu *CAG* wetu ukurasa namba 38 kwa kweli *CAG* ana sifa za kila aina jinsi anavyofanya kazi zake katika nchi yetu. Na tungelikuwa na mwanamama kama huyu ambaye anajituma hana tamaaa tungelihakikisha kwamba tunaye *CAG* ambaye Mkaguzi ano uhakika wa kazi zake pamoja na ofisi zake. Kwa kweli nimeona majengo yake ambayo amechukua dhamana mwenyewe amejenga ambayo ni ya kisasa si wizara nyingi ambazo zimehakikisha kuwa na majengo ya kileo. Wengi Wizara zao zilikuwa na majengo ya kurithi ama ya kuazimwa, lakini *CAG* amehakikisha majengo mawili ya kisasa ambayo yanatokana na Wizara yake mwenyewe kusimamia na yeye anakwenda kusoma katika nchi nyengine za nje.

Kwa ushauri wangu sisi ambao tunamkaribia sana *CAG* aendelee kuomba nafasi katika nchi za nje na isiwe Wizara moja tu ambayo kuipeleka kwenda kupata masomo ambayo ndugu zetu wa *Press* ni afadhali kwamba kila section achukuwe vitengo vyote vyende kuhakikisha kwamba kupata ujuzi nchi za wenzetu kuhakikisha Zanzibar imepata wakaguzi wazuri ambao wanatoka katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na muda ulivyokuwa ni mdogo sana na wenzangu wanataka kuchangia nafasi hii, nasisitiza Mhe. Waziri atakapokuja atuhakikishie kwamba Ikulu zetu ambazo tunazitaja hivi sasa zaidi ya hii Ikulu kubwa zihakikishe zinafanyiwa ukarabati wa kileo na nyingi zake ziwe za ghorofa zisiwe zile za chini. Ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi nishukuru kupata fursa hii adhimu kuweza kuongea hotuba hii ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora. Mheshimiwa nitajitahidi kwenda haraka haraka ili niweze kupata muda wa kutosha muda uliobakia kwa sababu sina mambo mengi leo na sababu kwamba sina mambo mengi hii ni Ofisi nyeti Ofisi muhimu na tuna haja ya kumtunza kiongozi wetu mkuu wa nchi hii kama nilivyokuwa nikipiga kelele jana kumtunza kiongozi wetu mwengine na leo ninafikiri hili pia naweza kulipigia kelele zaidi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nataka nizungumzie katika suala la Idara ya Ushirikiaono wa Uratibu Diaspora. Mheshimiwa, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri kuwajengea uwezo zaidi hii Idara. Kwa sababu hii Idara ni muhimu kuna Wazanzibari wengi ambao wanaishi nje ya nchi wana uwezo sio uwezo wa kifedha tu hata uwezo wakitaaluma. Sasa ni vyema tukaijengea uwezo ili hawa maafisa wakaweza kutoka zaidi katika dunia kuweza kuitangaza hii Idara na kuweza kueleweka na kuweza kufika Zanzibar wale ndugu zetu ambao wanaishi nje na kuweza kutusaidia katika mambo mbali mbali.

Lakini katika Idara hii Mhe. Waziri, utakumbuka mwaka juzi waliwahi kuombewa kufanyiwa utaratibu wa kuweza kuondoka mle katika jengo Ikulu ili wawe na Ofisi yao *independence* nje kabisa ili waweze kufanya kazi zao kwa

ufanisi zaidi. Sasa Mhe. Waziri atakapokuja anijibu kwamba hili agizo ambalo lilitolewa na Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Kamati iliyopita kama imeshafanyiwa kazi ama bado na kama halijafanyiwa kazi sababu gani za msingi ambazo hazijaweza kufanyiwa kazi.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ambacho nilitaka kizungumzie ni katika hii taasisi ya *CAG* wengi wamezungumzia Mhe. Naibu Spika, na tutaendelea kuzungumzia kutokana na umuhimu wake. Mheshimiwa juzi nilipokuwa nikichangia katika Tume ya Uchaguzi nilizungumza lazima tukiri kwamba kuna nafasi zinakuwa ni nyeti na juzi niliiomba serikali kuangalia namna ya kuwasaidia kuwaongezea uwezo wa kimapato wafanyakazi wa Tume ya Uchaguzi ili waweze kufanya kazi yao kwa ufanisi na kujiamini na kutokuahadaika na mambo mengine.

Sasa leo narejea tena Mhe. Naibu Spika, kuiomba serikali kutafuta namna ya kuweza kuwazidishia uwezo wa kimapato watendaji wetu wa *CAG*. Mheshimiwa kuna maeneo kama hatukuyajengea uwezo basi yanakuwa ni hatari katika utendaji wao wa kazi. Na sote tunafahamu kwamba maeneo mengi mfano *ZRB*, *TRA*, Mabenki, wafanyakazi wake wanakuwa tofauti na wafanyakazi wa kawaida katika taasisi nyengine, kutokana na usiri au kutokana na hali halisi ya kazi zao ambao wanazifanya kila siku. Vyenginevyo Mhe. Naibu Spika, tutapelekea ushawishi kwa vijana wetu watashindwa kufanyakazi kwa uadilifu na hatimae yale matarajio tunayotegemea yasiweze kufanikiwa.

Mhe. Naibu Spika, sehemu nyengine ambayo ninataka niizungumzie ni sehemu ya *GSO*. Mheshimiwa hii taasisi ni muhimu kwa nchi yetu kwa sababu usipomfanyia mfanyakazi *vetting* kuna hatari na hasara yake, kwa sababu kuna maeneo ni nyeti, sasa usipojua hali halisi ya mfanyakazi kwa sababu wengi wetu wanafikiria labda tunawaangalia wafanyakazi wale katika mambo ya kawaida tu lakini wakati mwengine wanafanyiwa *vating* hata kujua uwezo wao wa zamani katika hali zao za kiafya. Wengine wanaugua wazimu nyuma huko hatuwezi kujua na tunawapeleka katika taasisi nyeti hili suala ni hatari.

Sasa nimuombe Mhe. Waziri mimi nina mashaka kwamba pana tatizo katika kitengo cha *GSO* kutokutoa ushirikiano kwa mawizara kwa *GSO* na kupelekea baadhi ya Taasisi kuajiri pasipo na watu kuwapeleka *GSO*. Sasa mimi nafikiri kuna haja ya kuwapa meno kwa wale watu ambao wanaajiriwa pasipo na kufatwa utaratibu wa kisheria katika kupita katika hiki kitengo cha *GSO*.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo nataka nilizungumzie kabla sijaingia kwenye kitabu cha bajeti hiki katika ukurasa wa 13 kifungu cha 21 utunzaji na matengenezo ya Ikulu ndogo ndogo Kibweni. Mheshimiwa aliyekaa hapa yeye alijaribu kuchangia kwa namna yake na kila mtu anakuwa na uoni wake, mimi niko tofauti zaidi na yeye. Kwa sababu mimi kabla sijaja hii Kamati ya Wanawake na Watoto, nilikuwa katika Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa na nilijaribu kuzitembelea Ikulu zote za Zanzibar. Tumeanza na Mnazimmoja, tukenda Fumba, tukaja Kibweni, tukenda Mkokotoni, tukenda Dodoma, tukamalizia na Dar es Salaam. Na nitoe pongezi za kutosha kwa Ofisi ya Rais Ikulu kwa namna walivyoanzisha utaratibu wa kuyaenzi haya majengo. Na ndio maana nitakuwa kidogo nitakuwa tofauti na mwenzangu.

Mhe. Naibu Spika, kitengo cha kuamua kuwa na mtaalam ndani ya taasisi nzito kama ile ni kitendo cha kupigiwa mfano kwa nchi yetu. Ninajua kwamba tumemuweka injinia mzoefu nilikuwa nikihangaika kutafuta jina lake pale, kuna mwenzetu yule mwenye asili ya kiasia kama sikosei Ndugu Mohammed, ni kijana ambaye anasimamia vizuri majengo na majengo kila siku yanakuwa yapo katika mazingira mazuri.

Ninachokiomba Mhe. Waziri ni kumjengea uwezo wa kifedha kwa sababu *the same time* anaweza akataka jambo la haraka kurekebisha na kukawa kuna mapungufu. Katika ziara hiyo Mhe. Naibu Spika, tulipata tatizo la ile Ikulu ya Mkokotoni, kulikuwa kuna tatizo la uzio na katika kipindi kile ambacho mimi niko katika Kamati Mhe. Naibu Spika, tulitoa agizo la kujenga uzio ili kuondosha usumbufu wa kupita katika lile eneo. Lakini lile jengo limeshafanyiwa ukarabati, ukarabati kidogo unaridhisha kwa kufikia mgeni kwa hatua za dharura ili kiongozi wetu anapotembea katika ule Mkoa kwa ajili ya mapumziko. Kwa sababu yale ni maeneo ya mapumziko wakati kiongozi anatembelea katika ile Mikoa. Sasa kulikuwa kuna tatizo la uzio tu, sasa Mhe.Waziri atakapokuja hapa atanijibu kwamba labda ule uzio tangu miaka ile miwili ya nyuma ambapo tangu mimi niko kwenye Kamati kwamba limeshafanyiwa kazi au kama bado na sababu za msingi kama bado hazijafanyiwa kazi atakuja kunielewesha.

Mheshimiwa sababu ya kusema hivyo, tulipata tabu sana na tukauliza sana katika jengo la Ikulu la Kibweni. Mheshimiwa lile jengo zuri sana na lile jengo limejengwa katika miaka ya nyuma ya kifalme linavutia, ndani lina

raha ukitoka nje kuna *beach*. Sasa moja ambalo walipiga kelele wataalam kwamba linakosa kukaliwa, unapolifanyia ukarabati, nyumba yoyote kama haikaliwi inachukua muda mfupi kuchakaa. Sasa serikali imekuwa inatumia gharama ya pesa kufanya ukarabati lakini makaazi hata ya dharura hakuna, sasa jana Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa nikichangia hapa tulipata tatizo kubwa la nyumba kwa viongozi wetu wakuu. Sasa nikaambiwa kwamba nyumba iliyotafutwa kwa kiongozi wetu mkuu Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais kwamba serikali ilikaa na ikatoa maamuzi hayo.

Sasa niombe basi serikali ikakae tena ifikirie na iwaze kama kuna haja au kama lile jengo basi halijapata mkaazi kwa kunusuru fedha za walipa kodi, kwa kunusu kukodi nyumba vichochoroni pasipokuwa na utaratibu mzuri na kupoteza gharama ambazo wananchi wanazihitaji. Mhe. Naibu Spika, nchi hii ina matatizo mengi tukenda hospitali matatizo yamejaa, tukija katika Mamlaka ya Maji matatizo yamejaa, lakini ninahisi kuna haja ya kutumia mapato yetu pasipokuwa na utaratibu wa msingi pia tunakuwa tunapoteza muelekeo uliokuwa si mzuri.

Sasa niombe Mhe. Naibu Spika, serikali hebu ikae wakamshauri Rais lile jengo zuri ambalo pale limekaa kwa haiba na lina nafasi ambalo limekaliwa na Wafalme tangu asili na asili basi huyu kiongozi wetu akawekwe pale ili apumzike ili kupunguza gharama zilizokuwa hazina msingi kwa kukodi majumba nje katika maeneo ya mitaani.

Mhe. Naibu Spika, sasa naingia kwenye kitabu kidogo tu kwa haraka haraka kwa ku-*save* muda wako dakika tatu tu. Mheshimiwa ukurasa 67 kifungu 22020. Mheshimiwa ninapata mashaka kifungu hiki kimepunguziwa bajeti na hii taasisi nyeti ina mambo muhimu sasa nina hofu tusije tukawapunguzia bajeti tukaja tukapata wageni matokeo yake tukaja tukaaibika, nipewe sababu za msingi za kupunguza bajeti hii katika Ofisi ya Rais Ikulu.

Mheshimiwa, kifungu chengine ambacho nilitaka nikizungumzie kwa haraka haraka ni ukurasa wa 86. Mheshimiwa ukurasa wa 86 katika kifungu 220501 *stationary suppliers* na vifaa vya kuandikia Mheshimiwa, mwaka jana walitengewa milioni 24,883,000 mwaka huu mara mbili zaidi ya bajeti, sababu za msingi vifaa vya kuandikia hata hesabu ikawa kubwa sana kiasi hiki. Nielezwe tukaweka bajeti kubwa kiasi hiki, karibuni tumeweka milioni 44,525,000, Mhe. Waziri atapokuja atanisaidia lakini katika ukurasa huo huo wa 86 Mheshimiwa matengenezo madogo 220700 Mheshimiwa mwaka jana walitengewa milioni 30,000,000 mwaka huu milioni 50,000,000.

Kwanza Mhe. Naibu Spika, napata tabu katika hiki kitabu, atakapokuja hebu anisaidie tofauti ya matengenezo makubwa ya majengo na tofauti ya matengenezo madogo madogo. Kwa sababu humu humu katika katika kitabu hiki hiki Naibu Spika, kuna Wizara nimeangalia milioni 20,000,000 imewekwa katika matengenezo makubwa. Lakini milioni 50,000,000 zimewekwa katika matengenezo madogo madogo. Halafu pia napata tabu mwaka jana walitengewa milioni 110,000,000. Sasa sijui kama wamezitumia katika matengenezo makubwa, na kama wamezitumia mwaka jana walipata hizi fedha kama walitengeneza, iweje mwaka jana walichukua pesa hizi na mwaka huu wachukue pesa karibuni nusu ya zile kufanya matengenezo madogo madogo.

Mheshimiwa kama kakaguliwa mwaka jana mwaka huu wanataka wafanye matengenezo mengine watatueleza.

Namalizia kifungu cha Mheshimiwa katika ukurasa wa 88 Kitengo cha Ofisi ya Usalama GSO. Mheshimiwa kifungu 220401 Petroli. Mheshimiwa fungu limepunguzwa kutoka mwaka jana milioni 20,700,000 mwaka huu milioni 18,000,000. Sasa ninapata tabu Mhe. Naibu Spika, kwamba gharama za mafuta bei zinapanda lakini mahitaji kwenye mawizara yanapunguzwa, sasa sijui kitu gani. Sasa na hiki kitengo Mheshimiwa kimepiga kelele sana kama kinashindwa kufanya kazi kufatilia kazi za nje, kwa sababu kazi hawana, uwezo wa mafuta mdogo, sasa leo baada ya kuwaongezea ili waweze kufanyakazi kwa ufanisi tunazidi kuwapunguzia ili hizi kazi zao wazifanye kwa ufanisi huo, halafu baadae tufike pahala tuwalaumu kwamba GSO hawafanyi kazi kumbe sisi wenyewe hatujawa tayari kuwasaidia kuweza kuwapa nguvu za kuweza kufanya kazi.

Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru ninaunga mkono hoja. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Niwashukuru kwa ushirikiano wenu tangu asubuhi hadi hivi sasa na naomba niwataje wataoanza kuchangia kipindi cha jioni na sote kwa jumla tujali muda bado tunachelewa. Kwa hivyo wa mwanzo jioni ataanza kuchangia Mhe. Abdi Mosi Kombo, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Wanu Hafidh Ameir na Farida Amour Mohammed. Wajitahidi kuja mapema ili tuweze kuchangia.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Ahsante Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya mwanzo jioni hii na mimi kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu.
Mhe. Mwenyekiti, mimi nikianza mchango wangu naanza katika ukurasa wa 5, ibara ya 9, *iterm* ya kwanza naomba kunukuu.

"Kuimarika kwa huduma bora kwa wananchi, kuwa na mipango endelevu ya maendeleo inayolenga kukuza uchumi na kupunguza umasikini, kuimarisha kwa maendeleo ya Zanzibar".

Mhe. Mwenyekiti, nikianza kutoa huduma za wananchi kwa jamii, kwanza kuna huduma ya afya, maji, barabara, elimu, ajira, biashara na mengineyo. Mhe. Mwenyekiti, afya tunayo lakini ninaiomba Serikali kwamba hivi sasa wananchi wengi wa Zanzibar bado wangali masikini sana kulinganisha na kipato chao cha kutwa. Kwa hivyo, kutokana na huduma za afya wakati mwengine wananchi wanaweza wakaenda hospitali wakaandikiwa madawa lakini ikawa hawana uwezo nayo. Kwa hiyo,naiomba Serikali vile vile ifikirie huduma za wananchi juu ya afya ambao waliokuwa hawana uwezo hata wakununua madawa, kuwafanyia tahafifu ya madawa katika hospitali zetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika huduma ya barabara kuna baadhi ya sehemu za Zanzibar bado huduma za barabara ziko duni sana hususan ukichukua sehemu zetu za Kaskazini kwengine hazijafika barabara, kwengine barabara mbovu kwa hivyo barabara hizo zitakuwa zinaleta upungufu hasa kwa huduma za wananchi kufika katika sehemu zile ambazo wanazohitaji, na hata uchumi unakuwa mfupi sana kwa wananchi hao kutokana na huduma hizo.

Tukiendelea katika huduma za ajira, Mhe. Mwenyekiti huduma za ajira katika nchi yetu bado zingali zina matatizo, vijana wengi wanasoma, wanamaliza kusoma lakini tatizo kubwa ni ajira. Kwa hivyo, naiomba Serikali ijapokuwa hakuna ajira za Serikali lakini ifanye mpango Serikali iwape ujasiriamali ambao wataendelea vijana hao kujiajiri ndani ya sehemu zao na ndani ya vikundi vyao.

Mhe. Mwenyekiti, nikimaliza katika huduma za wananchi na za kijamii nakwenda katika ukurasa wa 35 ibara ya 66 mamlaka ya kuzuia rushwa.

Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu ya Zanzibar imepea sana kwa mtindo wa rushwa, lakini ningelimuomba Mhe. Waziri aje atueleze ni sababu gani au ni watu gani hasa Zanzibar wanaosababisha rushwa katika nchi yetu. Kwa sababu ukienda kutaka ajira hupati kama hujatoa rushwa, ukienda katika vyombo vyengine ambavyo vya msaada hupati bila ya rushwa. Sasa namuomba Mhe. Waziri aje atueleze hasa kipi kinachosababisha rushwa katika nchi yetu ambacho mpaka hivi sasa tunalalamika kila unapokwenda rushwa, rushwa, rushwa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri labda atakuja kutueleza kipi ambacho kinasababisha rushwa katika nchi yetu hata maendeleo yanakuwa yanakwama kwa kitendo hiki cha rushwa, kimepea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi bila ya kupoteza wakati ili niwape wenzangu waendelee na mchango naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu. Ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai tukaweza kukutana jioni hii hapa. Lakini pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia na mimi nafasi yakuweza kuchangia matatu.

Mhe. Mwenyekiti, pia shukurani zangu nizipeleke kwa Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kutuletea hotuba hii ya bajeti ya mwaka 2014/15.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze mchango wangu katika ukurasa wa 26 ambapo kwenye Idara ya Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nisisitize kwa sababu hili jambo tunalizungumza kwa muda mrefu lakini bado inaonekana hatua hasa madhubuti za utawala bora hazijachukuliwa. Bado katika ofisi zetu hakuoneshi juhudi kubwa za kuonekana tunaufikia huo utawala Bora. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka nihimize pamoja na mipango mizuri ya Serikali inaonekana katika kitabu hiki, lakini bado nisisitize kihuduma hatujaufikia utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Mradi wa Uimarishaji wa Nyumba za Viongozi na Nyumba za Serikali. Mhe. Mwenyekiti, mradi huu ni muhimu sana, lakini niiombe Serikali iongeze jitihada za kuendeleza mradi huu kwani Serikali huwa inaziacha nyumba hizi muda mrefu bila ya kuzikarabati.

Mhe. Mwenyekiti, nyumba hizi zinapoachwa muda mwingi bila ya kufanyiwa ukarabati ndipo sasa Serikali inapokuja kujikuta ina gharama kubwa ya kuweza kushughulikia na majengo ni mengi inakuta sasa ule utekelezaji unakuwa dhaifu. Lakini ingekuwa Serikali inajiweka imara kwa kufanya ukarabati wa mara kwa mara hizi nyumba zisingewahi kufikia matengenezo makubwa au kuweza kujengwa upya kabisa wakati tunazishughulikia mara kwa mara.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu waliochangia walisema kama kweli nyumba za Ikulu ziweze kujengwa vizuri na wengine walipendekeza hata zijengwe za ghorofa si vibaya kwa sasa kwa sababu ardhi ya sasa hivi tuliyonayo huwezi kujenga majengo yanayoenda chini kwa sababu ya ku-*save* nafasi.

Mhe. Mwenyekiti, kweli nyumba za Ikulu zipo lakini utakuta hadhi yake haziendani na hadhi ile ya kuziita nyumba za Ikulu. Kwa hiyo, bado mimi niiombe Serikali iendelee kujenga majengo yenye hadhi na yanayokwenda na wakati.

Lakini pia niisisitize Serikali kwa kweli hatupendezewi kuona Serikali inakodi nyumba za viongozi, jambo hili halipendezi ingepaswa Serikali kujenga nyumba za viongozi wake ambazo zitakuwa na hadhi ya wale viongozi, kuliko Serikali kukodi nyumba ambapo zinagharimu gharama kubwa zaidi na ingeweza kufanyia mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Ikulu ya Mkokotoni wenzangu walizungumza na mimi nataka nisisitize kumwambia Mhe. Waziri uzio wa Mkokotoni ni muda mwingi mimi nikichangia bajeti nilikuwa nikisisitiza kwa sababu pale ni Ikulu na wanakuja viongozi mbali mbali, lakini mazingira yaliyopo pale kwa kweli mimi hata na wengine ambao wanaijua sehemu ya Ikulu itakuwa hayawavutii.

Mhe. Mwenyekiti, pale kunafungwa ng'ombe, watu wanakuja kuchunga mbuzi imekuwa kama siyo eneo la Ikulu. Kwa hiyo, tungeiomba Serikali kama haijawa na ule mpango madhubuti wakuwa una fedha za kutosha basi wangeweka angalau uzio ule utakaokuwa wa unafuu japo wa senyenge, lakini ikaonekane ile sehemu iko katika udhibiti kuliko kwamba eneo lile wanaingia kila mtu na pale wanakuja viongozi pia kiusalama lile eneo linapenda lihifadhiwe.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 38 ambapo kuna Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu kwa kuanza walimpongeza sana na mimi bila ya kuchelea niseme naunga mkono wenzangu waliompongeza na mimi naendelea kumpongeza Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa juhudi na kazi zake anazozifanya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi tu niombe zile taasisi nyengine kwa sababu ninavyokumbuka kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali huwa kuna changamoto ya kuziwasilisha zile hesabu ili na yeye akaweza kufanya kazi zake kwa wakati. Kwa hiyo, niwakumbushe tu watu wa taasisi mbali mbali waweze kufanya kazi kwa kuwasilisha zile hesabu ili na Mkaguzi na yeye aweze kufanya kazi zake kwa wakati na kuweza kumjengea sifa zaidi. Na pia nimpe hongera kwa jengo jipya la Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna *scheme of service* katika ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama mwenyewe ulivyoieleza katika kitabu na mimi nisisitize ni kweli ni haki yao na wao waweze kushughulikiwa ili *scheme of service* iweze kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Tume ya Mipango. Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Mipango ndiyo chombo cha juu cha kutayarisha, kuratibu na kutekeleza mipango ya kiuchumi na kijamii nchini. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli maneno haya na mimi nataka nijuulishwe kwa sababu wanaona miradi mingi ya Serikali ambayo yote huwa ina lengo la kupeleka maendeleo kwa jamii. Lakini niseme ni kwa nini wakati Tume hii ipo imeonesha katika kitabu hapa na wajumbe wanaoshughulika na Tume.

Lakini huona kwamba hakuzingatiwi wakati wa upangaji wa miradi ya kimaendeleo kwamba watu wakakaa na kupanga ili tunapopeleka mradi huu basi tuhakikishe hatuathiri ule mradi mwengine. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tukishuhudia fedha nyingi za Serikali zinatumika kwa kutekeleza mradi mmoja na hatimae mradi huo unaathiri mradi mwengine na wakati nao unakuwa umetumia fedha nyingi vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, nitoe mfano kama miradi ya barabara, miradi ya barabara inachukua fedha nyingi kusema kweli, lakini kama kutakuwa hakuna mpango endelevu wakuona labda Wizara ya Ardhi ambayo inashughulika na mambo ya utiaji wa mabomba ya maji ikazingatia kabla ya kufikia kujengwa ile barabara wao wakaweza kupitisha mabomba yao pale ili itakapokuja barabara isiweze kuvunjwa barabara ile wakati imejengwa kwa gharama kubwa. Naona ingeweza kusaidia na ingeweza kuokoa fedha za Serikali. Kwa sababu utakuta barabara imeshajengwa kwa gharama kubwa na imeshatiwa mpaka lami halafu panakuja kuvunjwa. Kusema kweli hii inatia uchungu sana na naomba sana katika mipango basi hata huu mpango wa barabara zetu naomba kuwe na utaratibu au sheria maalum pia itungwe ambayo itaweza kuzihifadhi barabara kuona hazifanyiwi uharibifu wa makusudi. Kwa sababu mtu anaona tu barabara ipo basi anaweza akaleta kitu kigumu akavunja katika barabara bila ya kujali kama hapa labda kumejengwa kwa fedha nyingi za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, pia tuliona mkongo wa Taifa ule ambao mimi mara nyingi nilikuwa nasema jamani mbona umepitishwa karibu ya barabara, nikaambiwa umetiwa chini sana lakini tuliona athari iliyotokea Gombani ambapo palivunjwa na ikabidi Serikali iingie gharama nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 73 ambapo hapa kuna mradi wa uimarishaji takwimu Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, mradi huu pia huwa unagharimu fedha nyingi kwa kutaka kujua uchambuzi wa takwimu za sense ya watu na makaazi, ili Serikali iweze kupanga mipango ya maendeleo ya wananchi wake. Lakini inaonekana Serikali inakosa ufanisi mzuri wa kujua hali halisi ya takwimu iliyopo kwa baadhi ya wananchi kukosa kushiriki katika zoezi la sensa.

Mhe. Mwenyekiti, sensa tumeshuhudia imekuja na baadhi ya wananchi walikosa kushiriki kujiandikisha. Kwa hiyo, niseme hapa Serikali inafanya tu mipango yake kwa kubahatisha, lakini si kwa kuwa wana takwimu sahihi kwa sababu wenzetu walipinga tena kwa juhudi kubwa. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti mimi niiombe sana Serikali kwa sababu kukosa watu kujiandikisha ni kujizuilia katika kuingia mipango ya maendeleo, kwa sababu mipango ile ya maendeleo inaandaliwa kwa mujibu wa takwimu za watu. Leo mfano mdogo mimi tu nyumbani kwangu ambao kama nina watoto wanne au watano basi lazima hapo nitataka niwe na uhakika wa kuwaletea wanangu chakula ambacho kitawatosha. Leo kama mimi napeleka chakula watoto wa tano mimi napeleka cha watu wawili hiyo nikuweza kuwadhulumu wengine.

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti mimi niiombe Serikali kwa kweli kuweza kuwa madhubuti, kuweza kuwa imara wakati ule wa uwandikishaji kuona wale ambao wanakwepa zoezi ama kuwe na adhabu ya kuwachukulia au kuwe na utambulisho maalum mtu inapofika kutaka kwenda kujiandikisha katika huduma zozote za kijamii aweze kuonesha uthibitisho wake kama yeye kweli aliingia katika daftari lile la takwimu. Vyenginevyo tutaipa Serikali mzigo mkubwa sana kuendesha watu ambao haijui ni watu wangapi. Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti mimi nilikuwa niiombe sana Serikali iweze kulizingatia hili kwa sababu tutakuwa tunajikosesha maendeleo sisi wenyewe. Kwa hiyo, Serikali kwa kuwa yeye ndiyo mwangalizi wetu mkuu inabidi ichukue juhudi za makusudi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mimi leo nilikuwa sina mengi kwa sababu hata afya yangu haiko vizuri, lakini nasema naipongeza na nayapongeza mafanikio ambayo yamejionesha katika kitabu hiki na kwa niaba yangu na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia 100. Ahsante sana Mwenyekiti.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora. Awali ya yote na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujaalia kuja hapa tukiwa wazima wa afya.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza sana waziri pamoja na watendaji wake wote wa wizara yake kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya, lakini vile vile na kuweza kututayarishia hotuba iliyo nzuri. Nikisema hivyo haina maana kwamba sitotoa kasoro hotuba hii, lakini mwalimu yeyote anapokuwa anaiangalia kazi anakuwa anaipa *marks* na *wrong* zinakuwepo lakini *right* zikiwa nyingi ina maana kwamba lazima umpongeze mwanafunzi yule.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaanza katika ukurasa wa 20. Ukurasa huu kubwa ni kuhusiana na Idara ya Mawasiliano Ikulu. Kwanza nipongeze kwa kazi nzuri ambayo imekuwa ikifanya idara hii katika masuala ya mawasiliano hasa katika kurusha taarifa mbali mbali za utekelezaji wa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, shughuli nyingi ambazo zimekuwa zikifanywa na serikali zimekuwa zikionekana kama hazionekani, kwa maana kwamba wananchi hawapewi taarifa. Lakini kitengo hiki kwa kweli kimekuwa kinafanya kazi kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niende katika ukurasa wa 31 ambao unazungumzia suala zima la Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nje. Mimi nitoe pongezi sana katika idara hii kwa kazi wanayoifanya na kwa kweli tangu kuanzishwa kwa idara hii tumeona hatua mbali mbali ambazo tayari zimeshaweza kuchukuliwa na tumeona kwamba sasa hivi idara imekuwa na uwezo wa kuwapata Wazanzibari katika sehemu nyingi za ulimwengu. Kwa hiyo, mimi nichukue fursa hii vile vile kuwapongeza sana idara hii lakini nina masikitiko yangu.

Kwa kuwa Idara hii moja katika shughuli yao ni kushiriki katika mikutano mbali mbali ya kimataifa, kwa bahati mbaya sana bajeti ya idara hii siku zote inakuwa ndogo na naweza kusema kwamba sasa hivi tumeshachelewa. Lakini ningeiombea Idara hii ili kuweza kuhuwisha na kuboresha kazi zao basi ipewe bajeti ambayo itaweza kusaidia katika utekelezaji wa kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naipongeza vile vile Zanzibar kama Zanzibar kwa kuteuliwa kuwa Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mimi naipongeza na nafikiri sifa hiyo Zanzibar inastahili hasa kwa kujua kwamba Kiswahili ni lugha pekee ambayo inatumika vizuri katika nchi zote za Afrika Mashariki.

Lakini pia nilikuwa nataka kumuuliza Mhe. Waziri kwa sababu katika kumbukumbu yangu na kwa bahati nzuri Mhe. Mwenyekiti pamoja na wewe ambaye ulikuwa ndiye mkuu wa msafara wetu tulipokwenda Uganda, tulizungumzia suala na tukaambiwa kwamba bado Tanzania haijasaini mkataba wa makubaliano ya kuwa Zanzibar iwe ni kituo kikuu cha Kiswahili katika Afrika ya Mashariki. Hiyo ilikuwa inakwaza maendeleo mengi ya Kiswahili pamoja na nchi jirani wenzetu wa Afrika Mashariki. Nilikuwa nauliza na niliwahi kufuatilia nikaambiwa kwamba barua au huo mkataba kuna mambo yanafanyiwa kazi katika Baraza la Mawaziri la Tanzania. Sasa namuomba sana Mhe. Waziri atueleze imefikia wapi. Kwa sababu hapa taarifa iliyotolewa kwa kweli ni ya juu juu mno kiasi ambacho haitupi uelewa mzuri wa kuona wamefikia hatua gani.

Mhe. Mwenyekiti, niende vile vile katika suala hilo kwenye Idara hii. Nilikuwa nataka kujua na kwa hilo ambalo nalizungumzia kwa bahati nzuri vile vile mwaka jana tulipata bahati Kamati yangu kutembelea katika *Interparliamentary Conference* huko Kenya, Nairobi; tukashiriki katika masuala ya afya hasa katika masuala ya vifo vya mama na watoto.

Kwa bahati nzuri sana tuliweza kuiwakilisha Zanzibar na Tanzania nzima kwa sababu Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Tanzania hawakuwepo. Kwa hiyo, Zanzibar tuliweza kuwakilisha Tanzania nzima.

Lakini lilikuja suala moja ambalo pale wenzetu Wabunge wa Afrika Mashariki walitwambia, kunakuwa na shughuli nyingi na mikutano mingi inayohusiana na zile wizara ambazo hazimo ndani ya Muungano, lakini Wazanzibari hatukuoneni. Suala hilo Mhe. Waziri nilikuwa nataka utueleze kidogo kwa nini basi ushiriki wetu hasa katika yale masuala ambayo sio ya Muungano ni mdogo, au pengine haupo kabisa. Kwa sababu ninaamini kwamba kuna fedha zinawekwa kwa ajili ya maendeleo ya wadau wote wa Afrika Mashariki, lakini na Zanzibar tunataka tufaidike na

fedha zile ambazo zinatolewa. Hivyo Mhe. Waziri aje utwambie kwa nini au vipi, kuna utaratibu gani au kama kuna mikutano yoyote au kitu chochote ambacho tunashiriki kama Zanzibar kwenye zile wizara ambazo hazimo ndani ya Muungano zinashiriki.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakwenda katika ukurasa wa 35 ambapo mengi wamezungumza wenzangu na mimi vile vile nitajaribu kuzungumza kidogo, hasa kwenye ukurasa wa 36. Mhe. Waziri ametupa kesi ambazo zimefanyiwa uchunguzi juu ya tuhuma za rushwa, ambapo amesema kwamba tuhuma 21 zinazohusiana na makosa ya kutoa na kupokea rushwa, matumizi mabaya ya ofisi, ulanguzi wa tiketi za kusafiria, ukwepaji wa kodi, kughushi na kadhalika, kwa hiyo, mamlaka imeshaanza kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, hizi kesi sijui ni kwa ajili ya mwaka gani, huu ambao tunauzungumza wa bajeti, uliopita, kama ni hizi kesi 21 Mhe. Waziri naziona ni kidogo sana na nina hofu kwamba idara yake hii haifanyi kazi vizuri, haiwezekani kutokana na rushwa iliyopo ndani ya kisiwa chetu leo tuwe tuna kesi 21. Aidha, inawezekana sana kwamba hakuna vitendea kazi, au inawezekana uwezo wa wafanyakazi ni mdogo, haiwezekani tuwe na kesi 21 tu au panafichwa ukweli. Lakini Mhe. Waziri ningemuomba sana aje atwambie hizi kesi 21 ni za kipindi gani.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala ambalo Mhe. Waziri vile vile nataka kumuuliza linalohusiana na takwimu kwa ujumla wake katika hotuba yake, hili nilikuwa kwanza nataka kulisema mwanzo lakini nitalisema sasa hivi. Mhe. Waziri ametupa takwimu nyingi katika idara zake zote na hasa kuhusiana na masuala ya elimu ambazo wanapata wafanyakazi mbali mbali katika idara zake. Mhe. Waziri mimi nilikuwa nataka kumueleza kwamba, kuna umuhimu mkubwa sana katika dunia ya sasa hivi kutupa takwimu ambazo zitakuwa zimechambuliwa kijinsia.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kijinsia katika jamii yetu ya sasa hivi ni muhimu sana, hivyo ningemuomba Mhe. Waziri hivi sasa naamini kwamba si rahisi tena kuanza kuchambua hasa kwa hizi takwimu alizotupa, lakini ningeomba sana tena hili ni kwa mawaziri wote kwamba takwimu zozote zinazohusu wafanyakazi ndani ya wizara zao basi wazichambue kijinsia. Kuna umuhimu mkubwa kwa sababu mara nyingi sana kunatokea malalamiko kadhaa wa kadhaa kutokuwepo na usawa wa kijinsia ndani ya masuala mazima ya elimu, *promotion* pamoja na mambo mengine. Ili hili tuliondoe na tujisafishe kuna umuhimu mkubwa wa takwimu hizo kujitokeza ndani ya hotuba zetu.

Mhe. Waziri kama akigeuka nyuma sasa hivi tu idadi ya wanaume imeongezeka, lakini nimwambie tu kwamba katika Baraza letu ni asilimia 30 tu ndio ya kinamama, lakini tulipoingia mwanzo hapa tumekuta walioingia wanawake walikuwa karibu asilimia 90, kinababa wamechelewa. Hivyo, nataka kusema *how serious,* kinamama wapo katika utekelezaji wa shughuli zao. Kwa hivyo Mheshimiwa, tunataka na sisi tuone raha, tunapoona kwamba wenzetu wanapata haki zao katika idara zao wanazofanyia kazi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naendelea katika ukurasa wa 38 suala ambalo limezungumzwa na wengi na mimi nichukue fursa hii nimpongeze sana mwanamke mwenzangu, mwanamke mwenzetu ambaye kwa kweli tumemuona umahiri wake wa kufanya kazi, ndio maana nikasema wanawake wanaweza bila ya kuwezeshwa.

Mhe. Mwenyekiti, mwanamama mwenzetu huyu amekuwa *serious* katika kazi zake na kwa kweli anazifanya kazi vizuri sana. Sijawahi mimi kumsikia mtu ambaye hasa katika watu ambao anafanyanao kazi, watu wa *PAC* wanafanyanae kazi sana na sifa zote wanampa. Kama ingekuwa kila mwaka kuna zawadi fulani ambayo inatolewa nafikiri mama huyu anastahiki kupewa zawadi hizo.

Sasa katika ukurasa wa 38 nilikuwa nina swali najiuliza hapa, kwa sababu najua huyu mama anafanya kazi nzuri lakini kuna sehemu katika ukurasa huu inaeleza ripoti yake. Kwa sababu inaeleza kuwa ofisi yake imepita katika wizara 16 pamoja na Mashirika ya Umma manane (8) na miradi 12 inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo, lakini haijaelezea baada ya hapo imefanyika tu. Lakini hatujaambiwa kwamba kuna kasoro zozote ambazo zimejitokeza ndani ya ukaguzi wake wala hatua ambazo zimechukuliwa.

Labda taarifa hii ingeelezea kidogo kutupa taarifa kwamba katika hizo wizara ambazo zimekaguliwa pamoja na idara hizi basi angalau kuna maendeleo fulani katika mwaka fulani, ilikuwa hivi lakini sasa maendeleo, tunataka kuona *improvement,* sio mama huyu afanye kazi ya bure, tuone *improvement* ndani yake bila ya hivyo itakuwa kila siku tunasoma haya mabuku hayana maana, tunapewa mipango mingi lakini maendeleo na mafanikio ndio kitu tunaweza kusema *we are proud of*. Lakini mazungumzo haya kwa kweli mara nyingi sana unaona kwamba ni kitu

ambacho ni mipango tunapanga, lakini utekelezaji wake umefikia wapi? Mhe. Waziri naomba hapa anisaidie katika maelezo ya ziada.

Mhe. Mwenyekiti, nikiingia katika ukurasa wa 42 ambao unazungumzia suala zima la Idara ya Mipango na masuala ya kisekta ya kupunguza umasikini. Nimeona katika ukurasa wa 43 unaelezea kwamba imefanyika tathmini ya ufuatiliaji wa programu na miradi ya maendeleo katika maeneo mbali mbali ikiwemo Unguja na Pemba, kuna programu 18 na miradi 60. Nilikuwa naomba sana nipate taarifa nijue hii miradi ni ya kipindi gani na kitu gani kimepatikana katika tathmini hiyo, kwamba hii miradi inaendelea au haiendelei, imepatwa na matatizo gani au imepata mafanikio gani. Mhe. Waziri naomba hilo anieleze, nauliza kwa sababu midari mingi tunakuwa tunaianzisha na fedha nyingi serikali imekuwa inatoa katika miradi hiyo lakini matokeo yake inakuwa inasikitisha. Miradia ambayo inakuwa *successful* ni kidogo mno, sasa nilikuwa naomba nijue hasa hapa ni miradi ipi ambayo tumefanikiwa ili tujifunze katika haya.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba niende katika ukurasa wa 56 ni kuhusiana na Mradi wa Uimarishaji wa Nyumba za Viongozi. Hapa wenzangu wamezungumza sana juu ya suala zima la usalama wa viongozi, kwa nini viongozi wanakodiwa nyumba? Kwa kweli ukitizama hasa viongozi wetu wote takriban maeneo ambayo wanaishi hayalingani na nafasi zao, huo ndio ukweli na hili ni tatizo kwa sababu kiusalama sivyo. Lakini vile vile hali ya mazingira ya kumfanya kiongozi yule kesho anaamka asubuhi na kwenda kufanya kazi vizuri pia sio nzuri, sasa hilo tunaliweka kando hatulizungumzii sana, kwa sababu tunajua kwamba kuna changamoto mbali mbali na kuna hali ya uchumi hairuhusu. Lakini ningeomba sana na waziri hili naomba kuwe na eneo maalum sasa hivi litengwe kwa ajili ya nyumba za viongozi, litengwe eneo ambalo tutakuwa na mipango hata kama ya miaka 10 ijayo au 20 lakini tunajua eneo hili litakuwa ni eneo ambalo kutakuwa na nyumba za viongozi.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu maeneo mengi sasa hivi yanavamiwa tutakuja kujikuta kwamba gharama ya kuwaondosha wananchi kuwaambia hapa ondokeni tunataka kujenga nyumba za viongozi na eneo jengine hatuna.

Kwa hivyo, ningeomba sana sasa hivi kama eneo lipo mimi sijui nafikiri wenzangu wengi hawajui, lakini tujipange katika kuhakikisha kwamba tunapata eneo kubwa na zuri lenye usalama ambalo halipo barabarani, sio kwenye barabara kuu kwamba viongizi wetu wanaishi katika nyumba zinazostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kwenda ukurasa wa 58 ambao unazungumzia suala zima la Mradi wa Uimarishaji wa Juhudi za Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi wa Nchi. Hili nilikuwa naliomba na namuomba sana Mhe. Waziri kuna sehemu inasema kwamba, "Itachukua juhudi ya kuelimisha jamii ya mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu wa uchumi".

Mhe. Waziri ningekuomba sana elimu kubwa inataka kutolewa kwa wananchi na wananchi wengi hawafahamu kwamba ni jukumu lao kuhakikisha kwamba wahujumu ambao wanahujumu uchumi wa nchi hii wanatakiwa kutolewa taarifa, hilo ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, jukumu la maendeleo na jukumu la kulinda nchi yetu ni letu sisi wananchi. Lakini mengi yanatokea kwa sababu wananchi hawana elimu ya kufahamu, kinapoathirika kitu chochote ikiwa kama ni chanzo ambacho kinaweza katika kuukuza uchumi, ameathirika na yeye mtu mmoja. Hiyo ni *issue* ambayo inabidi kwa vyovyote vile elimu itolewe, lakini elimu hii kama sisi watu wazima tumeikosa lakini vile vile elimu hii iingizwe ndani ya Mitaala yetu ni muhimu sana. Kwa sababu haya mambo sasa hivi yanatokea mengi sana ambayo yanaharibu, jambo ambalo anafanya mtu mmoja lakini linaathiri wengi.

Kwa hiyo, Mhe. Waziri nakuomba sana elimu itolewe, elimu isambazwe kila pahala zitumiwe mbinu mbali mbali za kutoa elimu alimradi elimu hizi zifikie lengo na tuone mabadiliko. Kwa sababu baada ya elimu hiyo sio tu kuweka elimu lakini tuone mabadiliko kwamba watu sasa wanaelewa na hatua zinachukuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nitakwenda ukurasa wa 61 ..

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika tano.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nitamalizia sasa hivi naomba unipe muda mdogo kwa sababu wenzangu hawakuzungumza sana na wamenambia kwamba nizungumze muda mrefu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka nizungumzie kuhusu ukurasa wa 61, suala la mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Matokeo ya MKUZA. Mhe. Mwenyekiti, mimi nimefurahi sana Mhe. Waziri kwamba hili linafanyiwa tathmini na natarajia kwamba tathmini hii italeta mabadiliko makubwa kwa sababu bado huu MKUZA tumeanza zamani *Program* hii. Lakini bado unaona watu ni masikini hasa katika baadhi ya maeneo, kuna ambayo umasikini umezidi.

Sasa katika kutathimini kwenu lazima mhakikishe kwamba kuna mpango maalum wa kuyaangalia haya maendeleo ambayo kwa kweli umasikini umekithiri na mimi ningeomba sana katika mipango hii na mikakati hii Mhe. Waziri, Wajumbe wako Wawakilishi wa Baraza la Wawakilishi wakiwemo na Wabunge katika maeneo yao wahusishwe kikamilifu kwa sababu wao ndio wanayajua maeneo yao, ili kuwe na *bridge* baina ya Serikali na Wawakilishi katika maendeleo ya Majimbo yao.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu hapa kunakuwa saa nyengine na nafasi kiasi ambacho Wajumbe au Wawakilishi wao ambao wamechaguliwa na wananchi wanakuwa hawajui nini serikali inafanya, na wao ndio wasaidizi wakubwa wa serikali hii. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana na hili pia ulitilie maanani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitamalizia katika ukurasa wa 68 unaozungumzia mradi wa mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ambayo unaitwa *PPP*. Mhe. Mwenyekiti, huu mradi ni muhimu sana, kwa sababu hapo ndipo itakapokuwa nafasi nzuri kwa wananchi wazawa wakaweza kunufaika kiuchumi au hata wale ambao wanaotaka kuekeza wataweza kunufaika kiichumi. Sasa mimi ningeomba sana elimu itolewe sana kwa sababu wengi wanasikia hata na sisi Waheshimiwa Wajumbe tunasikia suala zima la Mashirikiano haya ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, lakini hadi sasa hivi bado hatujaambiwa vizuri, ina maanisha nini? Ukweli ndio huo Mhe. Waziri.

Tungeomba sana utupe elimu sisi pamoja kwa ujumla na wananchi ili waweze kutambua wale ambao wanataka kujiingiza katika masuala hayo, basi wawe na elimu ya kutosha kuweza sasa kutambua nini hasa wanaweza kufanya katika kusaidia kukuza uchumi wa Taifa hili.

Mhe. Mwenyekiti baada ya kusema hayo makushukuru sana kwa kuniongezea na namuomba sana Mhe. Waziri nataka kumwambia tu kwamba nimeikubali hotuba yake kwa asilimia mia moja. Isipokuwa naomba sana, sina nia ya kupiga buti lakini naomba sana anijibu maswali yangu. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusu Makadirio na Mapato ya Mwaka 2014/15.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanzia naomba nianze na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi ukurasa wa 35.

Kwanza naunga mkono Hotuba ya Mwenyekiti, wa Kamati kwamba Bajeti inayopangiwa Mamlaka hii ni ndogo haikufika hapa 50% ya Bajeti yote ambayo imetengewa. Lakini nifananishe Mamlaka hii sawa sawa na ile Tume ya Kuzuia Madawa ya Kulevya kwamba wanatengewa Bajeti kidogo, lakini kesi ambazo wanaenda kuhangaika nazo ni kesi ambazo za pesa nyingi. Kwa hiyo, ni vyema Serikali ikaangalia kwamba taasisi kama hizi ziwe zinatengewa bajeti yake ya kutosha ili kuona kwamba wanapambana na zole *issues* ambazo wamepangiwa kupambana zanzo.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo katika Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kuhujumu uchumi nilikuwa naangalia utoaji wa elimu. Wamejitahidi wametoa elimu maeneo mengi. Lakini nilikuwa naona kama wame-*base* sana kwenye upande wa waombwaji rushwa yaani wametoa elimu zaidi kwa wananchi ambao wanaombwa kuliko kwa wale ambao wanaomba rushwa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana katika kipindi cha bajeti hii waangalie sana ili waone kwamba angalau kunakuwa kuna-*balance*, kwa sababu kama hujaombwa sio sana kutoa, mtu akijitolea tu mwenyewe kama mimi nitakupa kiasi fulani nifanyie hiki, sana sana wanaombwa ndio maana wanatoa. Kwa hiyo, ni vyema wakaangalia kwamba ule utoaji wa elimu unakuwa *balance* katika sehemu zote kwa sababu mtoaji na mpokeaji wote wana makosa.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, katika hii Uhujumu Uchumi hapo hapo katika suala la elimu hakuna anaejue sote tunazungumzia kuhusu Mahakama zimekithiri rushwa. Lakini sijaona katika utoaji wa elimu hii kwamba wamekusanywa wale Waheshimiwa wakawapa semina au elimu kuhusiana na madhara ya kuomba rushwa na mambo kama hayo, yaani haki wanazokosa wananchi kutokana na rushwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo nimeona kwamba wametoa elimu kwa Makamishna wa Polisi lakini kwa kweli Mahakama ambazo zinalalamikiwa sana elimu hiyo haijafika. Mhe. Mwenyekiti, nikimaliza na Uhujumu Uchumi naomba niingie Idara ya Mawasiliano Ikulu ukurasa namba 20. Napongeza kazi nzuri inayofanywa na Idara ya Mawasiliano Ikulu kwa kuendeleza taswira nzuri ya Mhe. Rais wa Zanzibar. Kwa kuendeleza Mawasiliano baina yake na wananchi ambao anawatumikia. Kwa kutoa taarifa mbali mbali na elimu kwa wananchi juu ya mambo ambayo Mhe. Rais anafanya. Nimeangalia vipindi ambavyo wamerusha vingi ni vya TV kuliko vile ambavyo taarifa za Redio au Majarida ambayo ndio nzuri kwa sababu wananchi wengi wanafikiwa kwa hizi TV na Redio kuliko hivi vijarida ambavyo vinatolewa.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na wazo moja kwa nini hii Idara ya Mawasiliano Ikulu isifanye kazi sambamba na Ofisi ya Faragha hasa pale Mhe. Rais anapoenda safari za nje, tunaona kwa upande wa wenzetu Bara kwamba ziara nzima inaweza ikaoneshwa katika TV na wananchi wakajua kwamba Mhe. Rais kaenda nchi hii, kafanya hiki, faida iliyopatikana hii.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba kwamba wasione shida wawapeleke hawa waandishi wa habari waende wakaangalie nini Rais anafanya, wakusanye ile *documentary* ili wakija hapa wananchi wanatapa kuona Rais kenda nchi gan,i kafanya nini na faida gani zimepatikana kutokana na safari zile alizofanya, kuliko kusubiri arudi hapa tukusanye waandishi wa habari Uwanja wa ndege pale waanze kumuhoji. Ni vyema tukapeleka, tusione uchoyo, kizuri kinajitangaza msipojitangaza hakuna atakaekujua. Kwa hiyo, vyema Rais anapoenda safari za nje muambatanishe na wanandishi wa habari, wananchi waone mambo mazuri ambayo Raisi wao wanafanya.

Mhe. Mwenyekiti, tunaelekea 2015 *End of the Road* nikimaliza idara hii hii natoa pongezi kwa lengo namba 3 la kuanzisha Kitengo Maalum cha Uwekaji wa Kumbukumbu za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Mwenyekiti, naipongeza sana idara hii kwa hatua ambayo imechukuwa kwa sababu ni vyema tukawa na historia ya Marais waliopita tukakusanya kumbukumbu zao na hotuba zao kwa sababu katika hotuba zao mnakuwa mara nyingi hujaa nasaha, ushauri na miongozo mizuri ambayo hata viongozi wa baadaye wanaokuja wanaweza wakatumia.

Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tukishuhudia Mhe. Saleh Nassor akiulizia sana kumbukumbu ya Hotuba ya Mhe. Mzee Abeid Aman Karume. Sasa kama idara hii imeamua kufanya hivi ni vyema kwa sababu Mhe. Saleh Nassor Juma sana ana-*base* kuuliza Wizara ya Habari. Sasa kama Wizara ya Habari haziko *at least* Ikulu zitakuwa zipo, kwa hiyo mtu yeyote anaetaka kumbukumbu hizi anapata. Kwa hiyo, niipongeze Idara kwa kufikiria hili na ni vyema ikatelezeka kama walivyojipangia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niendelee katika Mradi wa Uimarishaji wa Nyumba za Viongozi na Nyumba za Serikali na mimi naungana na wote wale waliosema kwamba ipo haja sasa, nimeona katika maagizo ambayo kamati imetoa kuna agizo namba 8 kiambatanisho namba 14 kwamba kamati imeagiza Ukarabati wa Jengo la Ikulu Kibweni na utekelezaji ni kwamba Ofisi tayari imewasilisha waraka Serikalini ili kuomba kuwa na mradi maalum wa matengenezo wa majengo yote ya urithi.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli haipendezi kuona kwamba majengo tunayo tunayaacha yanaharibika na tunakwenda kukodi nyumba za watu, viongozi wetu wanakaa haileti taswira nzuri. Kwa hivyo, ni vyema mradi huu ukaanza ili kuona kwamba viongozi wetu baada ya kuishi mitaani na watu wengine wa kawaida wanaishi maeneo maalum ambayo ni salama na hakuna kelele kama wanavyosema.

Mhe. Mwenyekiti, naungana na wenzangu wote ambao wamesimama hapa kuipongeza Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mhe. Mwenyekikti, mimi nafahamu utendaji wake kwa sababu wakati taasisi hii ipo katika Wizara ya Utumishi sisi Kamati ya Katiba na Sheria tulikuwa tunasimamia taasisi hii. Kwa hiyo, mimi naelewa utendaji wake na wala hizo sifa zinavyotoka hapa sishangai kwa sababu najua ni mwanamama anaweza, nafahamu utendaji wake na naamini kwamba viongozi wengi hawa wa serikali wasione haya waende wakamuulize,

wakapate ushauri ili kuona kwamba na wao mambo yao yanakwenda vizuri kama yanavyokwenda ya huyu mwanamama.

Mhe. Mwenyekiti, nikimaliza hapo naomba niingie kidogo kwenye vifungu ukusarasa wa 71 Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Utawala Bora kifungu 311202 Ununuzi wa gari. Nilikuwa nauliza tu Mhe. Mwenyekiti, yaani gari ya aina gani ambayo inakwenda kununuliwa, kwa sababu nimeangalia kiasi cha pesa kinachotengwa kwa ununuzi wa gari kuanzia milioni 50,60 na kwenda mbele. Lakini hapa wametenga milioni 20. Kwa hiyo, nilitaka kujua ni gari ya aina gani ambayo Idara ya Utawala Bora inakwenda kununua.

Ukurasa wa 74 Ofisi Kuu Pemba, huduma za Utafiti nimeona hapa Huduma za Utafiti zimetengewa bilioni mbili tu. Nilikuwa nauliza hii ni pesa ya huo utafiti au ndio utafiti umeshafanyika unaendelea, kwa sababu naona pesa iliyotengwa milioni mbili ni kidogo sana. Juzi tulikuwa tunaangalia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kuna fedha kama milioni sabini na sita zimetengwa kwa utafiti. Sasa nilikuwa najiuliza huu utafiti umeshaanza, unaendelea au ndio unaenda kufanya hivi sasa kwa sababu hizi pesa zilizotengwa ni kidogo sana.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 76 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti katika gharama za Umeme hapa nilikuwa nataka maelezo kwamba wenzetu wameanza kutumia *Solar* hawalipii tena umeme au vipi? Kwa sababu ukiangalia katika fungu la umeme hapa 0 tangu mwaka juzi. Sasa watwambie siri kama wameanza kutumia *Solar* waanze kuwaelimisha na wenzao ili ku-*save* pesa za wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, katika Idara hiyo hiyo ukurasa wa 77 kifungu 263178 Ushauri Nasaha HIV *counceling* haijaekewa kitu. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kufahamu kwamba Ikulu mambo poa hamna wanaohitaji kuelimishwa kuhusu UKIMWI yaani haifahamiki tunasisitizwa kwamba elimu itolewe lakini hakuna fungu lolote ambalo limetengwa kuendana na *HIV Counseling.*

Ukurasa wa 87 Mhe. Mwenyekiti, kifungu 281401 Malipo ya Kodi hii nafikiri ni Idara ya Utumishi na Uendeshaji milioni kumi. Nilikuwa naomba maelezo Ofisi *Rent* ni Ofisi gani ambayo imetengewa milioni kumi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia nilikuwa naangalia *Trend* ya Uingizaji wa pesa wa Ofisi hii na nikaona kuna baadhi ya taasisi ziko chini. Lakini kuna baadhi ya taasisi hazijafikia hata matumizi ya asilimia 50, lakini kuna hiyo Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watenda kazi yaani wamepindukia matumizi ambayo walioidhinishiwa, waliidhinishiwa mia moja arubaini na tisa *point* moja, fedha zilizopatikana ni mia moja na tisini na tano, yaani wamefikia asilimia ya fedha mia moja na thalathini ya matumizi. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba maelezo kulikuwa na nini mpaka wakatumia kupindukia. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia machahe katika hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu alietujaalia, akatupa afya njema na tukafika hapa leo tukiwa wazima.

Mhe. Mwenyekiti, pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kumpongeza Mhe. Waziri kwa dhati kabisa jinsi alivyotoa hotuba yake na imefahamika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze kwa kusema hivi ripoti ya utekelezaji wa haki za binadamu kwa mwaka 2013 imetoka. Sasa hapa naomba niishauri Serikali ifanye mazingatio katika ripoti hii. Nasema hivi kwa sababu ripoti ile iliyotoka ni kama kioo, sasa Serikali inapojiangalia katika kioo cha ripoti hii itaweza kufanya marekebisho pale ambapo panahitaji kufanyiwa marekebisho. Mhe. Mwenyekiti, unapojiangalia kwenye kioo ukaona mapungufu yako basi utaweza kujifanyia wepesi kwa kurekebisha shughuli zako. Kwa hiyo katika hili, naiomba Serikali ijitizame vizuri katika kioo hiki cha ripoti ile ya haki za binadamu iliyotoka, ili tupate kujisahihisha.

Mhe. Mwenyekiti, Idara inayoshughulikia Wazanzibari waliopo nje ni muhimu sana, kwani Wazanzibari wengi wanaishi nje ya nchi, na hawa ni sehemu ya mafanikio yetu tunawategemea sana. Sasa hapa nahitaji maelezo kidogo ili nipate ufahamu zaidi. Je, Idara inayoshughulikia hawa wenzetu waliopo nje ya nchi, imefanya usajili gani wa kuwatambua Wazanzibari hawa waliopo nje na wamepatiwa kitambulisho cha aina gani ili kuzidi kupata moyo wa

kuisaidia nchi yao kwa mambo tofauti kwa hali na mali na ushauri pia. Kwa sababu msaada si pesa tu, hata ushauri pia. Kwa kuwa hawa wenzetu wapo nje ya nchi wanaweza wakaishauri Serikali yetu, lakini sasa Waswahili wanasema "Mcheza kwao hutunzwa". Sasa je, nataka kujua wenzetu hawa wanasaidiwa kiasi gani.

Halafu mchango wa uchumi wa Wazanzibari waliopo nje unaratibiwa vipi na kwa mwaka ni kiasi gani. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anisaidie kidogo maelezo haya nipate ufahamu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu cha Mhe. Waziri kuna Idara inayoshughulikia Kupunguza Umaskini na kuna Idara ya Ukuzaji wa Uchumi. Kwa ufahamu wangu naona Idara mbili hizi zote zinafanya kazi moja. Sasa hebu Mhe. Waziri naomba niulize kuna umuhimu gani wa kuwa na Idara mbili zinazofanya kazi moja? Atakapokuja hapa Mhe. Waziri naomba anifafanulie kidogo ili nipate kufahamu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kiambatanisho namba 9 ukurasa wa 88 kuna wafanyakazi waliopatiwa udhamini wa masomo kwa mwaka 2014/15. Hili ni jambo zuri sana kwa sababu kupatiwa udhamini wafanyakazi wetu ni jambo sahihi na tunalipongeza kwa dhati kabisa. Lakini katika hili naomba niulize. Wafanyakazi hawa ni kwa Wizara zote au ni kwa ofisi yako tu Mhe. Waziri. Kwa nini mafunzo ya gesi na mafuta hayamo katika wafanyakazi waliopatiwa udhamini huu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika kiambatanisho namba 19 ukurasa wa 93 bajeti ya kawaida ya Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Wanu Hafidh Ameir kalizungumzia kidogo lakini na mimi pia nataka nilizungumzie. Hapa inaonekana wenzetu hawa wametumia hadi asilimia 131 ya makadirio yaliyopitishwa na Baraza lako tukufu. Mhe. Mwenyekiti, naomba kupata maelezo ya kina kwa nini hali hii imejitokeza kwa Idara hii kupewa pesa nyingi sana wakati kuna Idara nyengine zimepatiwa asilimia 40 tu ya makadirio. Je, huu si upendeleo Mhe. Waziri. Hawa wenzetu wengine waliopewa asilimia 40 watafanyaje kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, katika kiambatanisho namba 12 pia ukurasa wa 94 kuna matumizi ya programu ya maendeleo ya mradi wa mashirikiano baina ya sekta za umma na sekta binafsi. Pia imepata asilimia 6.7 tu. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hii pia naona haileti picha nzuri. Kwa sababu tunakuwa tukiambiwa kila wakati kama Serikali inatoa kipaumbele kwa mashirikiano ya sekta za umma na sekta binafsi, wenyewe wanaita *PPP*. Lakini hizi kutiliwa asilimia 6.7, kweli hayo matarajio au mafanikio yatapatikana katika hali kama hii. Naomba hili uliangalie vizuri halafu utakapokuja hapa unisaidie kidogo kupata maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, kama wenzangu walio wengi walivyotangulia kuzungumza kuhusu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Nawaomba sana watendaji wa Serikali wasione choyo kwa kumtaja Mdhibiti na Mkaguzi kila wakati, ni haki yake kutajwa kwa sababu utendaji wake kila mmoja anauona. Lakini naziomba Wizara zote za Serikali anazozifanyia kazi zimsaidie huyu mama azidi kufanya shughuli zake kwa ufanisi zaidi. Ingawaje anafanya lakini kuna baadhi ya mambo yanarudisha nyuma kidogo kumpa nafasi ya kufanya shughuli zake vizuri zaidi. Kwa sababu yeye ana kipindi huwa anachukua taarifa zile za hesabu za mwisho wa mwaka. Ni muda mwingi tokea mimi nipo kwenye Kamati ile ya *PAC* hilo tunalipigia kelele mpaka nimeondoka na pia bado wenzangu wanaendelea kulipigia kelele.

Baadhi ya watendaji wanachelewa sana kupeleka zile hesabu za mwisho wa mwaka, jambo ambalo linarudisha nyuma kupatikana ili Serikali kujua hasa mipango yake, hesabu zake zipo vipi. Sasa hili nawaomba sana watendaji wasione choyo kumpelekea hizi ili akafanya kazi zake vizuri, na wao wakifanya mambo vizuri watasifiwa. Hii ni haki yake huyu mama kusifiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kuna kiambatanisho kuimarisha mazingira katika Idara ili iweze kutoa huduma nzuri. Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha mazingira ya kazi katika Idara ili iweze kutoa huduma nzuri basi ni lazima hayo mazingira yawezeshwe vizuri. Kwa sababu katika Idara nyingi wengine kama hivi bajeti zao zinakuwa ni hafifu sana. Sasa katika mazingira haya kuwa bajeti zao ni ndogo na ukizingatia kazi zinazofanywa ni kubwa, sasa hapa inakuwa si rahisi kufanikisha. Baadae tutakuja kuzilaumu baadhi ya Idara hazifanyi kazi vizuri lakini wana nia ya kufanya vizuri, isipokuwa tatizo lao bajeti zinakuwa ndogo katika baadhi ya Idara nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache sina nia ya kuzuia bajeti hii, isipokuwa Mhe. Waziri atakapokuja hapa anijibu maswali yangu niliyomuuliza ili twende vizuri tupate ufahamu tuendelee na bajeti yetu. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri nitakuwa sina mchango mkubwa sana kwa vile nilikuwa nikikaimu huko mbele. Nianze na Kitengo cha Rushwa. Kitengo hiki tokea kilipoanzishwa wakati huo dhamana alikuwa Waziri Mhe. Haji Omar Kheir, mimi nilikipigia kelele sana kutokana na uwezo wake waliopewa ni mdogo, ikafika wakati Mhe. Haji hata akaniona mimi ni mbaya kiasi fulani katika vifungu. Lakini ukweli kitengo hiki hakifanyiwi haki. Nilisema kifutwe hasa mimi, Serikali haijawa tayari na kitengo hiki. Kitengo hiki kifutwe mpaka Serikali itakapokuwa tayari ilete. Huu ushahidi upo mwingi.

Mhe. Mwenyekiti, tuanze na gari, nafikiri gari waliyokuwa nayo ni ya Mkurugenzi wa Utawala Bora. Mhe. Mkurugenzi kama upo huko juu mimi ni mtetezi wenu kwa muda mrefu wa Kitengo cha Rushwa. Kama Bwana Mussa upo juu hii hali ndio ilivyo. Mwaka jana nafikiri waliomba bajeti ya milioni 800, watu hawana ofisi, hawana gari hao, wamepewa kama milioni 610. Uwajibikaji uko wapi, watafanya kazi kwa njia gani. Hii ofisi iliyokuwepo nafikiri wanatumia Baraza la Manispaa na wao ninavyofahamu mimi. Kwa hiyo tusijaribu kudandia gari uchungu wake tuliokuwa hatuujui. Hii Serikali hapa bado haijawa tayari kwa kitengo hiki. Ikae ifikirie tena, hawawezi kufanya kazi ikawa gari moja tu, nafikiri wanayotumia kitengo hiki watafanya kazi katika mazingira gani, watafanya wakati gani.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la mishahara hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu ni watu lazima wafikiriwe. Ofisi yao inaitwa Kupambana na Rushwa, ikiwa mishahara midogo hawawezi kufanya kazi kweli rushwa itazidi. Mhe. Mwenyekiti, Dkt. Mwinyihaji Makame mimi nampenda sana, mzee wangu, hiki kitengo bado hakijawa tayari kufanya kazi zake, hatujawapa nyenzo. Mhe. Mwenyekiti, Pemba nafikiri mpaka leo hakuna ofisi, wala halitaki tochi, wala kumurikwa suala hilo. Sehemu za Makunduchi, kwengine huko Kaskazini watafikaje kwa gari moja. Wakitaka mafuta wakatafute mtu wamuombe. Nafikiri kitengo hiki bado kifikiriwe kwa hali na mali, na kama kinaomba pesa basi kipewe pesa zake zote. Kisiende ikapiga hodi, vyengine hakiwezi kufanya kazi. Nafikiri kimeajiri watu 51, sijui hivi kama sikosei.

Mhe. Mwenyekiti, nije suala la Utawala Bora pamoja na watu kupata haki hasa Mahakamani. Hapa bado kidogo kuna matatizo sana, hili moja la Utawala Bora Mahakamani kumekuwa kitendawili sana. Huku rushwa inaonekana, uzembe, uwajibikaji haupo. Kuna kesi nyingi za ardhi bado watu wanalalamika. Watu wamekuwa wakiteseka kwa muda mrefu, wanakwenda wengine hawarudi mpaka wengine wanapoteza maisha yao kule, haki yao haipatikani. Utawala Bora uko wapi hapa, uwajibikaji haupo. Hapa wananchi ndipo wanaposhindwa kuiona Serikali yao ukweli wake uko wapi.

Hebu tulifikirie suala la Mahakama ya Ardhi ni suala la kuliangalia sana. Tuna uhakika bado kuna wengine watapoteza maisha yao pamoja na haki zao, miaka saba, minane wengine hata kupanda ngazi hawawezi. Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri suala la utawala bora aliangalie kwa jicho la huruma sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache mpaka nitakapopata maelezo kuhusu Kitengo cha Rushwa nitamuunga mkono Mhe. Waziri kwa nia njema kabisa.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* kutujaalia jioni hii kuwepo hapa katika kutekeleza majukumu yetu ya kuzisimamia Wizara mbali mbali za Serikali kwa niaba ya wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, pia nachukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kunipa nafasi hii ya kuchangia. Vile vile nimpongeze Waziri mahiri huyu Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame kwa kuwasilisha ripoti yake kwa ufasaha, iliyoambatana na ripoti ya Mwenyekiti wa Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu pamoja na ile iliyotolewa na Mwenyekiti wa *PAC,* Mhe. Omar Ali Shehe. Kwa jumla nasema kwamba wametupa ripoti nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu nitauanza katika ukurasa wa 38 kwenye Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mhe. Mwenyekiti, ofisi hii ni muhimu sana kwa sababu bila ya ofisi hii basi chochote kile ambacho kinachangwa katika kodi za wananchi, bila ya ofisi hii kuzisimamia kwa kuzikagua basi kusingekuwa

na chochote ambacho kingeliendelea. Lakini ofisi hii imepewa jukumu kikatiba kuzisimamia Wizara zote kimatumizi baada ya kupitishwa bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze basi na mimi kama walivyompongeza wenzangu huyu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa jinsi anavyofanya kazi vizuri na kwa ueledi wa hali ya juu. Masikitiko yangu makubwa Mhe. Mwenyekiti, yapo kwa Serikali katika kutekeleza majukumu yao pale zinapokuja ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, ni masikitiko yangu makubwa kwa sababu tokea lianzwe Baraza hili 2010 tumepata ripoti ya mwaka 2008/2009, 2009/2010, 2010/2011 na 2011/2012. Lakini ripoti zote zinazoletwa kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zina mambo mengi ya uharibifu wa fedha, matumizi mabaya ya fedha, lakini hakuna hatua zozote za Serikali ambazo zinachukuliwa juu ya watendaji ambao wanafanya ubadhirifu wa matumizi ya fedha za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki niseme tu kwa mdomo mtupu, nataka niendelee na vielelezo kwa kukiangalia kitabu cha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambacho tunacho mbele yetu cha mwaka 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti, kitabu hiki nataka niwaambie Waheshimiwa Wawakilishi wote katika ukurasa wa 6 shukrani *paragraph* ya 10 hayo maneno ya mwisho kabisa. Mdhibiti anasema "Natarajia kuwa Baraza la Wawakilishi litaona ripoti hii kuwa ni muhimu katika kuiwajibisha Serikali kwa jukumu lake la usimamizi wa fedha za umma na utoaji wa huduma kwa wananchi. Hivyo, nitafurahi kupata maoni kwa watumiaji wa ripoti hii jinsi gani nitaweza kukuza na kuimarisha ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali."

Mhe. Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi wana wajibu mkubwa kuviangalia vitabu vya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuisimamia Serikali ipasavyo ili kuhakikisha kwamba fedha za umma zinatumika kama zilivyotarajiwa. Kinyume na hivyo tutawapa kodi kubwa wananchi wetu lakini matokeo yake wanaofaidika na kodi hizo ni watendaji wachache waliopewa dhamana za matumizi ya fedha za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, nikiangalie kitabu hiki ukurasa wa 21-22, Mhe. Mwenyekiti, kuna mapungufu mengi ambayo yanafanywa na watendaji waliopewa dhamana za fedha. Ukurasa wa 21 unasema "Kuongezeka kwa malipo ya viinua mgongo shilingi 35,899,595/=. Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya Mkaguzi yanasema "Ukaguzi uliofanyika umebaini kuwa kuna wastaafu mbali mbali walioongezewa mishahara kinyume na utaratibu kwa lengo la kupata viinua mgongo vikubwa ambavyo hawastahiki kupewa kulingana na mishahara yao.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba yule mkurugenzi, sijui tunamuita mkurugenzi wa uhujumu wa uchumi na rushwa, yule ikiwa hana pa kuanzia basi miongoni mwa vyanzo vyake vya kuangalia rushwa na matumizi mabaya ya uhujumu uchumi basi umo ndani ya vitabu mbali mbali vya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, ninapenda nimuulize Mhe. Waziri. Je, harakati hizi zinazofanywa na Mdhibiti zinamalizia wapi? Mhe. Mwenyekiti, niendelee na ukurasa wa 26 na 27 kuhusiana na masuala haya haya ambayo yanapoteza fedha nyingi bila ya hatua yoyote serikali inazozichukua. Mhe. Mwenyekiti, kuna ujenzi wa nyumba pamoja na utengenezaji wa mnara wa matangazo eneo la Bungi, jumla ya shilingi milioni moja ishirini na moja na mia saba na tisini. Fedha hizi Mkaguzi anasema hivi kwamba ukaguzi umebainika kuwa Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imefanya maliopo kwa Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Michezo na Utalii kupitia Kitengo cha madeni ya serikali kwa hati P/D05/11/211 yenye hundi namba hiyo hapo ya tarehe hiyo hapo. Hizi ni shilingi milioni moja na kitu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mambo haya yanasikitisha sana fedha ambazo zinatumika ovyo. Lakini nikiendelea na Ofisi ya Mdhibiti unavyofanya kazi bila ya hatua yoyote inayochukuliwa serikalini tusiyoijua sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi huko, kuna ukurasa wa 27 kuna malipo yasiyokuwa na vielelezo, yaani nyaraka pungufu shilingi milioni mia moja tisini na tano laki tisa sitini na saba elfu, haya yamefanyika bila ya vielelezo vyovyote.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hali hii inaumiza sana. Ukikiangalia kitabu hiki kina maeneo mengi ambayo yanaelezea matumizi ya fedha za serikali ambazo zinatumika bila ya utaratibu wa kisheria, bila ya utaratibu wa kutumia kanuni za fedha na kanuni za manunuzi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimuombe Mkaguzi na Mdhabiti Mkuu wa Hesabu za Serikali asivunjike moyo, aendelee na kazi yake kuwafichua wabadhirifu, yeye atakuwa amenawa. Waliobaki kutokutekeleza majukumu yao aawaachie wao majukumu yao. Mhe. Mwenyekiti, ninasema kwamba tunaambiwa kwamba sote ni wachunga, tutaulizwa namna gani tulivyowachunga watu wetu, tulivyokuwa tunavisimamia. Mhe. Mwenyekiti, Mkaguzi hongera kwa kazi yako na endelea na kazi hii, usione aibu hata kidogo kuwafichua wabadhirifu. Wale ambao wanaohusika na kuchukua hatua, kama hawachukui hatua basi wewe kazi yako imekwisha.

Mhe. Mwenyekiti, hiki kilikuwa ni kitabu cha ukaguzi wa hesabu kwa mawizira, mashirika na taasisi mbali mbali. Nimeangalia mifano michache tu, mifano ambayo nikiitia hesabu hapa, fedha ambazo zimetumika bila ya utaratibu zinazohusika ni shilingi bilioni moja, milioni mia moja na kumi na sita, laki nane, ishirini na tatu elfu, mia nane na tisini na sita. Hizi ni wizara chache, ni ofisi chache ambazo ukaguzi huu umefanyika mwaka 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kaguzi za nyuma zina maburungutu ya mapesa kama hizi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na kitabu cha Mdhibiti cha mwaka huu huu ambacho kinahusiana na miradi ya maendeleo. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, hapa napo kuna mambo mbali mbali ambayo yanasikitisha sana. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri anayehusika na Ofisi ya Mdhibiti basi ahusike na ofisi mbali mbali za serikali ambazo zinadhibiti fedha lakini hawazitumii fedha hizi ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na kitabu hiki cha miradi ya maendeleo. Kuna ucheleweshaji wa miradi ya maendeleo. Kuna Kikosi cha Valantia hiki, kuna shilingi milioni tisini. Mkaguzi anasema ukaguzi uliofanyika umegundua kwamba fedha hizo zote zimeingizwa kwa mujibu wa bajeti ya ujenzi huo, lakini hadi ukaguzi unakamilika hatua ya ujenzi huo hauridhishi kulingana na fedha zilizotolewa.

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana jinsi gani ya tunavyowakamua watu wetu vijijini, wanyonge hawapati muda wa kutononoka katika maisha, hawapati fedha za kuwasomeshea watoto wao kwa ajili ya maisha magumu, lakini watendaji wanazitumia fedha wanavyotaka.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 10, "Ukarabati wa nyumba za maendeleo Wete". Nyumba hizi zilitengewa shilingi milioni mia moja na kumi na kuingizwa kwa ajili ya ukarabati wa nyumba Nam. 4 iliopo Wete Mtemani Pemba. Ukaguzi uliofanywa umebaini fedha hizo ziliingizwa hazikutumika kwa ukarabati wa jumba hilo. Mhe. Mwenyekiti, kuna nini. Naomba huyu Mkurugenzi wa Mapambano ya Rushwa na Uhujumu Uchumi hapa ndio pakuanzia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mimi ninasikitika sana na kwa kweli kama nitaingia katika mchango wangu pahali pengine popote, ninahisi kama kwamba sijawatendea haki wananchi wa Zanzibar kama siwatetei jinsi ya fedha zao zinavyomumunywa na watu wasiopenda au watendaji wasiopenda maendeleo ya wanyonge wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningewaomba watendaji ambao wanahusika na kutumia taratibu za manunuzi pamoja na matumizi yoyote ya serikali wafuate utaratibu. Kwani inawezekana kwamba kukosekana kufuata kwa utaratibu huu ni mtandao mkubwa. Sasa lakini kwa sababu kuna msemo wa Kiswahili unaosema, "Mgwia na ngozi ndiye mwizi". Atakayekamatwa ni yeye ndio mwenye dhamana ya fedha, si mtu mwengine ambaye yupo mgongoni kwake.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi, kuna taarifa ya Mhe. Waziri aliposema taarifa yake anasema kwamba...

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika tano.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Ahsante sana dakika tano zitanitosha. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imekamilisha matengenezo makubwa ya jengo la ofisi hiyo iliopo Pemba kwa asilimia 99. Lakini niliisikia ripoti ya Mwenyekiti akisema kwamba Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

imejenga jengo ambalo limekamilika. Swali langu lipo hapa. Je, ni ipi kauli thabiti kutengeneza jengo na jengo hili lipo Pemba wapi au kujenga jengo jipya na jengo hili lipo wapi.

Mhe. Mwenyekiti, ninatoa shukurani zangu za dhati kwa wananchi wangu wa Jimbo la Chambani kwa kunipa tena ridhaa ya upendeleo, hivi sasa ninaona message ya watu wa Chambani kunipongeza juu ya mchango wangu huu. Kwa hivyo kwa niaba ya watu wangu wa Jimbo la Chambani sitoiunga mkono hotuba hii mpaka nipate maelezo ya kina juu ya ubadhirifu wa fedha za serikali.

Je, watendaji hawa wabadhirifu Mhe.Mwenyekiti, wanafanywa nini baada kugundulikana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali?

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante mheshimiwa. Sasa ni nafasi ya Mhe. Marina Joel Thomas na baadae Mhe. Machano Othman Said.

Mhe. Marina Joel Thomas: Mhe. Mwenyekiti ahsante na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, kabla sijachangia ninaunga mkono asilimia mia moja hotuba hii. Pili ninampongeza Waziri kwa kuandaa hotuba hii nzuri ambayo imejaa mambo mengi yaliyotekelezwa pamoja na watendaji wake kwa kumsaidia kuandaa taarifa hii. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nitaanza katika Mamlaka ya Kuzuia Rushwa. Mamlaka hii katika ripoti hii wameeleza wamechunguza tuhuma karibu 21 zinazohusiana na makosa ya kutoa na kupokea rushwa, matumizi mabaya ya ofisi, ukwepaji wa kodi, pamoja na kughushi nyaraka na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni hatua nzuri katika mamlaka hii kwani tukiangalia rushwa kwa kweli ni adui wa haki. Maana yake ukipokea rushwa hutotenda haki. Mhe.Mwenyekiti, rushwa imetawala katika Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Lakini mamlaka hii ina kazi kubwa kwa sababu kazi yao wanayoifanya ni kazi ya ushawishi, kazi ambayo inayoweza kuwatia katika mitihani, mitihani ambayo pengine watashindwa kuepukika.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nilikuwa na ushauri tu kuiomba serikali kuhusiana na mamlaka, naomba izidi kuwezeshwa, kupatiwa vitendea kazi, waangaliwe kimaslahi. Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana nilichangia hivi hivi lakini na leo ninachangia tena. Hivyo ninaomba wapatiwe vitendea kazi ambavyo vitaweza kuwasaidia kufanya kazi zao kwa uadilifu, waongezewe maslahi ili kuepukana na vishawishi mbali mbali ambavyo vinaweza kuwapelekea kuvunja maadili yao ya kazi.

Ninaamini kuna changamoto nyingi kwa sababu kwenda kumchunguza mtu mla rushwa ni kazi. Wewe unakwenda kumchunguza pengine ukifika tu kwanza yeye anakupa rushwa, kwa hivyo ina maana inataka uadilifu, uaminifu katika majukumu yao. Kwa hivyo ninaiomba serikali sana waiangalie mamlaka hii kwa jicho la huruma kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda katika mradi wa kuratibu utekelezaji wa MKURABITA. Katika ripoti imeeleza *page* ya 26, imesema imewezesha kuwatambua wafanyabiashara wadogo wadogo 587 na kupewa mafunzo ya ujasiriamali kwa Wilaya ya Kaskazini B. Hapa nilikuwa na swali niulize, baada ya mafunzo hayo nimuulize Mhe. Waziri kupitia wataalamu wake wamefuatilia na kuona kwamba wajasiriamali hawa baada ya mafunzo hayo, kuna mabadiliko yoyote yametokea katika kuendeleza shughuli au baada ya kutoa mafunzo pengine hawajafuatila kitu chochote. Hapa nilikuwa naomba nipate maelezo kwa sababu ukitoa mafunzo bila ya kufuatilia kuona yale mafunzo yameweza kuwasaidia wale watu, kwa hivyo yale mafunzo yatakuwa hayajawasaidia wajasiriamali hao.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo nilikuwa naomba nipate maelezo kuhusu wameshawapa mafunzo. Je, baada ya mafunzo wamefuatilia wameona labda kuna mabadiliko yoyote au changamoto gani. Hapa nilikuwa naomba nipate maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mradi wa uimarishaji wa nyumba za viongozi na nyumba za serikali. Hii katika kitabu cha hotuba ipo katika *page* ya 56. Wameeleza kuwa kujenga nyumba za viongozi ni muhimu sana Mhe.Mwenyekiti, na pia kuzifanyia matengenezo. Wameeleza kuna nyumba ya Mazizini, Kibweni wataifanyia matengenezo. Hili ni jambo jema Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ukiangalia nyumba za viongozi zikiendelea kukodiwa gharama zinakuwa kubwa.

Hata ukiangalia bajeti ya jana tuliyoipitisha ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, baadhi ya wajumbe wengi wamehoji kuhusu kodi za nyumba. Lakini kama serikali itakuwa na mpango maalum, kuzijenga hizi nyumba za viongozi itapunguza gharama. Pesa ambazo zitalipiwa kodi, ina maana zitasaidia shughuli mbali mbali za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda katika Idara ya Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Kisekta Kupunguza Umaskini. Mhe. Mwenyekiti, hii ipo katika *page* ya 42. Wamesema wametembelea miradi 60 kwa Ungujua na Pemba, na wakasema lengo la ufuatiliaji wa miradi hii ni kufanya tathmini juu ya hatua za utekelezaji wa miradi hiyo kwa kuwa imeendana kama ilivyoainishwa katika mpango kazi.

Hapa nilikuwa nipate maelezo tu. Je, miradi hiyo baada ya kuifuatilia kweli imeandana na mpango kazi, imeleta tija gani, ina changamoto gani. Sasa hapa nilitaka nipate maelezo hayo, kwa sababu hapa imeelezwa tu imetembelea miradi 60 kwa Unguja na Pemba. Nilikuwa naomba nipate maelezo. Baada ya ufuatiliaji huo mumegundua nini kwenye changamoto au mafanikio gani katika miradi hiyo miradi 60 ambayo wameeleza katika hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda katika mradi wa kuratibu utekelezaji wa changamoto za *millennium*. Hotuba imeeleza miradi ya barabara ambayo imekamilika katika kitabu hiki na wamesema kuwa imekamilika kwa mafanikio makubwa kabisa. Naipongeza sana serikali kwa hatua hii na ukiangalia wametaja miradi yenyewe. Kuna mradi wa Kipangani, Kangani, Chwale-Likoni, Mzambarauni-Karim, Mapofu, Bahanasa, hata na Mtambwe. Mhe. Mwenyekiti, ukitizama Mtambwe imo humu mradi wa barabara safi kabisa umekamilika na ninashukuru kuwa umeandikwa katika kitabu hiki cha bajeti. Kwa hivyo ni hongera kwa serikali kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, na mwisho nitakwenda katika Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Ninampongeza sana mwanamama huyu kama wenzangu walivyompongeza anafanya kazi nzuri. Ila anahitaji mashirikiano katika taasisi zote za serikali kwa sababu yeye ana-*deal* na masuala mazima ya ripoti za ukaguzi wa fedha za serikali katika kila wizara. Kwa hivyo hapa ningeziomba hizi taasisi nyengine au wizara nyengine zimpe ushirikiano wa kutosha huyu mwanamama ili afanye kazi kwa majukumu yake ipasavyo.

Pia ninaiomba serikali izifanyie kazi hizi ripoti ambazo Mkaguzi huyu anaziwasilisha. Ninajua kuna mapungufu mengi ambayo anaeleza lakini ninaiomba serikali izifanyie kazi kwa makusudi ili kupunguza na kuondoa kabisa matumizi mabaya ya fedha za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaunga mkono asilimia mia moja hotuba hii. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Marina Joel Thomas lakini kabla nilisema nitamkaribisha Mhe. Machano Othman Said, lakini kabla ya kuja Mhe. Machano, kwanza tumsikilize Mhe. Mohammed Haji Khalid.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kupata fursa hii ndogo ya kutaka kutoa mchango wangu juu Ofisi hii ya Ikulu na Utawala Bora ambayo inaongozwa na Waziri mahiri Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kabla sijatoa mchango wangu kidogo nitakuwa na masikitiko katika bajeti hii viongozi munatuendesha *race*. Kwa sababu katika hotuba zilizokwisha kupita huko nyuma ya bajeti kuu, Makamu wa Pili wa Rais, Makamu wa Kwanza wa Rais ilikuwa kuna watu ambao wanataka kuchangia, lakini wakanyimwa. Lakini kwenye ratiba hii, hii kazi tuliyoifanya leo ilikuwa ianze tarehe 29, hii kazi tunayoifanya hapa kama ratiba hii haina makosa ilikuwa kazi hii ianze tarehe 29.

Kwa sababu mumetubana, leo tarehe 27 tunafanaya kazi ya tarehe 29 Mei, 2014. Kwa hivyo ningeomba ningeweza kufuatilia, kama wachangiaji wapo kama leo wapewe nafasi ya kuchangia kwa sababu bado wakati haujatukimbia.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nianze sasa kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha jioni hii kufika hapa kwa wingi katika Baraza hili, ili kuendeleza kazi zetu za kawaida za kujadili bajeti za serikali. Pili nimpongeze Waziri na watendaji wake kwa kazi kubwa aliyofanya ya kutuandalia kitabu hiki kizuri kilichojaa ufasaha wa lugha na utekelezaji wa shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokuwa na mchango mkubwa. Lakini nataka nianze na Ofisi ya Faragha ya Mhe. Rais katika ukurasa wa 9 unaozungumzia ziara yake ya nje ya Uholanzi, katika kifungu cha 15 naomba nikikariri kidogo hicho kifungu kabla ya kutoa maelezo yangu. Mhe. Mwenyekiti, kinasema hivi;

"Katika ziara ya Uholanzi Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na ujumbe wako walipata fursa ya kutembelea Kampuni ya *Royal Dutch Shell* ambayo Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban na Mwakilishi wa Kampuni ya *Royal Dutch Shell* walisaini waraka wa makubaliano ambao utawezesha kuanza mashirikiano ya kufanya utafiti wa kuwepo kwa mafuta na gesi hapa nchini".

Kwanza nimalizie hapo. Kwa kuanza kufanya utafiti wa mafuta na gesi hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa siku zote sijafahamu kuwa bado utafiti wa kutafuta mafuta na gesi unaendelea. Kwa sababu utafiti huu Mhe. Mwenyekiti, ni wa muda mrefu umeanza tokea nyinyi wengine hamjazaliwa mwaka 1957, ikabainika kuwa yako mafuta katika visiwa vyetu. Lakini sijui kwa njia moja ama nyengine ukawachwa njiani. Katika miaka ya 1980 utafiti huu ukaendelezwa kidogo, ukawachwa njiani na umekuja kuibuka tena katika miaka hii tuliyonayo mpaka ikafika Zanzibar kudai jambo letu hili. Lakini leo hapa kwenye ziara hii ya Mhe. Rais inaonekana kuanzisha utafiti wa kuwepo kwa mafuta na gesi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa hapa sitokuwa na lolote, lakini niulize swali tu. Kwani Mhe. Waziri utafiti huu bado haujakamilika na bado nchi haja yake kuwa na mafuta na gesi ipo au haipo?

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, jambo hili ni la muda mrefu na mimi nilidhania kuwa sasa hivi sio utafiti tena, pengine ni kutafuta kampuni za kuja kufanya hiyo kazi ya uchimbaji, nilidhani hivyo.

Halafu kuna ziara nyengine ya Mhe. Rais aliyofanya nchini India, ambayo nayo kidogo nataka ninukuu sehemu fupi tu. India imekubali kushikana na Zanzibar katika upatikana wa huduma ya maji safi na salama katika mji wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, maji katika nchi yetu imekuwa ni tatizo, kila kampuni na kila nchi tunaiomba kuhusu masuala ya maji na hatimaye bado katika mji huu maji hayajakuwepo ya kutosha. Mhe. Mwenyekiti, sijui kuwa maji Zanzibar yametoweka au vipi. Kwa sababu zamani watu walikuwa wanachimba visima vifupi wanapata maji. Leo tunachimba visima virefu hatupati maji na maji yakitokea na zaidi katika sehemu za mjini yanakuwa ni maji ya chumvi.

Kwa hivyo, ziara hii ya Mhe. Rais ambayo aliambatana na waziri wake Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati itakuwa imezaa matunda fulani, pindipo hawa jamaa zetu wa India ni kweli watakuja kusaidia katika masuala ya maji, wataweza kutupunguzia tatizo kubwa la maji katika mji huu. Lakini pia nina hofu kwa sababu kuna kipindi tuliona kuwa Wajapani wangeweza kuliondoa tatizo la maji katika mji wa Zanzibar. Walifanya walivyofanya, lakini bado tatizo la maji kwa kiasi fulani liko pale pale. Kwa sababu maji bado hayajaenea na katika baadhi ya mitaa bado iko misururu ya watu wanangojea maji. Kwa hivyo, suala la maji ni suala ambalo serikali licha ya kuiachia wizara yenyewe kama hivi inavyofanya, lakini iwe ni kitu cha kipaumbele kwa sababu maji ni uhai.

Mhe. Mwenyekiti, nina msemo wangu wa kawaida kuwa zamani hapa kwetu maji yalikuwa sio tatizo na ilikuwa hakuna mtu akiona tabu kukoga ndoo tatu au nne za maji. Lakini leo hata mimi ambaye sio mtaalamu wa maji, kupita barabarani nikagundua kuwa maji yanapotea ovyo basi yananiuma, kwa sababu watu wanateka maji kwa matumizi ya majumbani na hayapatikani, lakini ukifika pahala maji yanapotea ovyo huwa sio jambo zuri.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu zamani nchi za majangwani walikuwa wanayathamini maji kuliko kitu chochote. Mhe. Mwenyekiti, jambo ambalo huwa nasema mara kwa mara nilipokuwa darasa la saba, niliandikiwa *composition* mwisho wake ilikuwa inasema hivi; *it is only those who live in the desert area that know the value of water*.

Leo watu wa majangwani thamani ya maji hawaijui tena, imegeuka sasa Wazanzibari ndio tunaojua thamani ya maji katika thamani yake ya kweli. Kwa sababu sisi leo ambao zamani tulikuwa na maji sasa hatuna, wale ambao zamani walikuwa hawana maji sasa wanayo. Kwa hivyo sasa na sisi tunaujua umuhimu wa maji. Kwa hivyo, nitaipongeza ziara hii na ofisi hii, pindipo mambo haya ya maji, hao jamaa zetu wa India wakitilia mkazo na kuja kutusaidia katika uwekezaji wa sehemu hii.

Mhe. Mwenyekiti, idara nyengine ni idara ya uhusiano wa kimataifa na uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nchi za nje. Mhe. Mwenyekiti, ofisi ya idara hii imo ndani ya jengo la Ikulu, kama haijahamishwa. Mara moja mimi nilikuwepo katika Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, tuliona kuwa ofisi hii tumo mule, hatusemi kuwa ibadilishwe isiwe ni sehemu ya ofisi ya Rais, lakini iwe nje ya jengo lile, ili watu wengi waweze kwenda na kutoa ushirikiano wao katika ofisi ile. Kuwepo pale kuna watu pengine kuingia mule ndani ya jengo lile la Ikulu sio rahisi, lakini kama ikiwa nje ya pale basi Wazanzibari walio wengi wataweza kwenda na kutoa ushirikiano wao.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kulizungumzwa kuhusu nyumba za viongozi. Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo muhimu na viongozi wakuu Mhe. Mwenyekiti, sio wale wa kisiasa tu. Mimi katika ukanda ninaokaa nakaa na kiongozi mmoja mkubwa sana ni Jaji Mkuu wa Zanzibar, lakini kama ingekuwa hatembei kwa gari kutoka kule nyumbani kwenda kazini, basi buti zake angekuja kuvalia barabara kuu, kwa sababu njia anayotoka maji ni mpaka kwenye futi kwa siku za mvua, anakaa buriani kabisa kabisa. Sasa viongozi kama wale kukaa katika maeneo hayo kwa kweli sio vizuri, ingawaje ni raia lakini ana cheo chengine.

Kwa hivyo, ujenzi na uimarishaji wa nyumba za viongozi, sio lazima wale viongozi wa kisiasa tu, lakini na viongozi wengine wote ambao wana hadhi kubwa katika nchi hii na wao wanastahili watafutiwe makaazi yanayolingana na hadhi yao.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, una dakika tano za ziada.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Mwenyekiti, niitazame kidogo Idara ya Utawala Bora. Nataka kusema jambo dogo tu katika hii Idara ya Utawala Bora, kwenye kifungu cha 55. Kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 Idara ya Utawala Bora ilipangiwa kutekeleza malengo yafuatayo.

Kufanya utafiti mdogo wa utawala bora, kuendeleza kutoa mafunzo juu ya misingi ya utawala bora kwa viongozi wa kisiasa, kiutendaji na wananchi, kutayarisha ripoti ya mwaka ya utawala bora, kutoa elimu ya uraia kupitia redio na televisheni.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Utawala Bora kwa mwaka huu wa fedha itashughulikia mambo hayo manne tu na takriban yote ni ya kutoa elimu. Nahisi mimi kuwa hii idara bado haijapewa kazi hasa ya kufanya. Mimi kwa mtazamo wangu nadhani hii idara ya utawala bora ndio idara kubwa yenye majukumu, kwa sababu nadhani inawezekana mimi maana ya utawala bora siijui. Lakini kama ni hivyo ninavyojua mimi idara hii iwe ni kama idara mama katika ofisi hii, ambayo itaweza kusimamia majukumu ya idara nyengine zote, ili ziende vizuri kisheria na kikatiba katika kutoa haki kwa watu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mohammed Mbwana hapa alipokuwa akichangia alizungumzia juu ya ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali, na alionesha kasoro kubwa zilizomo ya matumizi kinyume na taratibu. Sasa matumizi haya ambayo yanakwenda kinyume na taratibu yanasimamiwa na nani. Mimi nilidhani kuwa utawala bora ungeelekeza namna ya watendaji kuweza kutumia fedha kulingana na sera inavyotakikana, ili utawala bora uwe ni utawala bora na wala isiwe bora utawala. Libakie jina lake halisi la utawala bora, utawala bora ni ule ambao utasimamia utekelezaji wa shughuli za kiserikali kwa ufanisi. Lakini kama baadhi ya watendaji wanafanya watakavyo, basi itakuwa kuna bora utawala, ili tufanye tunavyopenda. Ningeomba waziri usimamie ili huu utawala uwe ni utawala bora kweli wala isiwe bora utawala. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mohammed Haji Khalid. Sasa ni nafasi ya Mhe. Machano Othman Said.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima. Lakini pia nichukuwe fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni yangu katika bajeti hii ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambayo imesomwa na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze pia na Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote, kwa utekelezaji mzuri wa ilani ya Chama cha Mapinduzi, lakini pia utekelezaji mzuri wa bajeti ya mwaka 2013/2014 na ni matarajio yangu kwamba kwa kitabu hiki kizuri, pia kutakuwa na mafanikio katika mwaka 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, bajeti ya ofisi hii ndio bajeti ya ofisi kuu ya serikali, ni Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Nianze pia kwa kumshukuru Mhe. Rais kwa utendaji wake katika kipindi cha miaka 3 kwa 4 sasa, tangu wameanza na utawala wa awamu ya saba. Katika kitabu hiki Mhe. Waziri alieleza kwamba Mhe. Rais amepata fursa ya kutembelea nchi ya Uholanzi na India na ameonana na viongozi mbali mbali. Kwa hakika ziara zake zimeleta tija sana kwa nchi yetu. Makampuni makubwa ya kidunia yameonesha nia ya kuekeza Zanzibar, na tuna matumaini kwamba nchi yetu itasonga mbele kutokana na ziara hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, ukiwacha safari za nje Mhe. Rais pia amekuwa na utamaduni mzuri sana. Kila mwaka Mhe. Rais wetu anatembelea Mikoa yote ya Zanzibar kwa Unguja na Pemba na wilaya kwa wilaya. Ni utaratibu ambao kajiwekea na hakuna mwaka ambao ume-*fell,* kila mwaka anafanya na ziara zake zinaleta hamasa sana kwa wananchi.

Kwa hivyo, hatuna budi kumshukuru sana. Suala hili litasaidia kuinua uchumi wetu, lakini pia kuimarisha ustawi wa jamii na kuweka amani na utulivu katika nchi. Nchi yetu hii kila wakati anatakiwa kiongozi afanye ziara za kuonana na wananchi, afanye ziara ya kuonana na wafanyabiashara na afanye ziara ya kuonana na watu mbali mbali kwa maslahi ya kiuchumi, kisiasa, lakini pia kiustawi wa jamii.

Mhe. Rais kwa kupitia pia Baraza la Mapinduzi aliongoza vikao vingi, kwenye kitabu hiki vimeelezwa kama 18, lakini hivyo vikao 18 vyenyewe wakati mwengine ni vya siku mbili na kawaida ni siku mbili, kwa hivyo ni vikao vingi.

Mhe. Mwenyekiti miswada yote kama kuna mafanikio ya Baraza la Wawakilishi katika kupitisha miswada ya sheria na kutunga sheria, basi kilele cha mwenye mafanikio makubwa na Mhe. Rais, maana hakuna mswada ambao utakuja hapa bila kuzungumzwa na kujadiliwa na Baraza la Mapinduzi na Baraza la Mapinduzi Mwenyekiti wetu ni Mhe. Rais. Kwa hivyo, tumpongeze pia kwamba anaiendesha serikali vizuri, kwa uwazi na kwa mashirikiano ya hali ya juu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie Ofisi ya Mipango ya Serikali na hapa naomba nichanganye na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu. Kwa sababu ili uwe na mipango bora ni lazima uwe na takwimu nzuri. Kwanza nimshukuru Katibu Mtendaji na timu yake, Katibu Mipango na nimshukuru pia na Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, taasisi hizi katika kipindi kilichopita zilikuwa chini ya Wizara ya Fedha, lakini kwa kawaida hata kwa wenzetu jirani, vinakuwa katika Ofisi ya Rais ili kupata nguvu zaidi za utendaji na kupanga mipango mizuri ya uchumi wa nchi.

Sasa Mtakwimu Mkuu anazo takwimu mbali mbali za nchi yetu. Mfano, idadi ya wakazi na idadi ya miundombinu ya taasisi mbali mbali kwa hivyo ni rahisi kupitia kwake kuweza kupata takwimu sahihi na kupeleka kwenye mipango ya maendeleo ili nchi yetu isonge mbele. Mathalan katika sensa ya 2012 kwa Mkoa wa Mjini Magharibi zipo baadhi ya Shehiya ambazo zina wakaazi wasiopungua 26,000 mpaka 35,000. Lakini kuna shehiya nyengine katika nchi hii hii ya Zanzibar zina kati wa watu mia 400 na 700, sasa kama hakuna mipango maalum ya kutambulikana unaweza kuona kama maendeleo hayapo kwa upande mmoja. Kwa sababu mfano katika skuli zetu kuna maeneo wanafunzi wanaingia asubuhi na jioni lakini bado madarasa yao ni makubwa sana na yanazidi uwezo wa kawaida wa madarasa ya skuli. Lakini kuna maeneo wanaingia asubuhi tu mkondo mmoja tu lakini madarasa yao pengine hayazidi wanafunzi 60 au 70.

Sasa haya mambo kwa kupitia Ofisi ya Mtakwimu Mkuu na kwa kushirikiana na Tume ya Mipango ndio Serikali inafanya kazi na ndio maana kunakuwa na miradi mipya ya ujenzi wa maskuli, hospitali na mambo mengine, kwa hivyo naipongeza na napongeza uamuzi wa Serikali kwamba kufanya mabadiliko ya kuirekebisha muundo wake na taasisi hizi kupelekwa katika Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, pia nizungumzie kwa ufupi taasisi ambayo wenzangu wameizungumza sana nayo ni Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi. Mimi niombe wenzangu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba inatupasa tuwape moyo taasisi hii au mamlaka hii, kwa sababu umri wake wa kuanzishwa kwake hauzidi miaka miwili kwa hivyo taasisi hii inajengwa na ni taasisi ngumu, nimemsikia Mhe. Marina Joel Thomas alisema pale, huo ukamataji wa rushwa na utoaji wa rushwa ni mgumu sana kuthibitika na kwa bahati nzuri pia taasisi hii ipo lakini pia tunazo taasisi za utawala bora, na kwenye utawala bora kila mtu lazima apate haki ya kujieleza na kusikilizwa.

Sasa taasisi hii ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa inahitaji kuungwa mkono lakini pia inahitaji kwanza kupata muda wa kujijenga na kuwa na *man power* ya kutosha kwa wafanyakazi wake ili waweze kwenda sambamba na matukio mbali mbali ya kihalifu katika rushwa na uhujumu uchumi.

Maana wakati mwengine rushwa sio lazima fedha rushwa inaweza kuwa kwenye ajira, rushwa inaweza kuwa katika sehemu mbali mbali katika taasisi, na rushwa sio lazima ndani ya Serikali tu rushwa inaweza kuwepo nje ya Serikali na zinaendeshwa na watu wengine ambao hawapo moja kwa moja kwenye Serikali. Kwa hivyo mimi nina matumaini na hii taasisi au mamlaka hii kwamba baadae taasisi hii inaweza kutusaidia sana.

Lipo tatizo ambalo litaweza kuwakwaza kidogo, ni tabia yetu Wazanzibari pengine ya kufanyika jambo kama ovu lakini ushahidi wale ambao wameshuhudia inakuwa ni ngumu sana kujitokeza kwenda kutoa ushahidi kwa masuala kama haya. Sasa kama tutajirekebisha na tutakuwa sasa tumeamua kwamba kwa ujumla wetu, maana tukisema vita hivi viendeshwe na mamlaka peke yake hilo jambo litakuwa gumu sana, lakini kama tutaamua sasa basi na kila mmoja atathaminiwa na taasisi, maana wakati mwengine taasisi zinavyofanya tathmini inawezekana sie sie tukaanza kupiga kelele, kwamba mbona tunaingiliwa, mbona mambo haya yako hivi. Kwa hivyo nafikiri ikiwa tumeshakuwa tayari basi mambo haya yanaweza kwenda mbele.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho niipongeze Ofisi ya Mhe. Rais kwanza kwa mambo mawili au matatu kwanza kwa kuweza kuendeleza mradi wa ujenzi wa majengo mbali mbali yaliyokuwa chini ya Ofisi hii, kwenye kitabu hiki imeelezwa kwamba Ofisi za Baraza la Mapinduzi ambazo zipo pale *People's Palace* mwaka jana au bajeti hii ambayo tunamalizia zimefanyiwa matengenezo na ni matengenezo ya maana sana, yanaridhisha na mpaka sasa Tume ya Utumishi Serikalini ipo pale kwa sababu majengo yale yamefanyiwa marekebisho makubwa.

Pia kuna huu mradi wa kutengeneza nyumba za Ikulu Unguja, Pemba, Dar es Salaam na Dodoma nao huu ni mradi mzuri na unastahiki kuungwa mkono na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tupitishe bajeti yao, ili sasa nyumba zote ambazo zipo chini ya Ofisi ya Rais ziweze kuwa katika hali bora na ziweze kutumika ipasavyo, ikiwemo nyumba ya Kibweni, pia ambayo ilizungumziwa asubuhi. Nafikiri nayo inastahiki kufanyiwa marekebisho katika hali nzuri ya kiserikali.

Mwisho kabisa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chumbuni naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia na naomba waheshimiwa wenzangu tuunge mkono bajeti hii ya Mhe. Rais ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.*(Makofi)*

Mhe. Salma Mussa Bilali: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii. Kwanza kabisa na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha mbele ya baraza lako hili tukufu kuchangia angalau machache ya hotuba hii ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze ukurasa wa 35 Mamlaka ya Kuzuia Rushwa, wajumbe wengi sana wameshazungumza, wameshachangia kipengele hiki lakini na mimi angalau kwa uchache naomba nichangie kama ifuatavyo;

Mhe. Mwenyekiti, naomba niipongeze sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuanzisha taasisi hii ya Mamlaka ya kuzuia rushwa. Mamlaka hii bado ni changa na inafanya kazi katika mazingira magumu, hivyo basi naomba Serikali kuangalia vizuri taasisi hii kwa hali zote ili iweze kutekeleza majukumu yake vizuri na kwa maslahi ya nchi yetu. Kutokana na changamoto nyingi ambazo zinaikabili Taasisi hii katika utekelezaji wa majukumu yake taasisi hii naiomba Serikali kwa makusudi iongezee bajeti taasisi hii, ili iweze kutekeleza majukumu yake vizuri na kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti naomba niende kwenye ukurasa wa 38 kipengele cha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa ruhusa yako naomba kwa dhati kabisa nimpongeze Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa kazi ngumu. Naomba nimpongeze mama Fatma; mama ambaye ni mahiri kabisa na mama mchapa kazi kwa kazi ngumu anayokabiliana nayo na kusema kwamba mama huyu anaweza, lakini Mhe. Mwenyekiti anahitaji kuwezeshwa zaidi, ili aweze kutekeleza majukumu yake ya utekelezaji wa majukumu yake, na kuhakikisha kwamba kunakuwepo matumizi mazuri ya rasilimali ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi hii inakabiliwa na changamoto nyingi changamoto ambazo wenzangu wengi ambao wamechangia wameshazizungumza, changamoto ya kwanza ni ufinyu wa bajeti, pili upungufu wa wataalamu, nyengine ni *Scheme of service* ya wafanyakazi wa Ofisi hii, naomba Serikali au naomba Wizara kwa makusudi iangalie vizuri bajeti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali hasa ukizingatia kwamba Ofisi hii ina majukumu makubwa, ina majukumu mazito, na ina majukumu ya fitna.

Kwa hivyo naomba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri aiangalie tena bajeti ya Wizara ya hii waongezewe ili waweze kufanyakazi kwa ufanisi. Ofisi hii pia inakabiliwa na changamoto ya wataalamu wa fani mbali mbali, kwa hivyo naomba Wizara yako kupitia Tume ya Utumishi iwaruhusu au iruhusu ofisi hii iweze kuajiri wafanyakazi wataalam, ili Ofisi hii iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi, ili iweze kudhibiti zaidi fedha na upoteaji wa fedha za Serikali na iweze kufanikisha zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba Serikali kupitia Ofisi yako katika hotuba yako umesema kwamba *Scheme of service* imeshaangaliwa na itafanyiwa kazi, lakini ni siku nyingi inazungumzwa lakini bado haijafanyiwa kazi. Mhe. Mwenyekitik ukosefu wa wataalamu Ofisi hii unatokana pia kutokana na hii *scheme of service* kwamba haipandi ya ofisi hii. Wataalamu hata kama watatangaziwa, hata kama wataombwa waombe lakini kama hakutakuwa na maslahi mazuri ya wafanyakazi basi kila siku itakuwa hiyo ni nyimbo kama wimbo wa taifa. Tunahitaji wataalamu, lakini hawatapatikana kwa sababu wataona ni bora kwenda katika taasisi ambazo watapata maslahi, waweze kukidhi mahitaji yao kuliko kuja katika Ofisi ambayo watakuwa wanashindwa kutekeleza majukumu yao ya kazi halafu pia ya majumbani mwao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo naiomba Serikali iangalie kwa umakini umuhimu na uzito wa Ofisi hii na naomba kwamba wapatiwe maslahi stahili au stahiki, ili waweze kuchapa kazi vizuri zaidi na kwa udhibiti wa mali za umma, ili zisiweze kupotea na Serikali iweze kupata mapato zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi nimesema sitokuwa na mengi ya kuchangia katika bajeti hii lakini kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Unguja naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora, mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kushinda leo kutwa nikiwa salama pamoja na wenzangu wote waliomo katika baraza hili, pamoja na viongozi wengine waliopo juu hapo tukawa tunaisikiliza bajeti hii namna inavyochangiwa.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nije kwanza kwa kumsifu mwana mama mwenzetu kwa kazi zake kubwa anazozifanya, ingawaje nimeingia kwa muda mfupi tu katika kamati hii ya *PAC* lakini nimeona juhudi zake mama huyu anavyozifanya, hana uchungu wala hana kinyongo hili nimpongeze sana.

Pia nije katika ukurasa wa tano unaosema kwamba Shabaha ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, katika kifungu cha sita kinasema kwamba kuengeza mchango Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi katika shughuli za kimaendeleo ya kijamii Zanzibar. Hapa mimi niseme kuwa tangu kuanzishwa kwa *dyer scholar* Wazanzibari wemafaidika vipi kuisaidia Zanzibar katika pato la taifa hili, nimuulize Mhe. Waziri.

Vile vile nikija katika ukurasa wa saba kifungu cha 11 kinasema kwamba kufanya utafiti juu ya mchango wa Wazanzibari wanaoishi nchi za nje na maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Zanzibar, lakini nimuombe Mhe. Waziri anifafanulie kwa sababu katika kifungu hiki cha 6 kinasema kuongeza mchango wa Wazanzibari, lakini katika kifungu cha 11 kinasema kwamba kufanya utafiti juu ya mchango wa Wazanzibari wanaoishi nchi za nje. Naomba Mhe. Waziri aweze kunifafanulia.

Pia Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 6 unaosema kifungu cha 5 unasema kuanzisha Ofisi ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa nchi kwa uchumi Pemba, niseme kwamba katika kipindi cha miaka yote 50 bado kitengo cha Kuzuia Rushwa Pemba na wahujumu wa nchi wa uchumi bado hakijaanzishwa, ina maana kuanzia kipindi chote hicho Mhe. Mwenyekiti, haijawahi kuripotiwa kesi ya rushwa mpaka sasa hivi, wakati kesi nyingi zinazokamatwa Pemba na kwa mfano kama za karafuu kukamatwa, lakini leo katika kitabu chake hiki Mheshimiwa kinasema kwamba kuanzisha Ofisi ya mamlaka ya kuzuia rushwa Je, hizi pesa ambazo zinatengewa katika mamlaka hii huwa zinatengewa kwa kitu gani.

Mhe. Mwenyekiti nije katika mradi wa uimarishaji wa nyumba za viongozi, niseme kwamba sote humu tunafahamu kwamba viongozi huwa wanatengewa nyumba ambazo za kuishi, lakini mwaka juzi na mimi niliwahi kusema vile vile iko haja ya kujengewa viongozi au kutengewa sehemu ya viongozi kujengewa nyumba ambazo wakaweza kuishi bila ya matatizo bila ya vurugu.

Vile vile niseme kwamba hapa sisi tunafahamu kwamba Ikulu ni nyumba ya makaazi na nyumba ya makaazi hii ni nyumba ya viongozi ambao walioko juu wa kitaifa, leo inakuwaje baadhi ya viongozi wanapokwenda sehemu ya upande wa pili wa Muungano huwa wanalala katika hoteli. Mhe. Mwenyekiti hebu atueleze hii kwa nini wakati nyumba zipo na hawapewi nyumba zile wakaweza kuishi.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika ukurasa wa 42 unasema kwamba Idara ya Mipango ya Kitaifa ya Kimaendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umasikini, niseme kwamba kwa kuwa asilimia kubwa ya Wazanzibari ni masikini na kwa kuwa Tume ya Mipango imeunda Idara tatu ikiwemo idara ya Mipango Maalum ya Kupunguza umasikini. Je, Serikali imejipanga vipi kupambana na umasikini na pia katika kupanga hiyo mipango imewafikia vipi walengwa kwa kiasi gani? Mhe. Mwenyekiti, hapa namuuliza Mheshimiwa Waziri aweze kunijibu.

Pia Mhe. Mwenyekiti, nije ukurasa wa 55 unaosema utawala bora, kwa kuwa bado itanitatiza Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba Mhe. Waziri atafahamu utawala bora kifungu cha 55 kinasema kwamba kuanzishwa kwa elimu katika vituo, hii nimeikosea kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, niseme Televisheni imeandaa vipindi vingi na ambavyo vyengine wananchi huwa wanashindwa hata kuvitizama, kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, Je, Serikali haioni kuna haja ya kuanzishwa somo la uraia maskulini katika skuli za *Primary* na *Private* ili wafaidike na somo hili wananchi hawa na kuachana na kutumia TV na redio ambazo kila siku watu hawa wanazingalia. Naomba na suala hili Mhe. Waziri alichukue.

Mhe. Mwenyekiti baada ya hapo niseme ahsante sana nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kwa kadiri ya orodha ambayo ilikuwa imefika hapa na wajumbe wakataka kuchangia kwa sasa ndio imemalizika, na tukiangalia muda kwa ajili ya kumkaribisha Mhe. Waziri, ili aweze kufanya majumuisho dakika tulizonazo ni chache hazitoweza kutosha. Kwa hivyo basi nafikiri itakuwa jambo la msingi na jambo la busara tukamuacha Mhe. Waziri akenda kukaa pamoja na timu yake, ili wakaweza kutengeneza utaratibu mzuri wa kuja kutupatia majibu siku ya kesho asubuhi na baadae tuweze kupitisha vifungu kwa umoja wetu.

Kwa sasasa hivi na kwa dakika zilizokuwa zimebaki kama dakika 25 hivi mpaka 30 labda nichukue fursa hii tumuombe Waziri pale na kwa muda mrefu Mhe. Said Ali Mbarouk anakaimu hiyo nafasi na kwa sasa Mhe. Haji Omar Kheri yupo pale, kwa hivyo mtakubaliana hapo ili muweze kutoa hoja tuweze kuahirisha baraza ambalo wakati wake haujafika na baadae shughuli zetu tuweze kuendelea nazo kesho.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa muda wa kumalizika Baraza la Wawakilishi haujafika na kwa kuwa wachangiaji wa Hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wamemalizika, naliomba Baraza lako Tukufu likubali kuliakhirisha Baraza hili kabla ya muda wake hadi kesho tarehe 28/05/2014 Saa 3:00 Asubuhi.

Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 1:25 Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 28/05/2014 Saa 3:00 Asubuhi)